**15 APRILI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Sita – Tarehe 15 Aprili, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 05 la tarehe 02 Februari, 2024;
2. Toleo Na. 06 la tarehe 09 Februari, 2024;
3. Toleo Na. 07 la tarehe 16 Februari, 2024;
4. Toleo Na. 08 la tarehe 23 Februari, 2024;
5. Toleo Na. 09 la tarehe 01 Machi, 2024;
6. Toleo Na. 10 la tarehe 08 Machi, 2024;

7. Toleo Na. 11 la tarehe 15 Machi, 2024;
8. Toleo Na. 12 la tarehe 22 Machi, 2024;
9. Toleo Na. 13 la tarehe 29 Machi, 2024; na
10. Toleo Na. 14 la tarehe 05 Aprili, 2024.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:**

(a) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30, Juni 2023;

(b) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30, Juni 2023;

(c) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30, Juni 2023;

(d) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30, Juni 2023;

(e) Ripoti ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalum kwa kipindi kinachoishia tarehe 30, Juni 2023;

(f) Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA;

(g) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Upatikanaji wa Huduma za Afya ya Akili *(Performance Audit on Availability of Mental Healthcare Services);*

(h) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Udhibiti wa Vifaatiba katika Hospitali na Vituo vya Afya vya Umma *(Performance Audit on Regulation of Medical Equipment in the Public Health Facilities)*;

(i) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Udhibiti wa Mazao ya Biashara *(Performance Audit on Regulation of Cash Crops);*

(j) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Udhibiti wa Usambazaji wa Mbolea kwa Wakulima *(Performance Audit on the Management of Distribution of Fertilizers to Farmers);*

(k) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Udhibiti wa Elimu ya Ufundi Nchini *(Performance Audit on Regulation of Technical Education);*

(l) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Urejeshaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu *(Performance Audit on the Management of Higher Education Students' Loan Repayment);*

(m) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Uendelezaji, Ufuatiliaji, na Tathmini ya Umahiri wa Watumishi katika Sekta za Umma *(Performance Audit on Development, Monitoring and Evaluation of Competency of Staff in the Public Sector);*

(n) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utekelezaji wa Programu za Urekebu kwa Wafungwa *(Performance Audit on the Implementation of Prisoners Rehabilitation Programmes);*

(o) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mipango Miji *(Performance Audit on the Management of Town Planning);*

(p) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi na Ufuatiliaji wa Watoa Huduma za Bima Nchini *(Performance Audit on Supervision and Monitoring of Insurance Service Providers);*

(q) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Fukwe *(Performance Audit on the Management of Beaches);*

(r) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Uwezeshaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini *(Performance Audit on the Provision of Support to Small Scale Miners);*

(s) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi *(Performance Audit on the Management of Fisheries Resources);*

(t) Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Uingizaji wa Mafuta Nchini *(Performance Audit on the Management of Imported Petroleum);*

(u) Taarifa kuhusu Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi Yaliyotolewa Mwaka 2020 *(Follow-up Report on the Implementation of the Performance Audit Recommendations issued in the Year 2020)*.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda kwenye maswali, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi.

Na. 66

**Ujenzi wa Bwalo Sekondari ya Malagarasi**

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa Bwalo katika Sekondari ya Malagarasi - Muhambwe lililosimama tangu mwaka 2017?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka wa Fedha 2016/2017, Serikali ilitoa shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa Bwalo la Chakula katika Shule ya Sekondari Malagarasi. Fedha hiyo ilitumika kukamilisha kazi za ujenzi wa bwalo na hadi sasa lipo katika hatua za umaliziaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa baadhi ya miundombinu ya bwalo hilo haijakamilika kujengwa. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga bajeti ya shilingi milioni 187 kwa ajili ya kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Bwalo katika Shule ya Sekondari Malagarasi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Kwanza nashukuru Serikali kwa kutenga fedha hizi kwa ajili ya kumalizia bwalo hili la Shule ya Malagarasi, hata hivyo, nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; shule hii imeanza mwaka 1995 baada ya wananchi kujenga madarasa sita, madarasa haya hayajawahi kufanyiwa ukarabati. Je, ni lini Serikali itatenga fedha ili kukarabati madarasa ya shule hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; shule hii ina zaidi ya wanafunzi 1,240 ikiwa ni kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha sita na wanafunzi takribani 418 wa kidato cha sita hawana mabweni. Je, ni lini Serikali itajenga mabweni angalau mawili kwa ajili ya mabinti wetu katika shule hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyowapambania wananchi wake. Swali lake la kwanza, kuhusu ukarabati wa madarasa chakavu, napenda Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba Serikali inatambua uwepo wa shule chakavu za msingi na sekondari na ndio maana Serikali tayari imeshaanza ukarabati wa shule hizo kupitia miradi ya *EP4R, SEQUIP* na *BOOST*. Serikali kwa kutambua uhitaji na kwa kadri fedha zitakapokuwa zikipatikana, Serikali inakusudia kuja kufanya marekebisho katika shule yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, ambapo Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kuhusu ujenzi wa mabweni na hasa kwa wasichana. Mheshimiwa Mbunge naomba ufahamu Serikali inatambua kwamba kuna umuhimu wa kupata mabweni na hasa kwa watoto wa kike na ndio maana Serikali ilianza ujenzi wa shule za sekondari za bweni za wasichana katika kila mkoa kupitia Mradi wa *SEQUIP*. Kwa hiyo, kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na mabweni na hasa kwa watoto wa kike Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni hayo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja fupi. Shule ya Msingi Igumila madarasa yake mawili yamebomoka na Naibu Waziri Utumishi alipopita pale alituahidi kutupa madarasa mawili. Je, ni lini fedha hizo zitapelekwa ili turejeshe hayo madarasa mawili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge kutambua uhitaji wa madarasa katika Shule ya Msingi Igumila, Serikali inaendelea kuangalia vipaumbele na kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa

madarasa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itafanya jitahada kwa kadri fedha zinavyopatikana iweze kujenga madarasa haya. Ahsante

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Justin Nyamoga.

Na. 67

**Sekondari ya Kilolo kuwa ya Kidato cha Tano na Sita**

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapandisha hadhi shule ya Sekondari Kilolo kuwa ya Kidato cha Tano na Sita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Wilaya ya Kilolo ina tarafa tatu ambazo ni Kilolo, Mazombe na Mahenge ambazo zote zina Shule za Kidato cha Tano na Sita. Shule hizo ni: Udzungwa Sekondari (Kilolo); Ilula Sekondari (Mazombe) na Lukosi Sekondari (Mahenge) ambayo imepandishwa hadhi mwaka huu 2024 na inatarajiwa kuanza Julai, 2024, baada ya Serikali kupeleka shilingi milioni 260 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uwepo wa shule hizo, Serikali itaendelea na mpango wake wa kupandisha hadhi Shule ya Sekondari ya Kilolo kuwa na kidato cha tano na sita kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyamoga.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nashukuru kwa majibu, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; shule hii ilitembelewa na Mheshimiwa Rais wakati akiwa Makamu wa Rais na kuahidi kuipandisha hadhi mbele ya wadau na wadau hao tayari wameshakamilisha ujenzi wa madarasa. Je, Serikali wakati inaendelea kutafuta fedha haioni sababu ya kuwaomba wadau hao hao kukamilisha ujenzi wa mabweni ili shule hiyo iweze kuanza kwa sababu wako wadau ambao tayari wamejenga madarasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Shule ya Sekondari Ilula iliyotajwa kama yenye kidato cha tano na sita, mabweni yake yametitia kutokana na mvua na kuwa hatarishi kwa watoto wanaosoma pale. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuongozana na mimi kwenda kujionea hali hiyo na kuchukua hatua za dharura?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa natambua jitihada anazozifanya Mheshimiwa Mbunge kuwapigania wananchi wake. Kuhusu swali lake la kwanza ambapo anasema Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya ujenzi wa mabweni basi na yeye ameweza kutoa maoni kwamba Serikali itazame namna ya kushirikiana na wadau katika kukamilisha mabweni hayo. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge mawazo yake ni mazuri na Serikali imeyapokea na tutayachakata na kufanya mawasiliano na wadau ili tuone kwamba kwa pamoja Serikali na wadau tunaweza kujenga mabweni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuhusu bweni kuzama na nipo tayari kuambatana naye kwenda kuona hali halisi na kuchukua hatua za dharura. Nakubali Mheshimiwa Mbunge kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, ahsante

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa kukubali. Mheshimiwa Suma.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** ...tutaongozana ili twende kuona mazingira ya shule hiyo.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itaipandisha hadhi Shule ya Sekondari ya Lukoto iliyoko katika Wilaya ya Rungwe ukizingatia sekondari hiyo imezungukwa na kata ambazo na zenyewe zina uhitaji wa shule hiyo na kata zenyewe ni Kata ya Ikuti, Kimo, Masukuru, Bagamoyo, Suma na Sheli ya Masukuru?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Rungwe aweze kwenda kufanya tathmini katika shule aliyoitaja Mbunge ili kutazama miundombinu na kuweza kuona kama miundombinu inakidhi vigezo vya kupata usajili wa kidato cha tano na sita. Baada ya kukamilisha tathmini hiyo waweze kuwasilisha maombi katika Wizara ya Elimu kwa ajili ya taratibu za kupata usajili wa kidato cha tano na sita. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru kwa niaba yake Mheshimiwa Ritta Kabati.

Na. 68

**Kutenga Bajeti kwa ajili ya Taulo za Kike Mashuleni**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. NORAH W. MZERU** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali kutenga Bajeti kwa ajili ya Taulo za kike shuleni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuratibu upatikanaji wa taulo za kike kupitia fedha zinazotokana na ruzuku ya uendeshaji *(Capitation Grants),* wadau pamoja na mapato ya ndani ya halmashauri ambapo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, shilingi bilioni 3.16 zilitumika kugharamia taulo za kike. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1.97 zilitoka katika ruzuku ya uendeshaji, shilingi milioni 539 zilitoka katika mapato ya ndani ya halmashauri na shilingi milioni 655 zilitoka kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali ilitenga shilingi bilioni 2.64 kwa ajili ya kugharamia taulo za kike. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1.06 ni za ruzuku ya uendeshaji na shilingi bilioni 1.58 ni fedha kutoka mapato ya ndani ya halmashauri. Hadi Machi, 2024 shilingi bilioni 2.2 zimetumika. Pia, wadau mbalimbali walichangia jumla ya shilingi bilioni 1.5 na Miradi ya Shule ya Elimu ya Kujitegemea ilichangia shilingi milioni 119.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuzisisitiza halmashauri zote nchini kuhakikisha zinatenga bajeti kwa ajili ya upatikanaji wa taulo za kike shuleni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwanza kabisa nipongeze majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusiana na taulo za kike. Pamoja na kwamba Serikali zinatenga hizo fedha halmashauri, lakini bado kuna malalamiko makubwa sana katika shule zetu. Je, utaratibu gani unatumika kuhakikisha kwamba hizi fedha zinatengwa na hizi taulo zinawafikia wadau wanaotakiwa kupatiwa fedha hizi kwa sababu siku zote ukienda katika shule zote huoni kabisa taulo za kike?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kuhusiana na swali la Mheshimiwa Mbunge, nataka kumhakikishia kwamba, fedha hizi zinatoka. Nachukua nafasi hii kuwaagiza wakurugenzi wote wa halmashauri kusimamia kwa umakini zoezi hili, ili fedha hizi zinazotengwa kwa ajili ya kupata taulo za kike ziweze kusimamiwa kwa ufanisi na kuleta tija. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Ni nini mkakati wa Serikali wa kupunguza kodi kwa malighafi ambazo zinatumika kutengeneza taulo za kike, ili taulo hizi sasa ziweze kutengenezwa shuleni kwa kupitia somo la maarifa ya jamii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba arudie swali lake.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni nini mkakati wa Serikali wa kupunguza kodi kwa malighafi ambazo zinatumika kutengeneza taulo za kike ili kuwezesha mafunzo ya kutengeneza taulo za kike kufanyika katika somo la maarifa ya jamii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokea mawazo mazuri ya Mheshimiwa Mbunge na tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili kuangalia masuala haya ya kikodi na kuona kinachoweza kufanyika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Vincent Mbogo, kwa niaba yake Mheshimiwa Kapinga.

Na. 69

**Kugawanya Kata ya Nkasi**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA K.n.y MHE. VINCENT P. MBOGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itazigawa Kata za Chala, Kala na Ninde Nkasi kwa kuwa ni kubwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala huzingatia Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Wilaya, Sura ya 287 na Mamlaka za Miji, Sura ya 288, pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uhitaji wa kugawa baadhi ya maeneo mapya ya utawala, lakini kwa sasa Serikali imetoa kipaumbele katika kuboresha na kukamilisha miundombinu kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baadaye kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kipaumbele hiki cha Serikali, sisi wawakilishi wa wananchi kwenye maeneo haya tunaona kuna uhitaji wa kugawanya haya maeneo. Mazingira ya Kata hizi za Nkasi yanafanana kabisa na Kata za Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Kata ya Mkumbi, Kata

ya Nyoni, Kata ya Langilo na Kata ya Maguu. Je, Serikali inatoa kauli gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Kapinga kwa kufuatilia uanzishaji wa maeneo mapya ya utawala katika Halmashauri ya Mbinga Vijijini. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala kwa sababu, yanasogeza huduma za jamii karibu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku ni lazima tuwe na vipaumbele. Tuna majengo mengi ya wakuu wa wilaya hayajakamilika, majengo ya utawala ya halmashauri, ofisi za kata na maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, Serikali kwa sasa kwanza itakamilisha miundombinu hiyo ili ofisi hizo ziweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi kwa wananchi na baadaye tutakwenda kuanzisha maeneo mapya ya utawala. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala hilo litafanyiwa kazi wakati utakapofika. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, Kata hii ya Chala na Ninde iko Wilaya ya Nkasi na Serikali imekuwa ikitoa kauli mara kwa mara kwamba, hakuna mpango wa kuongeza maeneo ya kiutawala; kuongeza maeneo ya kiutawala ni takwa la kisheria. Je, ni lini Serikali itatekeleza agizo hili la kisheria kwa maeneo ambayo yamekidhi vigezo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali

haijawahi kutamka kwamba haina mpango wa kuongeza maeneo ya utawala. Serikali imetamka kwamba, imeweka vipaumbele, kwanza kukamilisha majengo ya utawala yaliyopo katika mamlaka zilizopo na hatimaye tutakwenda kuanzisha maeneo mapya ya utawala. Kwa hiyo, hakuna sehemu ambayo tumetamka kwamba, hatuanzishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mbunge kwamba, kwanza tunaendelea kukamilisha miundombinu iliyopo na baadaye tutakwenda kutoa kipaumbele kwenye kata aliyoitaja na maeneo mengine ambayo yatakidhi vigezo ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zedi, ajiandae Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Serikali itakapokuwa tayari kuanzisha maeneo mapya ya kiutawala, je, itakuwa tayari kuzingatia na kutoa kipaumbele kugawanya Kata za Igusule, Mambali na Semembela ambazo maombi yake yalishatolewa na mchakato ulishaanza mpaka umefika hatua ya *RCC*? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itakapokuwa tayari kuanzisha maeneo mapya ya utawala, itaanza na *first in, first out*. Kwa hiyo, naipongeza Halmashauri ya Nzega kwa kuwasilisha maombi hayo na pia, halmashauri nyingine ambazo zimeshawasilisha. Tutakapoanza kutoa nafasi hizo, basi tutawapa kipaumbele wale waliowasilisha mapema zaidi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, Serikali ilishatoa *GN* ya Mwaka 1992 kwa

ajili ya kuupandisha Mji wa Sengerema kuwa Halmashauri ya Mji. Katika halmashauri 21 zilizopandishwa kuwa mamlaka kamili za miji, Sengerema siyo mojawapo. Je, ni lini Sengerema itakuwepo kwa sababu, ilibakia peke yake? Ni nini Kauli ya Serikali kuhusu Halmashauri ya Mji wa Sengerema kwa sababu, huko jimboni imekuwa ni tabu kwangu na muda umeisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliainisha mamlaka za miji midogo ambazo zimeanzishwa kote nchini zinazosubiri kukidhi vigezo na kuwa halmashauri za miji. Kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Tabasam kwamba, Halmashauri ya Mji Mdogo wa Sengerema, kama imewasilisha maombi na Serikali inatambua uwepo wa mamlaka ya mji huo, muda ukifika wa kupandisha hadhi, tutakwenda kupandisha hadhi halmashauri hizo ambazo kimsingi zitakidhi vigezo vinavyotakiwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Joseph Kamonga.

Na. 70

**Zahanati ya Madope na Ludende kuwa Vituo vya Afya**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kupandisha hadhi Zahanati za Madope na Ludende kuwa Vituo vya Afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Zahanati za Madope na Ludende ni zahanati zilizopo kwenye Makao Makuu ya Kata za Madope na

Ludende mtawalia. Zahanati ya Madope ina eneo la takribani ekari 10, pamoja na vigezo vingine, inakidhi kuwa kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Ludewa itatenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuongeza majengo na kuanza utaratibu wa kuipandisha hadhi Zahanati ya Madope kuwa kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zahanati ya Ludende haikidhi vigezo vya kuwa kituo cha afya kwa kuwa, ina eneo dogo na uchache wa watu na pia, inapakana na Kituo cha Afya cha Mlangali na vingine. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu ya Serikali, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; wananchi wa Kijiji cha Chanjale kilichopo Kata ya Lumbila, baada ya kuona wanatembea kilometa 22 kufuata huduma za zahanati, mwaka 2014 walianza kujenga zahanati yao, lakini hadi leo haijakamilika. Je, ni ipi kauli ya matumaini kutoka kwa Serikali juu ya Zahanati hii ya Chanjale ili wananchi waweze kupata huduma?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; wananchi wa Kata ya Madope ambao wako 9,000 wanakaribia 10,000 na wao walianza jitihada za kujenga kituo cha afya ambacho Serikali ilituma wataalam kutoka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenda kukagua, wakaahidi kuwa watapeleka fedha kutoka Benki ya Dunia, lakini mpaka leo ikiwa ni mwaka wa pili bado hiyo fedha haijaenda. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha hiyo ili kukamilisha Kituo cha Afya cha Kata ya Madilu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu

Spika, kwanza naomba kutumia nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Kijiji cha Chanjale kwa kuchangia nguvu zao kwa ajili ya ujenzi wa zahanati. Naomba kuwapa habari njema kwamba, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesikia kilio chao kupitia kwa Mheshimiwa Mbunge wa jimbo hilo, Mheshimiwa Kamonga. Ifikapo tarehe 30 Aprili, ile fedha shilingi milioni 20, itakuwa imepelekwa katika Kijiji cha Chanjale kwa ajili ya kukamilisha ile zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Rais amepeleka shilingi milioni 50 katika Kijiji hicho cha Chanjale kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba ili zahanati hii ikikamilika ianze kutoa huduma kwa wananchi. Natumia nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ludewa kwamba, ifikapo tarehe 30 Juni, 2024 zahanati ile iwe imekamilika ili tarehe 1 Julai, 2024, wananchi wa Chanjale waanze kupata huduma za afya katika zahanati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ni kweli kwamba, wananchi wa Kata ya Madilu wanahitaji kituo cha afya na tayari Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imepeleka wataalam. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kituo kile kipo kwenye orodha ya vituo ambavyo vitapewa fedha kupitia Mfuko wa Benki ya Dunia ambapo tunaamini kabla ya Mwezi Juni mwaka huu fedha zitakuwa zimefika na kazi za ujenzi zitaanza kutekelezwa. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kijiji cha Kamsanga kina zahanati ambayo ina vigezo vinavyoipa hadhi ya kuwa kituo cha afya. Je, ni lini Serikali itaipandisha hadhi zahanati hiyo ya Kijiji cha Kamsanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu

Spika, naomba kupokea hoja ya Mheshimiwa Kakoso kuhusiana na uhitaji wa kuipandisha hadhi Zahanati ya Kamsamba kuwa Kituo cha Afya. Sisi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kupitia Mganga Mkuu wa Mkoa na halmashauri tutafuatilia tathmini ya kukidhi vigezo na baadaye tutaweka mpango, ili fedha ikipatikana tuweze kuipandisha hadhi kuwa kituo cha afya, kama itakidhi vigezo vinavyotakiwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Zahanati ya Sunzula, Wilaya ya Itilima inahudumia wananchi wengi sana. Je, ni lini Serikali itaipandisha hadhi zahanati hiyo kuwa kituo cha afya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, upandishaji wa hadhi zahanati kuwa vituo vya afya, unatokana na kukidhi vigezo ambavyo, kwanza, ni idadi ya wananchi wanaohudumiwa. Pili, ni eneo la zahanati yenyewe. Tatu ni umbali wa zahanati hiyo kutoka kituo cha afya kilicho karibu zaidi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaifuatilia zahanati hiyo ili kuona kama inakidhi vigezo hivyo na kama ni kata ya kimkakati basi tuweze kuanza mpango kwa ajili ya kuipandisha hadhi zahanati hiyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, ajiandae Mheshimiwa Paresso.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nimeuliza zaidi ya mara tano, je, ni lini Mheshimiwa Waziri atatoa pesa kiasi cha shilingi milioni 500 ili kuweza kukamilisha Zahanati ya Nkome, ambayo Waziri anaifahamu, zahanati ambayo kwa mwezi inazalisha wastani wa watoto 420? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Musukuma na pia nawapongeza wananchi wa kata hiyo kwa kweli, kasi ya kuleta watoto ni kubwa sana, watoto 400 kwa mwezi ni kasi kubwa sana. Sisi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tumefika pale, mimi mwenyewe nilifanya ziara na tumeweka mpango wa kutafuta fedha ili vituo kama vile vipandishwe hadhi kuwa vituo vya afya. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ipo kazini inatafuta fedha, mara ikipatikana tutakwenda kujenga kituo cha afya katika eneo lile. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso, ajiandae Mheshimiwa Mama Kikwete.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Upandishaji hadhi wa baadhi ya zahanati hapa nchini kuwa vituo vya afya unafanywa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na huwa ni mchakato mrefu sana. Je, ni kwa nini Serikali isifikirie kukaimisha madaraka hayo kwenye Sekretarieti za Mikoa kwa kutumia vigezo vilevile baada ya kufanya tathmini ili kufupisha mlolongo huu mrefu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hakuna mlolongo mrefu wa kupandisha hadhi zahanati kuwa vituo vya afya kwa sababu, wanaohusika ni Mganga Mkuu wa Halmashauri kupitia *CHMT* na Mkurugenzi. Wanafanya tathmini, wanawasilisha kwa Mganga Mkuu wa Mkoa kupitia *RAS* na baadaye wanawasilisha Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kazi ambayo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inaifanya ni kutoa idhini, lakini mchakato wote unafanyika katika ngazi ya halmashauri. Tutaendelea kuboresha mchakato huo ili vituo ambavyo vinakidhi haja viweze kupandishwa hadhi kwa wakati. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mama Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote naomba kuwapa pole Watanzania kwa kadhia iliyowakumba ya mafuriko ikiwemo Mbeya na Lindi Manispaa. Swali langu, je, ni lini Kituo cha Afya cha Kitomanga kitapandishwa hadhi kwa kuwa kinakidhi vigezo vyote? Tamko hili la kupandishwa hadhi ni la miaka mingi, zaidi ya nane, iliyopita. Je, ni nini kauli ya Serikali kwa Kituo cha Kitomanga, ukizingatia Jimbo la Mchinga halina hospitali hata moja? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, amefuatilia mara nyingi kuhusiana na haja ya kupandisha Kituo cha Afya cha Kitomanga kuwa Hospitali ya Halmashauri. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hili tumelipokea, tumeanza kulifanyia kazi na mara tutakapokamilisha utaratibu huo tutamletea taarifa rasmi kwamba, ni lini tunaanza kuongeza majengo ambayo yanastahili kuongezwa ili kituo kiwe na ngazi ya hospitali. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Omar Issa Kombo.

Na. 71

**Kodi na Tozo Fedha za Mfuko wa Jimbo – Zanzibar**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanyia kazi changamoto ya Kodi na Tozo kwenye Fedha za Mfuko wa Jimbo kwa upande wa Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Jimbo la Wingwi kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi na tozo hutozwa kwa mujibu wa Sheria pindi bidhaa au huduma zinapotolewa au kununuliwa. Aidha, bidhaa na huduma zinazotolewa hukatwa kodi ya zuio la kodi *(withholding tax)* kwa kuzingatia Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, chini ya Kifungu cha 83(1)(c) kwa mujibu wa ada ya huduma kwa ajili ya utoaji wa huduma za kitaalam. Aidha, Kifungu cha 83A, malipo ya bidhaa zinazotolewa na mkazi wa uendeshaji biashara. Vilevile, kodi hutozwa kwa kuzingatia Sheria ya Manunuzi iliyotumika Zanzibar inayojulikana kama Sheria zinazotolewa na mkazi wakati wa uendeshaji wa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za Mfuko wa Jimbo zinaendelea kuleta tija na matokeo chanya katika kuimarisha na kukuza uchumi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla na hivyo huleta manufaa kwa wananchi wa pande zote mbili za Muungano. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omar Issa Kombo.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini kabla sijauliza naomba kusahihisha, ni Mkoa wa Kaskazini Pemba, Wilaya ya Micheweni, siyo Mkoa wa Kaskazini Unguja. Sasa, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza Sheria mbalimbali ambazo zinakata kodi kwa Mfuko huu wa Majimbo kwa upande wa Zanzibar, ikiwemo upande wa Jamhuri na ile ya upande wa Serikali ya Zanzibar. Je, Serikali zote mbili hazioni haja ya kukaa pamoja na kuona namna ya kupunguza au kuondoa kabisa kodi hizi kwa ukizingatia kwamba, mifuko hii inakwenda kuwahudumia wananchi moja kwa moja?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali haioni haja ya kutoa maelekezo kwa Halmashauri za Zanzibar kwamba, wasitumie fedha hizi kama vyanzo vyao vingine vya mapato ya halmashauri kwa vile fedha hizi vilevile zinawahudumia wananchi wa Zanzibar kwenye majimbo yetu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kombo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka Waheshimiwa Wabunge wote wafahamu kwamba, makato ya fedha hizi yapo kisheria, yanakatwa kwa mujibu wa Sheria. Maana yake ni kwamba, uwepo wa hizi kodi ni kwa sababu, Sheria zipo na zinawaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri, wa Majiji, wa Mabaraza ya Miji kwamba, fedha hizi zinazotumika kununua vifaa kwa ajili ya Mfuko wa Jimbo ni lazima zikatwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli fedha hizi ni kidogo, lakini zinatumika kwenye miradi ya jamii, mahitaji ya fedha hizi ni mengi uki-*compare* na zinazotoka. Waheshimiwa Wabunge, ni lazima tukubaliane kwamba, fedha hizi ni lazima zikatwe kodi, ili halmashauri zetu ziweze kupata kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ninachotaka kuwaambia Waheshimiwa, ni tumefanya vikao mara kadhaa na Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri, wa Majiji, wa Mabaraza ya Miji na taasisi

zinazokusanya fedha, zikiwemo *ZRA* na *ZRB,* lengo na madhumuni ni kuona namna ambavyo tunawaelimisha Waheshimiwa Wabunge na wengine ili waweze kufahamu hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, mweleze kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama alivyoshauri basi tutalichukua na kwenda kuyafanyia kazi yale ambayo ameshauri.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Londo.

Na. 72

**Mkopo wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi**

**MHE. DENNIS L. LONDO** aliuliza:-

Je, Serikali imetoa na kukusanya kiasi gani kutokana na mkopo wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi na kiasi gani kimerudi kuendeleza mpango huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali ilitoa bilioni 50 kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK). Fedha hizo zilikopeshwa bila riba kwenda kwenye halmashauri 57 ambacho

kilikuwa ni kiasi cha shilingi bilioni 43.6. Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Iringa kiasi cha shilingi milioni 450, Vyuo vya Ardhi vya Tabora vilipata milioni 644, Morogoro vilipata bilioni 1.2 na Chuo Kikuu Ardhi kilipata milioni 892.8 ambazo zimewezesha jumla ya kupanga na kupima viwanja 218,337.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufika Machi, 2024, jumla ya shilingi bilioni 23.5 sawa na asilimia 47 zimekwisharejeshwa. Halmashauri 12 zimekamilisha marejesho yenye kiasi cha shilingi bilioni 11.3, halmashauri 43 zimerejesha sehemu ya fedha yenye jumla ya shilingi bilioni 10.9, Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Iringa imerejesha shilingi milioni 581.3, Chuo cha Ardhi Morogoro milioni 250, Chuo cha Ardhi Tabora milioni 100, Chuo Kikuu Ardhi milioni 100 na halmashauri mbili ambazo ni Shinyanga Manispaa shilingi bilioni 1.055 na Musoma *DC* shilingi milioni 200 hazijarejesha kabisa. Wizara yetu itaendelea kufuatilia halmashauri ambazo hazijakamilisha kurejesha fedha hizo ili zitekeleze wajibu huo kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa baina ya Wizara na halmashauri hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Londo.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Migogoro ya ardhi inazidi kushamiri katika maeneo mbalimbali hasa katika Wilaya ya Kilosa hususani Jimbo la Mikumi. Fedha hizi zilikuwa ni mpango endelevu kwa maana ya *revolving fund,* sehemu ya mwisho ya swali langu lilikuwa ni kwamba; je, fedha iliyorudi ni kiasi gani ambacho kimeendelea kukopeshwa kwenye halmashauri? Swali hilo halikujibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza; je, ni lini fedha zaidi ya bilioni 30 ambazo zimekopeshwa na kwenda kwenye matumizi mengine ambayo hayakukusudiwa, kwa mfano fidia, ujenzi wa mahoteli na miundombinu mingine ambayo siyo lengo la fedha hizi, watuhumiwa ama waliopeleka fedha hizo watachukuliwa hatua?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni lini Serikali itazisimamia fedha hizi ambazo ni *revolving fund* ili faida yake irudi kupima maeneo mengine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba Serikali imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba fedha hizi zote zilizotolewa zinarejeshwa. La kwanza, ipo mipango ambayo imekwishapangwa ikiwemo kutolewa kwa mwongozo maalum wa jinsi ya utoaji na urejeshaji wa fedha hizo baada ya kugundua kwamba yako baadhi au ziko baadhi ya halmashauri ambazo zimekwenda kinyume na utaratibu ule ambao ulitolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba mwongozo upo tayari kwa ajili ya kutoa hizo pesa kwa ajili ya halmashauri nyingine. Pia, kwa zile halmashauri ambazo hazijatoa tumekwishafanya mazungumzo pamoja na wenzetu wa USEMI ambao ni Kamati yako ya Bunge ili kuweza kuona kwamba kwa zile halmashauri ambazo hazijarejesha pesa zinaitwa mbele ya Kamati hiyo tukishirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili ziweze kurejesha pesa hizo kama ambavyo imekubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo kwa zile halmashauri katika swali lake la pili halmashauri ambazo hazijarejesha pesa ni hatua gani ambazo zinachukuliwa? Tumeshawasiliana na halmashauri hizo na tumeshazielekeza halmashauri hizo na kupeana muda zikiwemo halmashauri ambazo mpaka sasa hivi zimerejesha sehemu ya pesa hizo ambazo ni halmashauri 43 na zile halmashauri mbili ambazo hazijarejesha nazo zihakikishe kwamba fedha zimekuja ndani ya muda. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa zipo halmashauri ambazo zimefanya vizuri kwa kurejesha fedha hizo ikiwemo Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Je, Serikali ina mpango gani wa kuziongezea mkopo halmashauri hizi ili ziweze kufanya kazi hii ya kupanga, kupima na kumilikisha kwa uzuri zaidi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA K.n.y. WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyofahamika Mfuko huu ni Mfuko ambao fedha zake ni fedha za kuzungushwa. Kwa maana hiyo, kwa zile halmashauri ambazo zitakuwa zimefanya vizuri kwa kufanya marejesho vizuri na ndani ya muda, maelekezo ya mwongozo tulioutoa ni kuhakikisha kwamba halmashauri hizi zinabuni tena miradi na fedha hizi zinapelekwa katika halmashauri hizo ili kuendelea kuzalisha viwanja na kutengeneza makazi kwa ajili ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba, kwa zile halmashauri ambazo zimekwishakamilisha kurejesha fedha hizo tunawakaribisha ndani ya ofisi yetu ili tuweze kuendelea kuwakopesha ili waweze kupima ardhi, kupanga na kutengeneza utaratibu mzuri kwa ajili ya makazi yaliyo bora kwa wananchi wa Tanzania kama ambavyo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameelekeza kupitia Mradi huu wa Kupanga, Kupima na Kurasimisha Ardhi ya Tanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Ndugulile.

Na. 73

**Ujenzi wa Barabara ya Gomvu – Kimbiji hadi Pembamnazi**

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza:-

Je, lini barabara ya Gomvu - Kimbiji – Pembamnazi itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Gomvu – Kimbiji – Pembamnazi ni sehemu ya barabara ya Mjimwema – Kimbiji - Pembamnazi yenye urefu wa kilometa 49 ambayo inajengwa kwa awamu kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa sehemu ya Cheka – *Avic* yenye urefu wa kilometa mbili tayari ujenzi umekamilika. Kwa sehemu ya *Avic* – Kimbiji kilometa 10 taratibu za manunuzi ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi zinaendelea. Ujenzi kwa sehemu iliyobaki ya Kimbiji hadi Pembamnazi itajengwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; barabara ambayo ameitoa alipotoka kujibu maswali Mheshimiwa Waziri kutokana na athari za mvua zinazoendelea sasa hivi imekatika na wananchi wanapata shida kubwa sana *especially* katika maeneo ya kwa Moris na maeneo mengine pale Kimbiji. Je, nini mkakati wa muda mfupi wa ukarabati wa barabara hii ili wananchi wa Pemba Mnazi waweze kufika katika maeneo kwa gharama nafuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; ni Barabara ya Kibada – Mwasonga. Barabara hii yenye urefu wa kilometa 41 na inatumika kwa magari mengi mazito lakini barabara hii mkataba wake umeshasainiwa mwezi Machi, 2024 na sasa hivi imeharibika

sana. Wananchi wa Kigamboni wanataka kujua na kupata kauli ya Serikali ni lini ujenzi wa barabara hii utaanza? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ndugulile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kuhusu Mvua za *El-Nino* zinazoendelea na kukatika kwa barabara. Nitumie nafasi hii kuendelea kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa namna ambavyo wameendelea kutupa ushirikiano kwenye majimbo yao pale mawasiliano yanapokatika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru pia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutupatia fedha za *emergency* ili tuweze kurekebisha pale ambapo mawasiliano yanakatika. Kwa upande wa Mheshimiwa Dkt. Ndugulile nimwelekeze Meneja wa *TANROADS,* Mkoa wa Dar es Salaam kufika maeneo haya na kufanya tathmini ili tuweze kujitahidi kwa kadri inavyowezekana kuhakikisha mawasiliano ya barabara yanaendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la pili kuhusu Barabara ya Kibada – Mwasonga kilometa 47, tunamshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa kutupa kibali kwa kusaini baadhi ya barabara ambazo zimefikia hatua ya kusainiwa ili ujenzi uanze. Barabara hii Jimboni kwa Mheshimiwa Ndugulile ni kweli mkandarasi alisaini mkataba huu mwezi Machi na sasa hivi namwelekeza mkandarasi kuendelea na *mobilization* wakati tukimtafutia taratibu za malipo ya *advance*. Vilevile, Mkandarasi huyu anawajibika kufanya matengenezo ya barabara kwa sababu tumeshamkabidhi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli lazima tumpe maua yake Mheshimiwa Rais. Maeneo mengi yote yaliyoguswa na mafuriko Mheshimiwa Rais amepeleka pesa. Kwa hiyo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mtanda, ajiandae Mheshimiwa Michael.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Barabara ya kutoka Mtama – Kitangali kwenda Newala Jimbo la Newala Vijijini inapitika kwa shida kwa sababu ya ubovu wa barabara ile kwa muda mrefu. Je, ni lini Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami ili kuwanusuru wananchi wa Newala na hali ambayo ipo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Barabara ya Mtama – Newala ni kweli barabara hii Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiomba muda mrefu kujengwa kwa kiwango cha lami, lakini niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuitengeneza barabara hii kwa kiwango cha changarawe. Kwenye vipaumbele vya Wizara ya Ujenzi tutaangalia namna ya kuanza kwa kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana kwa kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Michael.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Barabara ya Makofia – Mlandizi – Mlandizi Vikumburu imeshafanyiwa tathmini na wananchi wanasubiri kupata fidia. Je, Serikali imefikia hatua gani ya kuwalipa ili barabara hii iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael kuhusu Barabara ya Makofia – Mlandizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni kipaumbele kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, lakini naomba yeye pamoja na wananchi waendelee kuwa na Subira, tutaiweka kwenye vipaumbele kwa kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Gwajima.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kwamba Barabara ya kutoka Bunju *B* kwenda Mabwepande mpaka Ubungo ijengwe kwa kiwango cha lami. Je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gwajima, Mbunge wa Jimbo la Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii ni muhimu, lakini Mheshimiwa Gwajima na Waheshimiwa Wabunge kama wanavyofahamu sasa hivi kuna ukatikaji wa mawasiliano ya barabara na madaraja kote nchini, kipaumbele namba moja ni kuhakikisha tunarudisha mawasiliano haya ili shughuli za uzalishaji kiuchumi na kijamii ziweze kuendelea. Kwa hiyo barabara hizi ikiwemo hii barabara ambayo Mheshimiwa Gwajima amekuwa akiifuatilia kwa karibu tumuahidi yeye pamoja na wananchi kwamba kadri fedha zitakavyopatikana na yenyewe tutaiweka kwenye vipaumbele. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, muda wetu unakwenda. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Kakunda

Na. 74

**Kushusha Bei ya Mbegu za Mahindi**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itasimamia ushushaji wa bei ya mbegu za mahindi kwa wakulima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mbuge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusimamia udhibiti wa upandishaji holela wa bei za mbegu za mazao ya kilimo hususani mahindi kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Wizara ya Kilimo imefanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kupitia Taasisi ya *TOSCI* imechukua hatua za kutangaza bei elekezi ya mbegu za mahindi kwa reja reja na jumla ili kudhibiti upandishaji holela wa bei za mbegu. Pili, imeunda timu ya Wataalamu kutoka Wizara ya Kilimo, Taasisi ya *TARI*, *ASA* na *TOSCI* pamoja na sekta binafsi na inaongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Maendeleo ya Mazao. Pamoja na mambo mengine itaandaa mjengeko wa bei za mbegu za mazao ya kilimo kwa ajili ya bei elekezi zitakazokuwa zinatangazwa mwezi Septemba kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo imeyaandikia makampuni yote ya mbegu kuwasilisha taarifa za gharama za uzalishaji wa aina mbalimbali za mbegu ili kuimarisha utaratibu wa kupanga bei elekezi. Naomba nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kuyakumbusha makampuni yote ya mbegu kuwasilisha taarifa hizo kabla ya tarehe 30 Aprili. Wizara haitasita kuyafutia leseni makapuni yote ya mbegu ambayo hayatawasilisha taarifa hizo kama zinavyohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kuishirikisha sekta binafsi kutumia Ardhi ya *ASA* na *TARI* kuzalisha mbegu kwa utaratibu wa kuingia mikataba ya muda mrefu ili kuongeza upatikanaji wa mbegu kwa wakulima na kwa bei nafuu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali na nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; bei elekezi ambazo zilitangazwa na *TOSCI* tarehe 20 Oktoba, 2023 ambayo ni shilingi 4,000 kwa kilo kwa mbegu zinazochavushwa huria au *OPV* na shilingi 7,150 hadi 8,000 kwa mbegu chotara, hili ndilo linalolalamikiwa na wananchi kwamba ni bei kubwa sana. Je, kwa nini Serikali haiweki ruzuku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kazi ya utafiti wa mbegu ni kazi ya msingi ya Serikali. Kwa nini hadi sasa mbegu 60% bado zinatoka nje? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kakunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza siyo sahihi kusema kwamba 60% ya mbegu zinazouzwa katika soko letu zinatoka nje. Mwaka huu kama nchi mbegu zinazotoka nje na mbegu zilizozalishwa ndani ya nchi jumla ilikuwa ni tani 60,000, ambapo tani 17,000 zimetoka nje na tani 43,000 zimezalishwa ndani ya nchi na asilimia 80 ya hizi tani 43,000 zimezalishwa na Makampuni ya Kitanzania na mbegu za msingi zimezalishwa kutoka *TARI* katika Taasisi yetu ya Utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo amesema ni suala la ruzuku. Kwanza kabla ya bei elekezi mbegu ambazo zilikuwa zimetangazwa na Serikali kuuzwa shilingi 4,000 zilikuwa zinauzwa kati ya shilingi 20,000 mpaka 25,000 katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu kwa kilo mbili. Kwa maana ya wastani wa shilingi 12,000, lakini baada ya bei elekezi ya Serikali zimeuzwa kwa shilingi 7,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipokea wazo lake la kwamba kwa nini Serikali isiweke ruzuku katika mbegu? Wizara sasa hivi

inafanya tathmini ya kutengeneza mjengeko wa bei na mabadiliko ya Kanuni ya *TOSCI* ili Mamlaka ya *TOSCI* ipewe haki ya kisheria ya kuweza kusimamia suala la udhibiti wa bei. Kwa hiyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge watupe muda, tutaangalia mfumo mzuri wa kusaidia sekta ndogo ya mbegu na tunaelewa umuhimu wa Serikali kuweka ruzuku kama tulivyoweka kwenye mbolea. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mama Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuchukua hatua nyingi na kuhakikisha kwamba pembejeo zinazifika kwa wakati; je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba *cotton twine* na *jute twine* zinafika kwa wakati na pia zinauzwa kwa bei iliyopangwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mama Sitta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri kumetokea changamoto msimu huu wa tumbaku *cotton twine* na *jute twine* zilichelewa na changamoto ya msingi kwa nini zilichelewa Vyama Vikuu vya Ushirika vilichelewa kupata *letter of credit* kutoka Taasisi za Fedha, hatukuwa na tatizo hili katika misimu miwili, mitatu iliyopita. Nataka niwaahidi wakulima wa tumbaku na Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka katika maeneo ya tumbaku kama tulivyorekebisha mfumo wa upatikanaji wa mbolea na kufika kwa wakati; tutahakikisha tatizo lililojitokeza mwaka huu la *cotton twine* na *jute twine* halitokei kwa sababu tumeshaanza kuongea na viwanda vya ndani vya Watanzania ili viwekeze kwenye eneo la kuzalisha *cotton twine* kwa sababu pamba inapatikana ndani ya nchi. Majaribio ya awali yameanza Mkoa wa Tabora kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali wadogo

wadogo waweze kuzalisha *cotton twine* na tuache kutumia dola milioni nne kuagiza kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie Bunge lako Tukufu kuwataka *ginners* na wanaoongeza thamani kwenye pamba, Serikali ipo tayari kumpa mwekezaji yeyote *concession agreement* ya muda mrefu, kwa ajili ya kuzalisha *cotton twine* na atapata mkataba wa muda mrefu na hatuta-*import cotton twine* kama atawekeza katika eneo hilo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo, Mheshimiwa Venant Daud Protas.

Na. 75

**Kutoa Elimu na Chanjo bure kwa Wafugaji**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali isitoe elimu pamoja na chanjo bure kwa wafugaji wa ng'ombe nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutoa elimu ya umuhimu wa chanjo kupitia vyombo vya habari, maonesho mbalimbali yakiwemo Maonesho ya Nanenane, Sabasaba, programu mbalimballi za utoaji elimu kwa umma na mafunzo rejea kwa wataalam wa mifugo. Aidha, Mamlaka ya Serikali za Mitaa kupitia wataalam wa mifugo zimeendelea kutoa elimu bure kwa wafugaji juu ya umuhimu wa chanjo na uchanjaji wa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha wafugaji wanachanja mifugo yao, Wizara iliandaa Kanuni za Chanjo na Utoaji wa Chanjo *(The Animal Diseases Vaccine and Vaccination*

*Regulations of 2020)* ambazo zinamtaka mfugaji kuchanja mifugo yake kuendana na kalenda ya uchanjaji wa magonjwa ya mifugo. Hata hivyo, hali ya uchanjaji kwa sasa ipo chini ya 50% ambayo ni chini ya malengo ya kuchanja mifugo, kwa angalau ya 70% kwa kila ugonjwa unaolengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha utoaji chanjo unafikia 70% iliyolengwa, Wizara imeandaa programu ya uchanjaji mifugo dhidi ya magonjwa ya kipaumbele ya miaka mitano ambayo itagharimu shilingi bilioni 216. Aidha, programu hiyo itaanza kutekelezwa katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 ambapo kiasi cha shilingi billioni 29 kimetengwa kwa ajili ya kuanza kampeni ya utoaji wa chanjo ya ruzuku, dhidi ya magonjwa ya mifugo ya kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venant.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.  Swali langu la kwanza; tumekuwa na chanjo nyingi ambazo sisi kama Serikali tunapeleka. Tumepeleka chanjo za surua tunatoa bure. Tumepeleka pepopunda tunatoa bure. Ni kwa nini sasa, Serikali isipeleke chanjo za mifugo na zikatolewa bure na wataalam wetu wakatumika kutoa hizo chanjo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; tumekuwa na chanjo ambazo zinaendelea katika halmashauri zetu na majimbo yetu, lakini hizi chanjo zinatolewa *tender* na wazabuni wana-*tender* wanakwenda kuchanja kule, lakini mfugaji akipata athari kwenye mifugo yake hakuna msaada wowote ambao anaweza kuupata kupitia hao watoa huduma. Je, Serikali haioni haja ya kupeleka madawa na wataalam wetu wakaenda kuwachanjia wafugaji wetu ili ziweze kuwasaidia *direct* na wakipata matatizo wajue wapi wanakwenda? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba, chanjo nyingi zimekuwa zikitolewa bure, chanjo za binadamu na maeneo mengine. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba Mwaka wa Fedha 2024/2025, tayari Serikali imekwishatenga bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 29, kuanza kutoa chanjo bure kwa mifugo yetu ambayo wananchi wetu wanamiliki katika maeneo yao. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mwaka huu katika bajeti hii itakapokuja aipitishe kwa kishindo ili twende kutekeleza jambo hili ambalo na yeye yamekuwa ni maono yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili tumepokea ushauri na ushauri huu tutakwenda kuufanyia kazi tuone namna ambavyo Serikali kupitia Wizara inaweza kuutekeleza ushauri huu. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Katika Kata ya Mkindi kuna Kijiji cha Kihwenda ambapo panajengwa bwawa kwa ajili ya wafugaji. Ni takribani mwaka wa pili sasa Mkandarasi ameondoka *site* na bwawa lile ni muhimu sana kwa maji kwa ajili ya wafugaji pamoja na wananchi. Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha kuwa, Mkandarasi anarudi na bwawa lile linakamilika? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli bwawa hilo limesimamishwa ujenzi wake. Nimhakikishie Mbunge tutakwenda kufuatilia, tutaangalia mimi na yeye twende kule, tuangalie na wataalam tuone namna ambavyo tunamrudisha Mkandarasi *site* ili aweze kukamilisha bwawa hilo na wananchi waweze kupata huduma katika eneo hilo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa Ally Kassinge.

Na. 76

**Fidia kwa Wananchi Wanaopisha Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Kilwa Masoko**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani kuwalipa fidia wananchi 438 waliofanyiwa uthamini ili kupisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Kilwa Masoko?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kushughulikia na kufuatilia kwa ukaribu suala la ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege, Kilwa Masoko linakamilika. Hatua ya awali ya kutambua wafidiwa na mali zao imekamilika na kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali. Sambamba na hilo maombi hayo yamewasilishwa Serikalini kwa ajili ya malipo. Hivyo, Serikali itahakikisha kuwa wananchi wote wanaopisha maeneo yao kwa ajili ya upanuzi wa kiwanja hicho wanalipwa fidia zao stahiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipate faraja kidogo kwa majibu ya Serikali kwamba hatua iliyofikiwa sasa hivi ni kwamba tayari daftari lipo kwa Mthamini Mkuu Hazina kwa maana ya Wizara ya Fedha. Wananchi hawa wamekuwa wakiathirika kwa muda mrefu tangu 2013 walikuwa ni 144, ukafanyika tena uthamini 2023 wakafikia wananchi 438. Hivi tunavyozungumza wananchi wangu hawa 438, hawana makazi kutokana na kushindwa kuziendeleza nyumba zao kwa kusubiri taratibu za Serikali. Hali ni tete kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kutokana na ukweli kwamba tumeshakaa na Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara ya Fedha na kukubaliana kwamba, wananchi hao walipwe haraka iwezekanavyo. Je, ni nini kauli ya Serikali kulipa wananchi hawa fidia ndani ya kipindi kifupi kijacho kabla hawajaendelea kuathirika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; Uwanja wa Ndege wa Kilwa Masoko ni moingoni mwa viwanja 12 ambavyo tuliviingiza katika mpango wa miaka mitano wa kuboresha na kupanua. Faraja tuliyonayo pale Kilwa Masoko tunajenga Bandari ya Uvuvi. Kufuatia ujenzi wa Bandari ya Uvuvi, umuhimu mkubwa wa kuimarisha kiwanja hiki upo na uhitaji mkubwa utahitajika huko mbele ya safari. Je, ni lini sasa Serikali baada ya kulipa wananchi wangu ndani ya muda mfupi, itaanza ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Kilwa Masoko? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Ally Kassinge kwa ufuatiliaji makini wa Kiwanja hiki cha Ndege. Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa Kiwanja cha Ndege cha Kilwa Masoko. Moja, ameeleza vizuri sana, Serikali imewekeza bilioni 268 kwa ajili ya ujenzi wa bandari kubwa katika Ukanda wetu wa *East Africa,* Bandari ya Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunao Mradi mkubwa sana wa Gesi wa Mkoa wa Lindi. Hivyo, kiwanja hiki ni muhimu sana siyo tu kwa wananchi wa Lindi na ukanda huo, lakini kwa Taifa letu. Hivyo nimhakikishie Mbunge kwamba, Serikali kauli yake imeshafanya uthamini hatua ya kwanza na ya pili na mpaka wamefika wananchi karibu 454 ambao tunategemea kuwalipa karibu 6,200,000,000. Naomba Mbunge apokee kauli ya Serikali ninayoenda kuitamka sasa. Serikali italipa fidia wananchi hao, mara tu itakapokamilisha hatua za ndani na itaanza hatua za ujenzi mara moja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mwenye pesa kasimama.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu kwa majibu yake mazuri, pia nimpongeze sana muuliza swali. Muuliza swali amehusisha Wizara ya Fedha. Ni kweli suala hili tunalitambua na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wake kule Kilwa, wawe na amani kabisa fedha hiyo italipwa kwa wakati. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Ndulane.

Na. 77

**Ujenzi wa Jengo la Makumbusho Kijiji cha Nandete – Kilwa**

**MHE. FRANCIS K. NDULANE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Jengo la Makumbusho katika Kijiji cha Nandete ili kuhifadhi kumbukumbu za Vita vya Majimaji?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Ndulane kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa makumbusho unahitaji utafiti wa kina wa historia ya eneo husika ili kuweza kupata taarifa na mikusanyo itakayowekwa kwenye makumbusho tarajiwa. Kwa kutambua umuhimu wa historia ya vita vya Majimaji katika eneo la Nandete, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeanza kufanya utafiti kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na jitihada hizo mwaka 2022 Serikali imefanya maboresho ya Sheria ya Mambo ya Kale, Sura ya 333 ili kuruhusu watu binafsi na taasisi mbalimbali kuanzisha makumbusho binafsi kwa lengo la kuhifadhi na kuendeleza utalii unaohusiana na utajiri wa kihistoria uliopo. Natoa wito kwa wadau wetu kutumia fursa hiyo kujenga makumbusho

kwenye maeneo ya kihistoria hapa nchini ili kuendeleza historia na kujipatia kipato.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kupata jibu zuri linaloashiria uendelevu wa kumbukizi hizi. Pia napenda kuipongeza Serikali mwezi uliopita tarehe 15 ilitoa *GN* ya Maadhimisho haya ya Kumbukizi za Majimaji. Kwa hiyo, kwa niaba ya mashujaa 30 walioongoza vita hii pamoja na wananchi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini, naipongeza sana Serikali kwa hatua hii, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa *GN* imepatikana ya kumbukizi hizi, je, ni lini Serikali itaanza kutenga fedha kwa ajili ya maadhimisho ya kumbukizi hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, Serikali ina mkakati gani kwa kushirikisha Wizara ya Maliasili na Utalii, Taasisi ya *TARURA* na *TANROADS* kuwezesha barabara zinazokwenda kwenye kumbukizi hizi ziweze kupitika katika kipindi chote cha mwaka mzima? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea pongezi za Mheshimiwa Mbunge. Kama tunavyofahamu tupo kwenye kipindi cha bajeti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge kipindi bajeti ya Wizara hii itakapofika, basi tuweze kuipitisha ili tuweze kufanya haya ambayo yanayoombwa na Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na hili suala la barabara, barabara zote ambazo zipo kwenye maeneo ya hifadhi tunaishukuru Serikali imetupatia vifaa na fedha za kuweza

kufanya ukarabati kwenye maeneo haya. Vilevile kama tulivyomsikia Waziri wa Miundombinu muda mfupi uliopita kwamba Serikali imetoa fedha za kuhakikisha inafanya ukarabati kwenye maeneo ambayo yamepata changamoto ili ziweze kupitika. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwa barabara mahsusi ambazo zina tatizo hili, awasiliane na Wizara husika ili ziweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Cosato David Chumi.

Na. 78

**Wahitimu wa Kidato cha Nne na Sita Kujiunga na JKT**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kuiongezea bajeti JKT ili kuiwezesha kuchukua wahitimu wote wa Kidato cha Nne na Sita wenye sifa za kujiunga na JKT?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali kutoa mafunzo kwa wahitimu wote ambao wana sifa ya kujiunga na mafunzo ya JKT kwa kujitolea na kwa mujibu wa sheria. Kwa sasa, vijana wote hawapati fursa ya kuhudhuria mafunzo hayo kutokana na ufinyu wa bajeti. Mpango uliopo ni kulijengea Jeshi la Kujenga Taifa uwezo ili liweze kuchukua vijana wengi zaidi wa kujitolea na wahitimu wote wa kidato cha sita, ambao wanastahili kujiunga na mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria, kwa kuongeza bajeti ili kuboresha mafunzo na kuongeza idadi ya makambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha, ili kuongeza miundombinu ya makambi na bajeti ya kuendesha mafunzo ya JKT kadri uwezo wa Serikali utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali kimsingi Jeshi la Kujenga Taifa wao wanapokea vijana kulingana na bajeti waliyotengewa. Kwa hiyo, swali langu kimsingi nilikuwa nimelielekeza Wizara ya Fedha, kuona kwa namna gani itawaongezea bajeti JKT ili ichukue vijana wengi kadri inavyowezekana. Kwa hivyo, sitakuwa na swali la msingi kwa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, tunaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha ili kuongeza bajeti kwa ajili ya makambi pia uendeshaji wa Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba, tumekwishapokea maelekezo kutoka kwenye Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ya kufanya tathmini, ili kuweza kujua ni kiasi gani kinahitajika, miundombinu kiasi gani inatakiwa ili tuweze kuwachukua vijana wote. Tathmini hii inaendelea, tumekwishatoa taarifa kwamba itakamilika Mwezi wa Sita mwaka huu na baada ya hapo, tutakuja na mpango mkakati ambao utaainisha mahitaji yote na haya tutayafanya kwa kushirikiana na Wizara ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tukikamilisha tutaleta taarifa kuonesha kwa ujumla wake ni kiasi gani kinahitajika, tumejipanga namna gani na tutaweza kuwachukua vijana hawa

kwa utaratibu gani hatua kwa hatua. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na maswali yote yamekwisha.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni:-

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika ambao ni wageni saba wa Mheshimiwa Spika kutoka Kampuni ya Ndege ya *Precision* ambao ni Ndugu Vicent Shirima, Makamu Mwenyekiti wa Bodi; Ndugu Patrick Mwanri, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika; Ndugu Lilian Masawe, Mkuu wa Kitengo cha Biashara; Ndugu Nelson Mesuli, Meneja Mauzo na Huduma za Shirika; Ndugu Hillari Mremi, Meneja Mawasiliano na Masoko; Ndugu Gloria Kaira, Mratibu Mauzo Ofisi ya Dodoma; na Ndugu Elvis Audat, Afisa Mauzo Ofisi ya Dar es Salaam. Karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, viongozi hawa wa *Precision Air* wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wako Viwanja vya Bunge, nyuma ya Jengo la Msekwa kuonesha huduma wanazozitoa. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Spika ni watumishi 29 wa Taasisi ya *Tulia Trust* kutoka Jijini Mbeya. Karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao ni Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar, Sera, Uratibu. Karibu. *(Makofi)*

Wapo pia Dkt. Jim James Yonazi, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu; Ndugu Mary Ngelela Maganga, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira; Ndugu Salhina Mwita Ameir, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Sera, Uratibu na Baraza; Ndugu Ramadhani Kombwey Kailima, Mkurugenzi wa Uchaguzi, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi; na Ndugu Thabit Idarous Faina, Mkurugenzi wa Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi Zanzibar *(ZEC)*. *(Makofi)*

Tunao Ndugu Mohamed Ahmed, Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa; Ndugu Aretas James Lyimo, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya; Ndugu Jerome Kamwela, Mkurugenzi Mtendaji wa *TACAIDS;* Ndugu Masha Mshomba, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa *NSSF;* Ndugu Abdul-Razaq Badru, Mkurugenzi wa Mfuko wa *PSSSF;* Ndugu Hadija Mwenda, Mtendaji Mkuu *OSHA;* na Ndugu Beng'i Issa, Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Karibuni. *(Makofi)*

Tunao pia Mheshimiwa Juma Ally Khatib, Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa na pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Siasa *ADA-TADEA,* Mheshimiwa Abdul Mluya, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge na Siasa ya Baraza la Vyama vya Siasa na pia ni Katibu Mkuu wa Chama cha Siasa cha *Democratic Party,*na Mheshimiwa Doyo Hassan Doyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Baraza la Vyama vya Siasa na pia ni Katibu Mkuu wa Chama cha Siasa cha *ADC;* Mheshimiwa Saum Rashid, Katibu Mkuu wa Chama cha Siasa cha *UDP;* Ndugu Usekelege Nashon Mpulla, Mkurugenzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA);* na Mheshimiwa Majaliwa Kyara, Katibu Mkuu wa Chama cha Siasa cha *SAU*. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Bunge kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoka Ofisi ya *CAG;* Bwana Charles Kichere Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Waheshimiwa Wabunge ahsanteni. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine ambao ni Bwana Johanes Kasiri, Afisa Masuuli; Bwana Selihina Mkumbwa, Naibu Mkaguzi Mkuu anayesimamia ukaguzi wa Mashirika ya Umma; Bi. Wendy Massoy, Naibu Mkaguzi Mkuu anayesimamia ukaguzi wa Serikali Kuu; na Bi. Kubela Mwakatundu, Naibu Mkaguzi Mkuu anayesimamia Ukaguzi wa Serikali za Mitaa; Bi. Esneath Hendry, Kaimu Naibu Mkaguzi Mkuu anayesimamia Ukaguzi wa Ufanisi; Bwana Benja Majura, Naibu Mkaguzi Mkuu anayesimamia Ukaguzi wa Hesabu za Taifa; Ndugu Gabriel Ntengo, Katibu wa *CAG;* na wameambatana na Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo kutoka

Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge waliopo leo ni:-

Tuna wageni tisa wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Kamati ya Siasa ya CCM kutoka Iringa Vijijini. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 34 wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kutoka mikoa mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, watumishi wa Taasisi ya *EGPAF* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni 12 wa Mheshimiwa Margaret Sitta ambao ni wapigakura wake kutoka Urambo Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Juma Usonge, Watendaji wa Kata za Nachingwea, Mkoa wa Lindi na Mpwapwa, Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Wenyeviti wa Kata CCM kutoka Wilaya ya Geita. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Taasisi ya *Miriam Odemba Foundation* kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, Mjumbe wa Kamati ya Uchumi wa Fedha - UVCCM Taifa. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Abdallah Chikota, mtoto wake ambaye ni mtumishi wa Benki ya *CRDB,* Tawi la Kilindi kutoka Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Venant Daud, Diwani pamoja na rafiki zake kutoka Jimbo la Uyui, Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Wapo wageni 75 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq, wadau wa Taasisi ya Na Yeye Ni Mama Pia. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni Ndugu Fidelis Baru kutoka Jijini Dodoma na Mwinjilisti Nicholaus Fungameza wa Kanisa la *EAGT* kutoka Jijini Arusha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa yamefanyika marekebisho ya ratiba ya Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge unaoendelea, marekebisho hayo yametokana na msiba wa Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil uliotokea tarehe 8 Aprili, 2024. Ratiba yenye mabadiliko inatumwa kwenye vishikwambi vyenu hivi punde.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MWEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano.

Tunaanza na Mheshimiwa Mohammed Said Issa dakika tano, wajiandae Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi na Mheshimiwa Chumi.

Mheshimiwa Mohammed Said Issa hayupo, Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, wajiandae Mheshimiwa Chumi na Mheshimiwa Protas.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote naishukuru sana Serikali kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mlimba. Wananchi wangu wa Jimbo la Mlimba ni miongoni mwa wananchi ambao wamepata maafa ya mvua hizi za *El-Nino*. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa sababu Serikali imechukua hatua mara moja baada ya wananchi wangu kupata changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii wananchi wa Kata ya Masagati, takribani kaya 391 na wananchi 1,486 wanatafuta chakula. Serikali iliweza kunisaidia usafiri wa helikopta na sisi wananchi wa Mlimba kwa kushirikiana na wafanyabiashara tuliweza kupata chakula tani nne tukawapelekea chakula kiwasaidie kwa muda huo mfupi. Sambamba na hilo, Mheshimiwa Rais alielekeza timu ya Mawaziri wanne na Manaibu watatu, ikiongozwa na Mama yangu Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, walifika Masagati, walifika Mlimba. Jambo hili naendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kweli naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze kwenye sababu za maafa. Sababu za maafa ziko mbili; moja ni mabadiliko ya tabianchi, mbili ni ukosefu wa matumizi bora ya ardhi (mipango ya matumizi bora ya ardhi). Mabadiliko ya tabianchi yametokea baadhi ya maeneo kama vile Manyara halikadhalika na kule kwangu Mlimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia pia kwa habari ya ukosefu wa mipango na matumizi bora ya ardhi kwa sababu Taifa letu lina changamoto hiyo. Katika maeneo mengi wananchi wamekuwa wakijenga maeneo ambayo ni hatarishi, *(hazardous areas)*. Sasa kama tungekuwa na mipango ya matumizi bora maana yake ni nini? Tungeweza kuchukua tahadhari haraka wananchi hao wasijenge maeneo hayo, wakajenga maeneo ambayo kimsingi yanafaa kwa kujenga makazi yao, mathalani Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiutazama Mkoa wa Dar es Salaam hauna *Infrastructure Masterplan*, hata kama ipo basi

haijatekelezwa, kwa sababu, *Infrastructure Masterplan* inaeleza wapi maji ya mvua yanaelekezwa. Sasa, katika mazingira hayo maafa haya yametokea na nimesema tu kwa sababu ya muda nieleze kwa ufupi kwamba, sababu kuu ni mbili. Ni mabadiliko ya tabianchi, ya pili ni ukosefu wa mipango na matumizi bora ya ardhi na kwa kuwa sasa hivi Waziri wa Ardhi ni Waziri anayeshaurika tutampa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nieleze madhara yaliyotokana na maafa haya hasa katika Jimbo langu la Mlimba. Huduma ya usafiri wa barabara haupatikani, Barabara yote ya kutoka Ifakara – Mlimba – Madeke – Njombe haina mawasiliano, imekatika. Upande wa huduma ya usafiri wa reli, nayo imekatika katika eneo hili. Kwa hiyo, wananchi wangu wa Jimbo la Mlimba wapo kisiwani. Leo hii ili ufike Mlimba hakuna mbadala zaidi ya kwenda na helikopta. Kwa hiyo, naiomba Serikali, Wizara husika, Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi waone namna ya kuchukua hatua za haraka kurejesha mawasiliano ya barabara na reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iwasaidie *TAZARA*. Reli imekatika, leo hii mwezi mzima umepita lakini hakuna jitihada za makusudi zinazofanywa pale na *TAZARA* kurejesha mawasiliano ya reli. Hivyo, naiomba Serikali hata kwa kutumia vikosi vyetu hivi kama SUMA JKT na hata Jeshi lenyewe, wachukue hatua pale. Ni jambo la kutoa tu ule udongo uliolala kwenye reli ili ile reli ipitike.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu lingine kwa niaba ya wananchi wa Mlimba, tunayo ile Treni ya Mwakyembe pale inayosafirisha watu kutoka Dar es Salaam kuja Mlimba. Ombi langu iongeze safari zake, badala ya kusafiri mara mbili kwa wiki, basi safari zile zifanywe angalau mara nne kwa sababu sisi wananchi wa Mlimba kwa kiasi kikubwa tunatibiwa hapa Ifakara. Kwa hiyo, leo hii akitokea mgonjwa wa Mlimba anatakiwa aende Ifakara *Saint Francis Referral Hospital*, hawezi kufika kwa sababu hakuna mawasiliano ya reli. Kwa hiyo, maombi yangu kwa kuwa najua na naamini Serikali ni sikivu, hivyo itakwenda kuwatendea haki wananchi wa Mlimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu eneo lingine, Serikali ijitahidi kuharakisha zoezi la kuwapatia chakula wananchi wa Mlimba. Tunafahamu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa inafanya kazi zake vizuri, tunafahamu Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatuma timu kule ya kufanya tathmini. Ombi letu wananchi wa Mlimba, watusaidie kile chakula kitufae sisi wananchi wa Masagati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, eneo lingine nigusie Shirika la Reli la *TAZARA*. Shirika hili la Reli la *TAZARA*, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa utashi wa Marais wawili. Rais wa Zambia na Rais wetu Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mahusiano aliyoyajenga na watu wa Zambia wamekubaliana kufanya maboresho ya Shirika letu la Reli. Maombi yangu, kuna shida kwenye upande wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria iliyoanzisha Shirika la Reli ina changamoto zake, hasa kwenye eneo la uwekezaji wa mtaji. Kwa hiyo, kwenye mabadiliko hayo, hofu yangu tusiachie tu utashi, tumwombe Waziri wa Uchukuzi atuletee mabadiliko ya sheria ya *TAZARA*. Sheria iliyoanzisha Shirika la Reli *(TAZARA)* wafanye mabadiliko kwenye eneo la uwekezaji wa mtaji. Kwa muda mrefu Serikali imeshindwa kuwekeza kwenye Shirika la Reli la *TAZARA* kwa sababu ya ombwe kwenye sheria yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake nini? Leo hii Sheria inasema, Zambia na Tanzania hisa ni 50% kwa 50%. Kwa hiyo, leo hii kinachofanywa na Waheshimiwa Marais hawa wawili ni utashi tu. Kwa hiyo, hatuna uhakika kwamba Rais mwingine atakayekuja atakuwa na utashi wa namna hii. Ili kutengeneza mazingira rafiki ya uwekezaji wa Reli ya *TAZARA*, ni muhimu sasa Waziri wa Uchukuzi atuletee Bungeni hapa mabadiliko ya Sheria ya *TAZARA* ili kuweka mgawanyo wa hisa. Yule anayewekeza mtaji zaidi, basi awe na hisa nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, labda watu hawafahamu umuhimu wa Reli ya *TAZARA*. Reli ya *TAZARA* ilianzishwa mwaka 1975. Ni kwa sababu ya kurahisisha huduma ya usafiri wa reli kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda *New Kapiri*

*Mposhi* Zambia. Hii ilisaidia kuunganisha mahusiano ya kibiashara baina ya nchi zetu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa kuwa kengele imegonga, nawaomba Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Ulinzi na hata Wizara ya Ujenzi, washirikiane kutusaidia kurejesha usafiri wa Reli ya *TAZARA*, kwani sasa hakuna mawasiliano ya reli kwa upande wa Mlimba kwenda Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chumi, ajiandae Mheshimiwa Venant Protas.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima na afya tulizonazo humu ndani. Pia kwa niaba ya wananchi wa Mafinga, napenda kutumia nafasi hii kuishukuru Serikali na Mheshimiwa Rais na wasaidizi wake wote kwa jinsi ambavyo tunaendelea kuijenga Mafinga. Hivi karibuni tulikabidhi gari la kubebea wagonjwa pale kwenye Kituo cha Afya cha Ifingo, kama hatua za kuboresha huduma za afya kwa wananchi wetu wa Jimbo la Mafinga Mjini ambalo pamoja na kuwa lina hospitali ambayo ni kama vile inahudumia Wilaya nzima na wilaya za jirani, lakini pia ipo kando ya barabara kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kupata *ambulance* ile maana yake ni kwamba inaenda kutusaidia kurahisisha utendaji. Hata hivyo, natumia nafasi hii kuomba gari kwa ajili ya kufanya tathmini. Nilizungumza na Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Festo Dugange, alinihakikishia kwamba tutapata wasaa wa kulijadili jambo hilo na kuona ni kwa namna gani watatusaidia watu wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga kupata gari kwa lengo lilelile la kuendelea kuboresha huduma za afya kwa wananchi wa Jimbo la Mafinga Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia pia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na wasaidizi wake kwa Hotuba nzuri ya Bajeti. Naipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla, kwa kuja na hii Idara inaitwa Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Shughuli za Serikali. Idara hii nimeona hapa kulikuwa na watu wa *CAG*, kwa namna fulani Idara hii inaisaidia Serikali kufanya *monitoring* ya utendaji wa kila siku wa shughuli za Serikali, hususan katika kufuatilia utekelezaji wa miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba, tofauti na siku za nyuma ambapo tungesubiri pengine mpaka mwisho ndiyo mradi uje ufanyiwe tathmini, lakini idara hii inafanya ufuatiliaji wa kazi kadri zinavyoendelea. Kwa hiyo, kama kuna mapungufu maana yake ni kwamba yatafanyiwa kazi wakati ile kazi inaendelea ili kuipunguzia Serikali hasara ambayo pengine ingekuwa imejitokeza. Kwa maana nyingine, hii ni kama vile tunasema *prevention is better than cure*, yaani kwamba hii badala usubiri kutibu, basi yenyewe inaanza kuchukua tahadhari mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo naomba kuishauri Serikali. Kwa sababu hii ni Idara muhimu sana ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Shughuli za Serikali, naomba mambo mawili muhimu. Kwanza, ili itimize wajibu wake kiufasaha na malengo yaweze kutimia, lazima tuiongezee nguvu kazi. Nguvukazi ya watu kwa maana ya watendaji, nguvukazi ya vitendea kazi na nguvukazi ya rasilimali fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kusisitiza jambo hili kwamba, ili iwe na thamani na maana halisi ya kuanzisha Idara hii, basi tuifanye kwa vitendo kwa maana ya kuiongezea watendaji, kuiongezea vitendea kazi na kuiongezea nguvu ya fedha. Kwa sababu, kazi inayofanya ni kuokoa mamilioni na mabilioni ya fedha za Serikali ambazo kama isingekuwepo, kama ingekuwa haifuatilii na kama itashindwa kufuatilia kama lengo lilivyo, maana yake ni kwamba tutashindwa kuokoa hizo fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo ningependa kushauri na kulizungumzia ni kuhusu kazi na ajira. Mojawapo ya kitu muhimu ambacho kinaweza kuimarisha suala zima la upatikanaji wa ajira ambazo ni rasmi na za kujiajiri, ni pamoja na uwepo wa miundombinu madhubuti. Kwa hiyo, nashauri sana, pamoja na kazi nzuri ambayo Ofisi ya Waziri Mkuu imeifanya katika hizi siku za karibuni kukabiliana na maafa kutokana na mafuriko, kutokana na miundombinu ya maeneo mbalimbali ya barabara kuharibika, naomba na kushauri, hili liwe kama funzo na fundisho kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba huwa tunakuwa na fedha ya dharura na inawezekana bajeti yetu ikawa ni finyu kiasi kwamba tusiwe na fungu kubwa la dharura, lakini maafa yaliyojitokeza mwaka huu, yawe funzo kwetu na tujielekeze kwa kiwango kikubwa kuwa na fedha za dharura *especially* kwa ajili ya miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivi? Sasa hivi ilivyo kama sehemu ya watu kujiajiri, nchi yetu asilimia kubwa ni wakulima. Leo hii miundombinu maeneo mengi hakuna mawasiliano. Nitatoa mfano tu, pale Mafinga Barabara ndogo tu ya kutoka Uguta kwenda Kikombo kalavati limezolewa na maji. Maana yake ni nini; wananchi kutoka Mafinga kwenda Kikombo kupeleka bidhaa watashindwa kwenda ama itabidi watumie safari ndefu kuzunguka maeneo ya Rungemba na Kitelewasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, wananchi hawa kutoa mazao yao kuyapeleka sokoni Mafinga Mjini, ama watashindwa kama mazao yao ni mali mbichi zitawaharibikia au itabidi wazunguke kwenda Rungemba ili wafike sokoni, maana yake tunawaongezea gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, maeneo kama kwenda Bumilayinga, maeneo kama ya Mtula ambako kuna Skimu ya Umwagiliaji, kama hakuna miundombinu ya uhakika maana yake ni kwamba kuhusu kipengele kizima cha kazi na ajira, hakitakuwepo kwa sababu hakuna *movement*, kutakuwa hakuna ajira kwa sababu hakuna *movement*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, hata matengenezo ya magari leo hii watu wa vibasi kama *hiace* wanaokwenda Mufindi kwa pale Mafinga, anatumia masaa mengi kufika kwenye kituo anachokwenda, lakini akienda akirudi atakuwa na gharama kubwa sana za ku-*service* chombo chake. Kwa hiyo, hata kile alichokipata kama sehemu ya kujiajiri na chenyewe chote kinapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu; tuwekeze katika miundombinu na ikiwezekana sijui kama nitaeleweka, lakini katika bajeti ya mwaka huu, kama kuna kitu ambacho inabidi tukiwekee macho mawili ni sehemu ya kuimarisha miundombinu. Leo hii Mafinga, Mufindi hata maeneo ya Njombe, watu wanaofanya shughuli zao za msitu hawawezi kwenda msituni kusomba magogo au kufanya shughuli zao kwa sababu miundombinu na barabara hazipitiki kwa namna inayotakiwa. Kwa hiyo nguvu yetu na akili yetu kama Taifa tuwekeze sana katika miundombinu kwa sababu kwa kuwepo miundombinu imara maana yake ni kwamba tutakuwa tumejitengenezea ajira kwa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yawezekana kabisa huu ukawa ni mzigo mkubwa sana kwa Serikali; ushauri wangu, tulipitisha hapa Sheria ya *PPP*, hebu tujaribu kuitumia sheria hiyo kuona kwa namna gani tuta-*engage private sector* katika kuimarisha na kujenga miundombinu. Nchi yetu ni kubwa, Serikali kwa hakika kama tutasema ijenge peke yake itachukua miaka mingi kuweza kuwa na miundombinu ya uhakika. Kwa hiyo tutumie utaratibu shirikishi wa kutumia sekta binafsi kujenga miundombinu katika baadhi ya maeneo. Naamini ni salama zaidi kwa wananchi kuongeza gharama kidogo, lakini wakafika kwa wakati na kwa usafiri wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la mwisho kwa kumalizia katika hili hili la ajira na kazi, naomba kuishauri na kuipongeza Serikali kwa mpango wa *BBT*. Sasa, kwa sababu hii ni programu, ushauri wangu bado naendelea kusisitiza ndani ya Serikali kushirikiana, JKT, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Kilimo tuone kwa namna gani tunaweza tukawashirikisha vijana ambao

wanaenda JKT kwa nia ya kujitolea, wanapata mafunzo ya uzalishaji mali, mafunzo ya nidhamu na kwa namna gani tutawa-*incorporate* kwenye mpango wa *BBT*, naamini watakuwa na tija kwao kama sehemu ya kujiajiri, lakini pia watakuwa na tija kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kuhusu Mradi wa *TACTIC*. Huu ni mradi wa kuboresha miji, manispaa na majiji kama ilivyo *DMDP* katika Jiji lako la Dar es Salaam. Mimi Mafinga na baadhi ya miji tupo awamu ya tatu. Ushauri wangu na ambao nimeutoa na nimeusema kila siku, kwa sababu mpango huu upo chini ya Benki ya Dunia na kwa sababu ni mkopo nashauri kwa kushirikiana na TAMISEMI Wabunge ambao tunatoka awamu ya tatu na ya pili tukutane ili tuweze kushauri kusudi mradi huu uweze kwenda kwa mapema na kwa haraka. Hii ni kwa sababu mradi huu pamoja na ujenzi wa barabara, lakini pia tunakwenda kujenga vitega uchumi ambavyo vitakuwa vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano sisi Mafinga tunaenda kujenga Stendi pale Kinyanambo, tunakusudia kujenga soko kubwa la mazao ya misitu na pia tunakusudia kuimarisha na kuboresha soko letu. Hivi vyote vinakuwa ni vyanzo vya mapato ambavyo hatimaye vitaipunguzia Serikali mzigo. Kwa mfano, zile fedha ambazo zingeenda *TARURA* kama miradi itatekelezwa hii ya *DMDP II* na *TACTIC* maana yake kuna *portion* itatoka *TARURA* itaenda kufanya kazi sehemu nyingine kwa sababu miradi hii itakuwa tayari imetekelezwa chini ya mpango wa Benki ya Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, Mungu atubariki wote, Mungu aibariki Mafinga, Mungu aibariki Tanzania na nawatakiwa wote mchezo mwema siku ya Jumapili kati ya Simba na Yanga. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Protas, wajiandae Mheshimiwa Mkenge na Mheshimiwa Yahaya Massare.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji katika bajeti

ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja mapendekezo yote ya bajeti ambayo yamewasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naipongeza Serikali kwa mambo makubwa inayofanya, kwa kipindi cha miaka minne ya Mheshimiwa Rais mambo mengi yamefanyika katika majimbo yetu na wananchi wote wanafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana kwenye bajeti hapa nililalamika sana kuhusu mambo mbalimbali ambayo yalikuwa yanawatatiza wananchi wangu katika Jimbo langu la Igalula, lakini kwa kuwa Serikali ni sikivu, mambo mengi yamefanyika ikiwemo ahadi za viongozi ambapo nililalamikia hapa kwamba, walikuwa wanakuja kwenye majimbo yetu, wanatoa ahadi, halafu wanaondoka moja kwa moja na kilio kile walikisikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nililalamikia wodi waliyokuwa wameanzisha wananchi, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda pale Imalakaseko akaahidi shilingi milioni 80 na leo milioni 80 imekwishakwenda na wodi imeshakamilika. Nawashukuru sana Serikali na namshukuru Mheshimiwa Jenista, aliisimamia kwa nguvu zote akasema yote yatakwenda, kwa hiyo niishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna changamoto chache chache ambazo bado hazijakamilika, lakini kwa usikivu wa Serikali naomba nikumbushe kwamba, tarehe 17 Mei, 2022, Mheshimiwa Rais alikuja katika Mkoa wa Tabora katika ufunguzi wa Barabara ya Chaya - Nyahua. Alipokuwa jimboni kwangu tulimpelekea maombi kadhaa, baadhi ya maombi aliyatolea ufafanuzi na akatoa maelekezo kwa Mawaziri. Ombi la kwanza, Mheshimiwa Rais, alitoa maelekezo ijengwe Shule ya Msingi Igalula ambayo Mradi wa *SGR* umepita, akatoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mkuu ile shule ijengwe, lakini mpaka leo shule bado haijajengwa. Kwa hiyo naikumbusha Serikali ahadi ya Kiongozi wetu Mkuu ilindwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, tulimwomba ujenzi wa Daraja la Loya katika Mto Loya ambalo kila mwaka wananchi wanakufa kwa sababu ya kutokupitika. Katika ahadi hii alitoa

maelekezo, naiomba niikumbushe Serikali. Serikali yetu ni Sikivu, nadhani wamekwishasikia na watu wapo hapa watafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba nina maombi machache, kwa kuwa sisi kazi yetu ni kuleta matatizo ya wananchi na Serikali kusikiliza matatizo ya wawakilishi wa wananchi. Ombi la kwanza, sisi Jimbo la Igalula tumepitiwa na mradi mkubwa wa *SGR* na baadhi ya maeneo ulikopita ni kwenye makazi ya watu. Kwanza nianze kuishukuru Serikali imekwishaanza kulipa fidia. Nilileta hapa maombi kwamba kuna watu waliifuata reli, leo Mheshimiwa Rais baada ya kuyasikia maombi hayo wale waliokuwa wameifuata reli walitakiwa wasilipwe hata shilingi 10, kwa mapenzi ya dhati ya Mheshimiwa Rais, leo wamelipwa kifuta jasho kwa sababu walikuwa wamekwishaendeleza maeneo hayo. Wananchi haoa wamenituma nitoe shukurani kwa Mheshimiwa Rais, fedha hizo wameshazipokea na wamekwishaanza ktengenezea makazi sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna changamoto ya baadhi ya watu ambao bado hawajalipwa fidia wa katika Kata za Goweko na baadhi katika Kata za Igalula. Niiombe Serikali, tathimini kisheria ikipita miezi sita lazima wakafanye tathmini upya na leo imekwishapita zaidi ya miezi 10 na kidogo. Kwa hiyo niiombe Serikali kabla ya Bunge hili la bajeti kuisha, watu wote wa Jimbo la Igalula ambao walitakiwa walipwe fidia katika Mradi wa *SGR,* basi wawe wamelipwa na kama watakuwa hawajalipwa basi Serikali warudi wakafanye tathmini upya ili sasa tuendane na matakwa ya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kulipa makaburi, wameleta kizungumkuti kule, wananchi tulikwenda tukawaomba tuhamishe mahali ambapo walikuwa wamewazika wapendwa wao na wananchi waliunga mkono juhudi za Serikali, lakini wananchi kila siku wanaahidiwa wiki ijayo, wiki ijayo. Wananchi wa Kata za Igalula, Kata za Goweko, Kizengi pamoja na Tura wametoa maeneo kwa nia ya dhati ili kuendeleza mradi wa Serikali, wakahamisha makaburi yao, lakini mpaka leo hakuna kinachoendelea. Niiombe Serikali waweze kuwalipa wananchi

hao hasa waliotoa maeneo yao kwa mapenzi ya dhati ya kupisha Mradi wa *SGR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine nina maombi katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Hapa wamezungumza na Waheshimiwa Wabunge wameuliza maswali hapa; sisi katika halmashauri yetu ya Wilaya ya Uyui tulileta mapendekezo ya kuiomba Serikali ione namna ya kulipunguza eneo la kiutawala ikiwemo kuomba halmashauri nyingine ya Kizengi. Mheshimiwa Rais alipokuja katika ziara Mkoa wa Tabora tulimpa ombi hilo, alituahidi akasema tengenezeni *document* kutokana na matakwa ya Serikali na bajeti zake ili siku wakihitaji kutoa maeneo ya kiutawala Wilaya ya Uyui ina sifa na uwezekano wa kupewa kwa sababu Wilaya ya Uyui kijiografia imekaa vibaya zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mtu akitoka Tura kwenda kuifuata Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, anatumia zaidi ya shilingi 20,000 lakini anatembea zaidi ya kilomita 200 na kidogo kwenda Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Uyui. Leo mgonjwa akipatikana katika Kata ya Loya anatakiwa kwenda Hospitali ya Wilaya yetu ya Halmashauri ya Wilaya ya Uyui anatembea zaidi ya kilomita 180 kuifuata kule huduma. Tukaona ni vyema sasa tupate halmashauri nyingine ambayo itakaa Makao Makuu katika Kata ya Kizengi na halmashauri hiyo tukasema itaitwa Halmashauri ya Kizengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa ni bajeti yake hii na tutasikiliza Ofisi ya Rais, TAMISEMI nini wamepanga kwenye bajeti hii, basi haya maeneo ambayo wananchi wanafuata huduma umbali mrefu waone namna gani ya kupunguza, ikiwemo kugawa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui kuwa na halmashauri mbili na kuongeza tarafa moja ya Kata ya Kizengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maombi yangu mengine Wilaya ya Uyui pamoja na ukubwa wake tuna Mkuu wa Wilaya ana kata 30, leo Wilaya ya Uyui ina *square kilometre* za mraba 11,000 na Mkuu wa Wilaya ni mmoja. Sasa kumekuwa na changamoto ya kutokuwepo na gari la uhakika la Mkuu wa

Wilaya. Niiombe Serikali, kwa kuwa hawa Wakuu wa Wilaya ni wasaidizi wa Mheshimiwa Rais, Wakuu wa Wilaya wanatusaidia kwenda kusikiliza kero wakati Mbunge akiwa katika majukumu ya kibunge na wakati Mheshimiwa Rais na Mkuu wa Mkoa wakiwa na majukumu mengine. Leo Mkuu wa Wilaya akishindwa kwenda kusikiliza kero kwa sababu ya kutokuwepo kwa uhakika wa usafiri basi, anaiangusha Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali yetu, Wakuu wa Wilaya wote wenye changamoto ya usafiri, ione namna gani ya kuwasaidia ili waweze kupata usafiri wa uhakika wa kwenda kuwasikiliza wananchi, akiwemo Mkuu wangu wa Wilaya ya Uyui ambaye amekuja kwa kasi, anakwenda kijiji kwa kijiji muda wote. Sasa ili asivunjike moyo, basi apate usafiri wa kufaa wa kuwafikia wananchi na kuwasikiliza kero zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Igalula pamoja na Tanzania nzima tumepata majanga ya kuongezeka kwa mvua, lakini kuna uharibifu mkubwa wa barabara hasa katika Barabara ya Goweko – Igalula - Ndevelwa. Awali mwananchi alikuwa anasafiri kwa shilingi 3,500 hadi 4,000, sasa hivi kwenda kuifuata huduma kwa kutumia hiyo Barabara ya Goweko – Igalula - Ndevelwa anatumia zaidi ya shilingi 20,000. Sasa anatumia shilingi 20,000 na muda anatumia kwenda huko ni zaidi ya masaa 10 ilhali zamani alikuwa anatumia zaidi ya masaa mawili kufuata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali, Jimbo la Igalula tumepata athari kubwa ya barabara, ikiwemo barabara ya Igalula – Kigwa kilomita 19 ambayo haipitiki, Goweko – Manta – Kigwa haipitiki. Vilevile barabara ya Mpumbuli – Izumba kuna mashimo makubwa nayo ni changamoto kwa wananchi na haipitiki, Mabeshi – Loya haipitiki, Izumba – Matuga – Isuli imekatika madaraja na kwa hiyo haipitiki. Niiombe Serikali kwa hizi barabara zinazofungua uchumi ipeleke huduma kwa haraka ili wananchi waweze kupata huduma...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venant Kengele ya pili hiyo.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante kwa muda wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Mkenge, ajiandae Mheshimiwa Massare.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii leo ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika bajeti hii ambayo imewasilishwa hivi punde. Kwanza kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya katika kushughulika na masuala mbalimbali ya kiserikali. Pia niwapongeze Mawaziri walio chini yake nikianzia na dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, ndugu yangu Mheshimiwa Katambi, ndugu yangu Mheshimiwa Ndejembi pamoja na dada, Mheshimiwa Ummy Nderiananga kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya, kwa kweli ni Mawaziri wa mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nataka kwanza nitumie nafasi hii kuwapa pole ndugu zangu wa Rufiji na Kibiti kwa maafa makubwa ambayo yamewakumba, kwa kweli ni changamoto kubwa sana ambayo wameipata. Nipende kuchukua nafasi hii kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inashughulika na Kitengo cha Maafa kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika maeneo ya Kibiti na Rufiji. Kwa kweli wanatutia moyo na wanawapa watu hali na moyo wa kuiona Serikali yao jinsi gani inawathamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitazungumzia suala la miundombinu. Kwa kweli Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mama yetu Samia Suluhu Hassan wanajitahidi sana sana katika suala la miundombinu, lakini bado tuna changamoto kubwa sana ambazo zinatukabili katika suala zima la miundombinu. Ningependa kuzungumzia hasa katika Jimbo langu la Bagamoyo. Leo hii Bagamoyo kuna barabara ambazo hazipo sawa, barabara ambazo zimekumbwa na mafuriko na zimeharibika vibaya sana. Nikichukulia Barabara moja ambayo inatoka Mingoi kwenda Kiembeni, barabara hii ilikuwa katika ahadi ya Mheshimiwa Rais, katika ujenzi wake lakini leo hii

barabara hii imekuwa haipitiki. Wananchi wanapambana na kujitahidi kadri siku zinavyokwenda kuhakikisha wanaweka sawa barabara hii kwa nguvu zao, lakini bado barabara ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu suala la daraja. Serikali kama inakumbuka mnamo tarehe 3 Januari, 2023, ilitia saini Mkataba wa Ujenzi wa Daraja la Mpiji, daraja ambalo linaunganisha Bagamoyo na Dar es Salaam. Daraja hili kwa kweli tangu mkataba umeingiwa na Wachina wale ambao wanataka kujenga hili daraja wamefika pale, sasa hivi muda mrefu unakwenda Wachina wameweka kambi lakini hakuna chochote kile ambacho kinaendelea kufanyika mpaka sasa hivi. Kwa hiyo niwaombe Serikali, kwa sababu tushaingia mkataba, basi wajitahidi daraja hili ili liweze kujengwa kwa sababu ni daraja ambalo ni kiunganishi kikubwa sana kati ya Bagamoyo na Dar es Salaam. Vilevile ni daraja ambalo litakapokamilika litapunguza foleni iliyopo katika njia ya Bagamoyo na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia barabara nyingine, barabara ya kutoka *TAMCO* Kibaha kuja Baobab Mapinga. Mkataba wa barabara hii ulitiwa saini tangu tarehe Mosi Julai, 2023 na mkandarasi alishaanza kazi, lakini cha kushangaza kwamba kasi ya ujenzi wa hii barabara ni ndogo sana na hairidhishi. Kwa hiyo niombe Serikali kuhakikisha kwamba wanaongeza kasi katika ujenzi wa barabara hii inayotokea *TAMCO* kuja Mapinga Baobab ili iweze kuhudumia wananchi katika shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuzungumzia barabara ya Makofia - Mlandizi. Muda mchache uliopita Mheshimiwa Mbunge mwenzangu wa Kibaha Vijijini aliulizia kuhusu barabara hii. Kwa kweli inasikitisha kwamba barabara hii tangu imeingizwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ni miongo miwili sasa hivi, zaidi ya miaka 20 inaingizwa lakini hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali ya Mama Samia, juzi wameanza hatua moja ya kufanya tathmini katika

barabara hii, lakini barabara hii bado ni changamoto kubwa sana. Kwa kweli naomba sana Serikali kuitupia macho mawili barabara hii, kwa sababu ni barabara ambayo inasaidia sana katika ukanda huu wa kuunganisha Kibaha pamoja na Bagamoyo. Juzi tu ilitokea ajali ya kuungua kwa mabasi na lori, barabara hii ilitumika sana kupitisha magari mengi ili waweze kufika Dar es Salaam kutokana na changamoto iliyojitokeza katika Barabara ya Morogoro. Niwaombe ndugu zangu wa Serikali, Wizara na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuitupia macho Barabara hii ya Makofia Mlandizi ili iweze kuwasaidia wananchi

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ambayo nataka niizungumzie ni barabara ya Makurunge – Pangani – Tanga. Barabara hii inaendelea kujengwa kwa muda mrefu na kwa kweli bado kasi yake hairidhishi. Naomba hii barabara kama ikiwezekana hawa wakandarasi nao waanze kuanzia kipande cha Makurunge kuelekea Tanga, kwa sababu kipande hiki ni muhimu sana katika uchumi wa Bagamoyo na Taifa kwa ujumla. Watakapoanza kujenga kipande cha Makurunge kuelekea Pangani kwenda Tanga kutasaidia kuifungua Mbuga ya Wanyama ya Saadani. Watalii wengi leo hii wanashindwa kwenda Saadani kuangalia wanyama kutokana na miundombinu mibovu ya barabara. Sasa barabara hii itakapokamilika itasaidia sana kunyanyua uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiachilia mbali suala la Mbuga ya Wanyama ya Saadani, bado kuna kiwanda kikubwa sana kinazalisha sukari na kuna mashamba ya miwa ya *Bagamoyo Sugar*. Bado kinahitaji barabara kusafirishia mizigo yao kupeleka na kutoa mizigo yao kutoka kule, kwa hiyo, niwaombe sana Serikali wahakikishe barabara hii wanaitupia macho. Hata ikiwezekana kuingia mkataba wa kuanza kujenga upande huu nao pia, kwa sababu itawasaidia hata ndugu zetu ambao wanazalisha miwa *(out growers)* kupeleka miwa katika Kiwanda cha *Bagamoyo Sugar. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, barabara hii itakapojengwa ya Makurunge kuelekea Saadani, itasaidia hata wazalishaji wa chumvi. Kuna mashamba mengi ya chumvi Kitame

pamoja na Saadani ambao wanategemea sana barabara hii. Kwa hiyo, naiomba Serikali kuitupia macho barabara hii katika kiwango ambacho wanakiona kinafaa. Ukiachilia mbali hilo kuna fursa nyingine vilevile, barabara hii inapotokea Makurunge sehemu kubwa ipo chini ya Serikali, kwa hiyo, Serikali haitapata gharama ya kufidia kwa watu ili kuweza kujenga hii barabara, itakuwa yenyewe imechukua eneo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kidogo katika upande wa afya; niishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kule Bagamoyo tumepata Kituo Kipya cha Afya, tumepata zahanati na vifaa tiba. Tuna changamoto kidogo bado Wahudumu wa Afya katika hiki Kituo cha Afya na hizi zahanati hawatoshelezi. Leo hii Kituo cha Afya ambacho kinakadiriwa kuchukua wafanyakazi 50, kinakuwa na wafanyakazi watano, kwa kweli utendaji kazi wake unakuwa hauridhishi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kutupia macho sana katika hili suala la Wahudumu katika Sekta ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme; tunatambua Serikali ina mkakati na ina mpango Bwawa la Mwalimu Nyerere litakapokwisha kuzalisha umeme wa kutosha. Leo hii tuna changamoto kubwa sana ya umeme na hasa katika Mji wangu Bagamoyo umeme unakatika mara kwa mara hatujui tatizo ni nini? Kila kukicha umeme unakatika mara tatu, mara nne, mara tano, malalamiko ya watu yamekuwa makubwa sana. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iangalie sana jinsi gani suala zima la uboreshaji wa miundombinu ya umeme linafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la elimu nigusie kidogo nako, kuna suala la upungufu wa madawati katika shule zetu za msingi. Tunatambua mchango mkubwa wa Serikali katika kutujengea madarasa, kutupatia madawati lakini haya madawati yanayokuja mwanzoni wakati madarasa yanajengwa yakishakwisha au yakishaharibika hakuna mbadala. Shule nyingi sasa hivi wanafunzi wanakaa chini kutokana na upungufu wa madawati. Kwa hiyo, tulitupie macho suala hili la madawati kwa vijana wetu ambao wengi wao sasa hivi wameshaanza kukaa

chini kutokana na uchakavu wa hii miundombinu ya madawati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nigusie vilevile suala la uvuvi; nimshukuru Mheshimiwa dada yangu Ummy Nderiananga, alikuja Bagamoyo kuja kukagua eneo la kujenga vichanja vya kuanikia samaki, kwa kweli Wizara inajitahidi. Nataka nizungumzie kitu kimoja, bado katika Wizara ya Uvuvi, kuna ahadi zao hawajakamilisha. Pale kwangu Bagamoyo waliniahidi boti ya uvuvi kwa ajili ya wakulima wa mwani katika Kikundi cha Msichoke kilichopo Mlingotini. Boti pamoja na vifaa vyote mpaka sasa hivi bado havijapatikana na huu sasa hivi ni mwaka wa pili. Naomba Serikali ile ahadi waliyoitoa ya boti katika Kikundi cha Msichoke ambacho kipo Mlingotini pamoja na vifaa vyake, basi waitimize ili kuhakikisha kwamba, wananchi wale wanafanya mradi wao kwa kujiamini zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba niishukuru tena Serikali na niishukuru Wizara. Naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Massare, wajiandae Mheshimiwa Genzabuke na Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi, nimshukuru Mungu kwa kupata fursa ya pumzi, lakini kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu, kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ameitoa juzi na naamini leo anaenda kuhitimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri ambazo zimefanyika katika Majimbo yetu likiwemo Jimbo langu la Manyoni Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapompongeza Mheshimiwa Rais, huwezi kuacha kuwapongeza wanaofanya kazi chini yake akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, kwa kazi zake nzuri lakini usikivu ndani ya nyumba hii tukufu na kubwa. Pia niwapongeze Mawaziri wanaomsaidia akiwemo Mheshimiwa Jenista Mhagama, ambaye kwa kweli anafanya kazi za kiwango cha juu sana na usikivu ambao ni wa kipekee katika Mawaziri waliopo katika Serikali hii, pia, Manaibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoipongeza Serikali tunapongeza na kuona namna gani wamefanya kazi katika maeneo yetu. Kwa miaka hii mitatu tumeshuhudia mageuzi makubwa sana katika ujenzi wa miundombinu ya elimu, afya na maji, ikiwemo miundombinu ya barabara na mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoipongeza Serikali pia kuna changamoto kadha wa kadha ambazo tunapaswa kuzisemea sisi kama Wawakilishi wa Wananchi ambao tumeletwa humu ili kuwasemea watu ambao wametutuma humu. Mimi ni Mbunge ninayetoka katika Majimbo ya Vijijini, watu wetu zaidi ni wakulima, niipongeze Serikali, Wizara ya Kilimo kwa mipango waliyonayo sasa kwa kiasi fulani inaonesha mwelekeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo ambalo nataka niishauri Wizara hii, ili tuwe *hub* ya chakula katika ukanda huu, tunapoenda kuwafundisha watu kulima kuna watu ambao siku zote walikuwa wanalima. Bei za pembejeo, bei za mbegu bado siyo rafiki kwa kilimo chetu. Wizara hii ilipoongezewa pesa kwa asilimia 300, nilitarajia wangeweka ruzuku katika pembejeo kwa kiasi kikubwa. Unapopunguza bei za matrekta unamsaidia si yule aliyenunua treka unasaidia walio wengi ambao wako katika eneo lile trekta moja linaweza kuwasaidia wakulima zaidi ya 30, 40, 50 katika eneo moja, maana yake tutaongeza nguvu kazi ya kilimo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya mbegu si rafiki, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alihimiza watu wa Singida, Simiyu na Dodoma kulima sana alizeti, lakini bei ya mbegu nzuri za alizeti hazinunuliki, matokeo yake watu wananunua mbegu hizi ambazo ni za kawaida na tija inakuwa ndogo. Niiombe Serikali ione namna gani

ya kuweka ruzuku katika mbegu, mbegu za mafuta, mbegu za chakula kama mahindi, bado bei ya mbegu unauza zaidi ya debe moja kupata kilo moja ya mbegu ya kupanda, kwa kweli hii siyo sawasawa na si haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze tena Serikali kwa mara nyingine katika eneo langu tunajenga Barabara ya kutoka Mkiwa kuelekea Mbeya kwa kilomita 56. Kwa kweli barabara ile inajengwa kwa kiwango kizuri sana na mtiririko unaonekana ni mzuri. Tunapojenga barabara upande wa *TANROADS* hakuna shida, kuna changamoto upande wa *TARURA*, bajeti yao haitoshi na barabara nyingi za vijijini zinasimamiwa na *TARURA* pamoja na miji. Kwa hiyo, matokeo ya mvua hizi kubwa ambazo ni neema kwa upande mmoja, lakini upande mwingine zimeleta majanga makubwa ya miundombinu hii kuharibika. Kwa hiyo, niiombe Serikali ione namna gani bora ya kuiwezesha *TARURA* kuwa na bajeti ya kutosha ili kukabiliana na changamoto hizi nyingi ambazo zipo katika barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Itigi pana mradi wa kilomita 10, unatekelezwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja pale nilimwomba taa kidogo kama 200 na kidogo na akatoa ahadi kwamba, zitatekelezwa, lakini hata Mheshimiwa Rais, alipokuja mwaka jana aliwaagiza watu wa *TANROADS* kufunga zile taa lakini mpaka saivi ni kimya. Naomba majibu ya Serikali lini wanaenda kufunga taa zilizoahidiwa na Mheshimiwa Rais alipokuja Itigi wakati anaweka jiwe la msingi la Barabara ya Mkiwa- Itigi na Noranga, kwa sababu, wananchi wanasubiri na kuona ahadi za viongozi wakubwa kama Mheshimiwa Rais, zinatekelezwa kwa haraka lakini kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo changamoto nyingine tunajenga Reli ya kiwango cha *Standard Gauge,* Itigi ni maeneo ambayo reli hii inapita, lakini inapita maeneo ambayo watu wamechukuliwa maeneo yao yakiwemo mashamba. Wengine wamechukuliwa maeneo ambayo walikuwa wanayatumia kwa maslahi mapana na kufanya maisha. Mimi ni mmoja wa watu waliochukuliwa shamba eneo langu ambalo nilikuwa nalitumia eti unalipwa hekari moja shilingi 200,000, hivi kweli hapa Tanzania

kuna eneo linauzwa hekari shilingi 200,000? Jirani uliyepakana naye analipwa kwa *square meter.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itende haki kwa wananchi wote bila kuangalia huyu ana rangi gani? Huyu ana ukubwa gani? Huyu yupo eneo gani? Huwezi kumlipa jirani yake kwa *square meter* na jirani mwingine ukamlipa kwa hekari, naomba Serikali itende haki. Mimi ni miongoni mwa wale ambaye sijachukua cheki yao kwa sababu, unalipwa eti hekari mbili *square meter* 8,000 unalipwa shilingi 500,000 kitu ambacho hakiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali sikivu ya Mheshimiwa Rais, wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye analipa hata watu waliokuwa wameifuata reli. Leo watu waliofuatwa na reli kwa hekari wanapunjwa. Naomba Serikali iache dhuluma hii ambayo inafanyika kwa watu wa Itigi, ni dhuluma kubwa wapo walioridhia. Basi wale ambao hawajaridhia haraka nao walipwe kulingana na wale wengine ili haki itendeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wachaguliwa ndio huwa tunalaumiwa kwamba, hatutetei watu wetu, kwa sababu Serikali inapofanya makosa kama haya, inapodhulumu watu hekari shilingi 200,000, Itigi shamba hekari moja linauzwa zaidi ya milioni mbili lakini wao wanalipa shilingi 200,000. Naomba Serikali isikie na ilifanyie kazi jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niishauri Serikali yangu namna gani tunatumia pesa nyingi kununua mafuta ya petroli. Tunayo gesi yetu hapa tumeona Vituo vya Gesi Dar es Salaam. Matumizi ya *CNG* sasa yameshashika kasi, wakati tunasubiri mchakato wa *LNG* ambao unaonekana unakwenda mbele nyuma. Basi *CNG* ichukue nafasi ili haya magari madogo yanayotumia petroli yaweze kutumia gesi kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vilivyopo ni vichahce sana Serikali inashindwa nini kuongeza Vituo vya *CNG* Dar es Salaam? Serikali inashindwa nini kusogeza *pipe* ya *CNG* kufika Morogoro?

Serikali inashindwa nini kusogeza *pipe* ya *CNG* kufika Dodoma? Serikali inashidwa nini kuifanya *CNG* ifike Mwanza? Ifike Arusha? Ifike Mbeya? Ili tupunguze manunuzi makubwa ya mafuta ya petroli ambayo yana gharimu pesa nyingi. Mafuta ya petroli kwa kiasi kikubwa hayaja-*stabilize* kila siku bei hazieleweki mara imepanda mara imeshuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna *CNG* hapa ambayo kiasi cha lita 10 za petroli manunuzi yake kwenye *CNG* unanunua zaidi ya lita 30, kilo 30 maana yake ni nafuu. Matumizi ya *CNG* ni mazuri zaidi pahali ambapo umetumia kilometa 10 za petroli kwenye *CNG* ungetumia kilometa 30, kwa kilo moja ya *CNG*. Kwa hiyo, maana yake nini? Naomba niishauri Serikali ione umuhimu hata kama ni kukopa pesa tuwekeze hapa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuepuke namna ya kutumia pesa nyingi kutoa mafuta kutoka huko Uarabuni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Massare, kwa mchango mzuri.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke, ajiandae Mheshimiwa Neema, baada ya Mheshimiwa Neema, atafuata Mheshimiwa Khadija Taya.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya na kunipa kibali cha kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya, Watanzania wanaona wana macho. Kwa hiyo, tunaomba tuendelee kumpa moyo sisi wanawake wa Tanzania tupo nyuma yake na tunaamini itakapofika 2025 ni nginjanginja mpaka Ikulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya, pia, nimpongeze Naibu Waziri Mkuu naye kwa jitihada zake anazozifanya kwa kuungana na Waziri wake Mkuu, nimpongeze Mheshimiwa Jenista Mhagama, sisi wengine ni mwalimu wetu, lakini niwapongeze na Mawaziri ambao wanafanya naye kazi katika Ofisi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia katika maeneo manne tu, nitachangia kwenye reli, nitachangia kwenye umeme na kwenye kilimo. Nianze kwenye reli; ninafahamu kabisa na naona juhudi zinazofanyika kuhakikisha reli ya kati inajengwa. Reli ya kati itakapokuwa imekamilika itakuwa ni mkombozi mkubwa kwa watu wa Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi, kwa sababu kwa muda mrefu sana tumekuwa tukipata shida katika usafiri wa reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, reli hiyo itakapokamilika itakuwa ni mkombozi kwa wananchi na hasa kwa wananchi wa kipato cha chini. Wataweza kusafiri kwa gharama nafuu lakini pia wataweza kusafirisha mizigo yao kuitoa sehemu mbalimbali kuipeleka sokoni. Kwa hiyo, naomba juhudi za Serikali ziongezeke ili kumpata huyo Mshauri Msimamizi na Mkandarasi ili kazi hiyo iweze kukamilika mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umeme vijijini; tunafahamu kazi kubwa inayofanywa na Serikali chini ya Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni Waziri wa Nishati, kwa kweli anafanya kazi kubwa na sisi tunaona. Tuwaombe wakandarasi wale ambao wapo *site* kwenye mikoa yetu, wakandarasi wale wa *REA* waweze kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii na kuweza kukamilisha miradi hiyo ili tunapofika mwaka kesho angalau miradi hiyo iweze

kuwa imeleta tija. Tunaomba vijiji viweze kuunganishwa lakini pia umeme uweze kufika kwenye Vitongoji wananchi waweze kunufaika na umeme huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze kwenye kilimo; tunafahamu kwamba kilimo kimeajiri wananchi wengi sana na hapa nimpongeze Mheshimiwa Bashe kwa kazi kubwa anayoifanya kuhakikisha kinakuwa ni kilimo chenye tija. Kilimo ambacho kinawaajiri wanawake wengi, vijana wengi ambao mpaka sasa wanajitahidi kufanya kazi japokuwa bado miundombinu siyo rafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa mwaka huu angalau kile kilio cha mbolea kimepungua, ukienda madukani unaikuta mbolea. Kwa hiyo, angalau kile kilio cha mbolea sasa hivi kimepungua. Bado changamoto ipo kwenye mbegu tunaomba sasa Serikali iweze kuweka bei elekezi hata kwa mbegu nyingine tofauti na pamba, wakulima wa pamba na wakulima wa kahawa angalau wao wamepata ruzuku kwenye pamba na kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba sasa Serikali iweze kutoa bei elekezi kwa mbolea ili watu wanaolima alizeti, maharage na mahindi waweze nao kupatiwa mbegu kwa ruzuku. Wakipata mbegu bora wataweza kuzalisha mazao mengi sana na wataweza kukuza kipato chao, hatimaye, kuweza kuchangia pato la Taifa. Kwa hiyo, naomba Serikali iweze kuliangalia eneo hilo la mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sukari; mwaka huu tumeona jinsi sukari ilivyoleta shida, lakini nampongeza Mheshimiwa Bashe alivyopambana kuhakikisha sukari inarejea kutoka kwenye kuuzwa kwa shilingi elfu kumi, shilingi elfu nane na kisha kurudi na kuwa shilingi 2,500. Kwa kweli, amefanya kazi kubwa sana, kupambana na walanguzi siyo kazi rahisi. Mheshimiwa Bashe nampa maua yake, amewasaidia wananchi na hasa ulipofika Mwezi wa Ramadhani tayari sukari ilikuwa imeshuka bei na kuwa shilingi 2,500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ilete Sheria Bungeni ili kufanya mabadiliko kwenye upande wa sukari, itungwe Sheria ambayo itafanya wananchi wasirudie tena kupata shida. Sheria ikiletwa Bungeni ikafanyiwa mabadiliko, naamini hakutakuwa tena na kilio cha sukari pia sidhani kama walanguzi wataendelea kuficha sukari kama wanavyofanya siku zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma tunalima zao la muhogo, zao hili ndilo linalochangia kwa kiasi kikubwa wananchi wa wilaya zote za Mkoa wa Kigoma waweze kukuza kipato chao. Mwaka jana zao hili lilikuwa na bei nzuri sana, lakini mwaka huu zao la muhogo Mkoa wa Kigoma limeanguka sana, wananchi wamepata hasara. Tunaomba Serikali ije na bei elekezi ili wakulima wanapolima zao hili wawe na uhakika wa bei elekezi ambayo haitawapa hasara. Vilevile tunaomba kujengewa soko la muhogo ndani ya Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Neema Mwandabila, wajiandae Mheshimiwa Khadija Taya na Mheshimiwa Dkt. Mollel, Naibu Waziri.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia asubuhi hii, nina yangu machache ambayo ni ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, natamani kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Mheshimiwa Judith Kapinga ambaye ni Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara hii ya Nishati kwa kufanikisha kupata umeme huu wa megawati 235, sisi kama Taifa kwetu ni faraja. Kumekuwa na *stabilization* ya umeme kwenye Taifa, zile kelele za umeme zimepungua, kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri. Kwa asilimia 96 ambayo bwawa limefika ni kwamba, zoezi la mgao wa umeme katika nchi hii

litaisha kabisa ndani ya muda mfupi, kutakuwa hakuna mgao wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia natumia nafasi hii kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupatia Chuo cha *VETA* pamoja na Chuo cha Watu Wenye Ulemavu katika Mkoa wa Songwe, ni faraja kwetu. Tunaomba wadau wote wa vyuo na vyuo vikuu waje kuwekeza katika Mkoa wetu wa Songwe kwani tunahitaji kuendelea kielimu. Kwa hiyo, natumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara ambayo iliona kwamba, upo umuhimu wa kupeleka vyuo hivi katika Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti ya mwaka jana ya Ofisi ya Waziri Mkuu niliuliza kuhusu suala la Sera ya Lishe, nikaambiwa ndani ya miezi sita tutapata matokeo ya kinachoendelea. Mpaka ninapoongea hivi sasa sijasikia, sijapata ufafanuzi na wala sijaona taarifa yoyote inayoonesha sera hiyo imefikia hatua gani, hata kwenye taarifa hii ambayo imetolewa na Waziri Mkuu haimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa kuwa kimya kwenye hii Taarifa ya Waziri Mkuu iliyotolewa hapa Bungeni inaonesha kwamba, katika suala la Sera ya Lishe hakuna kinachoendelea. Kwa hiyo, naomba kupitia Bunge hili, Waziri atakapokuwa ana-*wind up* aje na majibu ni kwa nini haijaonekana kwenye taarifa hii? Je, inafanyiwa kazi au haifanyiwi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine, natamani kutumia nafasi hii pia kuongelea suala la kikokotoo. Tunapoongelea kikokotoo kumekuwa na kelele nyingi sana kwenye jamii, hususani kutoka kwa watumishi. Wengi wame-*develop* hofu ambayo inawafanya wanapoelekea kustaafu wahisi kama Serikali inawadhulumu. Mimi pia kabla sijapewa mafunzo nilikuwa kama hao wananchi, lakini kwa mafunzo ambayo nimepatiwa kuhusu kikokotoo nimewaza ni wapi, kama Taifa, tunashidwa kuwaelimisha wananchi hususani watumishi kwamba, kikokotoo hiki ni kizuri, kina tija na kinamweka mstaafu katika hali nzuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokiona ni kwamba, Wizara haijawafikia watumishi na kuwaelimisha vizuri kuhusiana na kikokotoo kwa sababu, kwanza fedha ya mkupuo ambayo wanapewa ni ya kutosha. Sasa wanapewa asilimia 33 kutoka asilimia 25 waliyokuwa wanapewa awali, kwangu naona kuna ongezeko la asilimia nane ambayo huenda wananchi hawana ufahamu mzuri wa tofauti ya walichokuwa wanakipata awali na sasa imekaaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na nilivyoelekezwa, nilivyofundishwa, kwenye mafunzo maalum inaonesha kwamba, mwisho wa mwezi mtumishi huyu ambaye amestaafu anaendelea kupokea kipato ambacho ni karibu na mshahara wake aliokuwa anaupata awali. Kitu ambacho kinawasaidia wastaafu ambao walikuwa wanachoka sana baada ya kustaafu na wengi wanasema walikuwa wanakufa. Kwangu mimi naona kama hali ipo hivi kelele zinatoka wapi? Pia bado kuna fungu la mkupuo kwa familia endapo mstaafu huyu atafariki. Kwa hiyo, kwa hili natamani Wizara iende kutoa elimu hii kwa wananchi, kwa watumishi, ili wajiandae na kustaafu ilhali wakijua baada ya kustaafu watapata faida zipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia kwenye Mifuko ya Hifadhi ambayo ni *NSSF* na *PSSSF* bila kuusahau Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Kimsingi wanafanya kazi nzuri, wanajitahidi na wanapambana kuhakikisha wanalinda thamani ya fedha kwa kuanzisha miradi ambayo inaendelea kuipatia kipato Mifuko hii, lakini kuna changamoto ndogo ambayo Wizara haina budi kuifanyia kazi. Kwanza ni kuondokana au kuepuka miradi ambayo marejesho yake ya fedha yatachelewa zaidi ya miaka 10. Nasema hivi kwa sababu miradi mingine inayoibuliwa inachukua muda mrefu kurudisha gharama na kuanza kupata faida. Kwa hiyo, namwomba Waziri asaidie, ili miradi isichukue muda mrefu wa marejesho ya thamani ya fedha ambayo inakuwa imewekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu Kamishna wa Kazi na Mkurugenzi wa *OSHA*, watu hawa wanafanya kazi nzuri. Ombi langu kwa Waziri ni awasaidie kuongeza ofisi katika

mikoa mingine. Tunatambua mahali pa kazi ni sehemu inayopaswa kuwa salama, kazi zipo katika mikoa yote, haiwezekani mkurugenzi akawa anateseka kutoka mkoa mmoja hadi mwingine kuhakikisha kazi inafanyika wakati Serikali ingeweza kutengeneza mazingira rahisi ya ufanyaji kazi. Vivyo hivyo Kamishna wa Kazi naye atengenezewe ofisi katika mikoa mingine na pia apewe vitendea kazi vya kutosha pamoja na watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja kuhusu kupeleka fedha kwenye maeneo ambayo Serikali inakuwa imedhamiria. Upo mfano hai, kuna fedha ambayo ilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika shule fulani katika Mji wetu wa Tunduma, shule ile ina madarasa 36 ambayo yapo na yanahitaji ukarabati. Madarasa 18 yapo yanatumika, lakini Serikali imepeleka fedha kwa ajili ya kujenga madarasa mengine 10 wakati kuna vyumba vingine 18 vya madarasa ambavyo havitumiki. Sasa nawaza na kujihoji kwamba, hivi Serikali inapopeleka fedha kwenye maeneo yetu, inakuwa imefanya tathmini ya kina ya mahitaji ya watu katika maeneo husika?

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hivi kwa sababu, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ziara zake amekuwa mkali sana juu ya matumizi mabaya ya fedha, hata kitendo cha kupeleka fedha ambazo ni kinyume na mahitaji ya eneo husika pia ni matumizi mabaya ya fedha. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie, wanaposambaza fedha kwenye maeneo yetu wazingatie vipaumbele, kama kipaumbele chetu ni ukarabati basi watupatie fedha za ukarabati, kama mahitaji ni madarasa basi watupatie fedha za madarasa, lakini jambo hili la kusambaza hela kienyeji siyo zuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunategemea usimamizi utaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia nataka niongelee kuhusu ukatili wa kijinsia. Kwanza natumia nafasi hii kuwapa pole wananchi na wakazi wa Mji wa Tunduma ambao kwa namna moja au nyingine wameathiriwa na vitendo vya ubakaji na ulawiti ambavyo watoto wao wamekuwa wakifanyiwa. Vitendo hivi

vimekithiri sana, kiasi kwamba, sisi Wanatunduma, sisi Wanamomba, hatujisikii vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara, Sheria ya Ukatili wa Kijinsia, hususani juu ya ubakaji na ulawiti, ifanyiwe marekebisho ili hawa watu wakose dhamana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema, ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba watu hawa wasipate dhamana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, anapenda kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa, Wizara ya Nishati imeandaa Maonesho ya Wiki ya Nishati kwa mwaka 2024, kuanzia leo tarehe 15 Aprili hadi tarehe 19 Aprili, 2024 katika Viwanja vya Bunge, Jijini Dodoma. Lengo la maonesho hayo ni kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kuona na kuelewa shughuli zinazofanywa na Wizara ya Nishati pamoja na utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijini na shughuli mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara kwa kutekelezwa na Taasisi na Mashirika yake ya *TANESCO, REA, TPDC, EWURA, PURA, PBA* pamoja na kampuni zake tanzu za *GASCO, TANOIL, TGDC, ETDCO* na *TCPM*. Maonesho hayo yatafunguliwa rasmi siku ya tarehe 16 Aprili, 2024 na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa sana kwenye maonesho hayo.

Mheshimiwa Khadija, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata fursa ya kuzungumza, tena kwa ghafla, lakini umenipa fursa hii ya kuzungumza leo ili kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi

Mungu ambaye ametukutanisha tena leo katika bajeti hii ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana ambayo anaifanya, *especially* kwenye eneo la watu wenye ulemavu. Mheshimiwa Rais watu wenye ulemavu tunamshukuru sana, tupo pamoja na yeye, tunampenda sana na tunamtakia kila la heri katika majukumu yake yote ambayo anayafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitachangia katika maeneo kadhaa, lakini eneo ambalo ni muhimu sana kwangu kuchangia kila ninapopata fursa ya kuzungumza na naomba msinichoke, ni juu ya masuala ya watu wenye ulemavu. Mheshimiwa Rais amefanya mambo mengi sana kwa watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na kufungua vyuo na kutengeneza miundombinu mbalimbali katika maeneo mengi. Sasa hivi ukienda katika shule unakuta miundombinu ya watu wenye ulemavu ipo, ukienda kwenye vyuo tayari kuna vyuo vya watu wenye ulemavu, lakini pamoja na hayo yote naomba kutoa ushauri wa kuboresha katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya hivi vyuo ambavyo vinafunguliwa vinakosa vifaa vya kufundishia kwa mfano, kwa wale ambao wanapika keki na vitu kama hivyo. Jambo hili nimelipata nikaona nije kulizungumza ili Serikali iendelee kuweka mkazo katika eneo hilo. Pia, naomba kushauri katika hivi vyuo watu wajifunze namna ya kutengeneza fimbo pamoja na *wheel chairs,* ili waweze kujisaidia wenyewe kwa sababu, inaonekana kuna uhaba wa vifaa hivi saidizi kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi sasa unasikia kuna harambee kwa ajili ya kupata vifaa vya watu wenye ulemavu. Naamini Serikali ya Awamu ya Sita haijashindwa kutengeneza mkakati mzuri ambao unaweza kusaidia kupata vifaa hivi vya watu wenye ulemavu katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kushauri, kama tunapeleka wanafunzi katika hivi vyuo, basi tuwatengenezee

mkakati mzuri ili kujua mwanafunzi akitoka pale anaenda kufanya nini? Akitoka pale atawezeshwa namna gani? Akitoka pale tupate matokeo, ni kiasi gani watu wenye ulemavu wameweza kunufaika na vyuo hivi ambavyo wamepelekwa. *Issue* siyo vyuo, lakini *issue* ni hawa watu waweze kunufaika au kujikwamua kiuchumi wao pamoja na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itengeneze mkakati mzuri ambao utawawezesha watu wenye ulemavu baada ya kutoka kwenye vyuo hivi. Juzi nimemwona Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika mitandao ya kijamii, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, akisema kuwa 10% imerudi. Kama hii 10% imerudi, basi Serikali ije ituambie kwa sababu, kwa watu wenye ulemavu hili ni eneo ambalo wanalitegemea sana kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi katika zile asilimia mbili ambazo zinatolewa na Serikali. Kwa hiyo, tunahitaji Serikali itusaidie kwenye eneo hili, ili watu wenye ulemavu waweze kujikwamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2022 tumefanya sensa ya watu wote ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu. Matokeo yamekuja 11.2% ya watu wote Tanzania Bara wana ulemavu na Tanzania Visiwani watu wenye ulemavu ni 11.4%. Hii ni asilimia kubwa sana, natamani sana kuona Serikali inaweka mkakati kwa ajili ya kuwakwamua watu wenye ulemavu ikizingatia idadi kubwa ya watu wenye ulemavu wanatoka katika familia maskini, nasisitiza wanatoka katika familia maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natamani kuona Serikali ina mkakati gani wa kuondoa shida za watu wenye ulemavu. Watu hawa wapate shida ya maumbile yao, wapate shida ya changamoto zao za kimwili ila wasipate shida za kiuchumi kama ambavyo nchi nyingine ambazo zinafanya vizuri zina mkakati mzuri wa kunyanyua watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, haiwezi kushindwa. Rais wetu anajali wanyonge, anajali watu maskini, anajali watu wenye ulemavu na ameonesha hilo kwa sababu, ameweza kuwaita watu wenye ulemavu Ikulu na

kuzungumza nao, ameweza kutenga fedha kwa ajili ya mafuta, lakini pia ameweza kutenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuwezesha shughuli za watu wenye ulemavu katika Wizara ya Fedha. Mwaka jana tulipata hiyo bajeti na natumaini mwaka huu pia, tutaongezewa hiyo bajeti kwa sababu, shida za watu wenye ulemavu ni nyingi mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi kati niliangalia hizi takwimu na nilitamani sana kupata uelewa zaidi wa hizi takwimu *especially* kwa sisi watu wenye ulemavu, lakini ikipendeza Bunge zima lipate kujua hizi takwimu. Ni maeneo gani yenye watu wenye ulemavu na ni kiasi gani, au kuna aina gani ya watu wenye ulemavu na wingi wao katika maeneo yao tofauti tofauti kusudi Wabunge wanapokuja hapa kusaidia nchi yao na wananchi wao, watambue katika majimbo yao wana idadi kiasi gani ya watu wenye ulemavu na ni wa aina gani ili ifike mahali nipate kusikia hapa kila Mbunge akizungumzia masuala ya watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kusema masuala ya watu wenye ulemavu, pia naomba nichangie eneo la masuala ya dawa za kulevya kwa sababu hata watu wenye ulemavu wanaguswa na masuala ya madawa ya kulevya. Naomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Sita ya Mama Samia Suluhu Hassan. Imeweza kufanya kazi kubwa sana pamoja na Kamishna Mkuu wa Madawa ya Kulevya. Serikali tuendelee kumlinda yule baba ili aweze kufanya kazi nzuri ya kukomboa vijana wetu na watoto wetu kwa sababu Mama ameonesha nia ya dhati na thabiti ya kuhakikisha anasaidia vijana wake wasiingie au wasijihusishe sana na matumizi ya madawa ya kulevya au wasipate ule uwanja mpana sana wa matumizi ya madawa ya kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi kikubwa sana kimekamatwa mwaka jana Desemba, kiasi cha 3,182, kiasi kikubwa ambacho kwa historia hakijawahi kukamatwa au basi kama kimewahi kukamatwa, hatujawahi kutangaziwa kwamba kiasi kikubwa kama hiki kimeweza kukamatwa. Kwa hiyo, naomba niishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita ya Mama Samia Suluhu Hassan

kwa sababu tunaona kabisa nia yake ya dhati ya kuhakikisha vijana, wanawake, watoto pamoja na watu wenye ulemavu wanajiepusha na matumizi ya dawa za kulevya ambazo zinaharibu akili zetu, utendaji kazi wetu na inaondoa nguvu kazi. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuzingatia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, naomba nichangie na kusisitiza pia kwenye eneo la vifaa saidizi pamoja na ofisi za watu wenye ulemavu. Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kongamano langu la uzinduzi wa *NGO* yangu alitoa kauli akisema, kila halmashauri itenge chumba maalum kwa ajili ya SHIVYAWATA, wapate ofisi ili watu wenye ulemavu wajue eneo la kufika la kueleza shida zao kwa urahisi na kila halmashauri ipate kujua shida za watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningetamani sana kujua hili suala limefikia wapi kwa sababu namna ninavyosikia, bado kuna maeneo ambayo hawajatekeleza neno hili. Labda sasa tutafute namna ya kutengeneza kama sheria ili kila halmashauri kuwe na ofisi ambazo hazitakuwa zinachangiwa kiasi chochote cha pesa na wenye ulemavu waweze kupata huduma kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Serikali itengeneze mkakati mzuri wa kupata vifaa saidizi kama nilivyosema hapo awali. Ningetamani sana halmashauri ingetenga pesa ukiachana na hii asilimia mbili ambayo ni kwa ajili ya masuala ya uchumi, lakini nyingine kwa ajili ya kumwezesha mtu mwenye ulemavu. Sasa *wheel chairs* zimekuwa bei ghali, tunatamani sana kupata vifaa hivi kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Tupate mafuta kwenye halmashauri zetu ili wafikiwe kwa urahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo, naomba nikushukuru sana, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayofanya. Tuendelee kumtia moyo, tuzingatie uwezo wake, tufahamu na tuendelee kumsemea Mheshimiwa Rais wetu kwa sababu tunawiwa kufanya hivyo, kwa sababu tunawakilisha wananchi wale ambao wana shukurani kwa miradi ambayo imepelekwa kule chini, katika kila kata kuna miradi. Kwa hiyo,

tumshukuru sana Mheshimiwa Rais na tuendelee kumsemea mazuri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** ... na mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa nilimwita Mheshimiwa Dkt. Mollel lakini kulikuwa na mchangiaji Mheshimiwa Mohamed ambaye alikuwa na udhuru, sasa amerudi. Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Mohamed Said Issa. Nakupa dakika tano halafu atafuata Mheshimiwa Dkt. Mollel. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali hiki cha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitamalizia mchango wangu kwa mambo machache tu. Jambo la kwanza ni suala la Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi. Tulipitisha Sheria hapa, Sura namba 343 na 292 ambayo inahusiana na uchaguzi wa Wabunge, Madiwani na Uchaguzi wa Mheshimiwa Rais. Kwa kweli jambo hili lilikuwa ni jambo jema sana. Sasa basi, naomba, vyombo vinavyohusika tufanye utekelezaji wa jambo hili. Ni jambo la kufurahisha na la kupendeza, Mheshimiwa Rais ameshasaini sheria hii. Sasa, kwa sasa hivi chaguzi zinazokuja tuendelee na hii sheria kwa sababu juzi tumefanya chaguzi ndogo katika Kata 22, yaliyotokea ni yale yale ambayo yalinung'unikiwa kwenye chaguzi zilizopita kama ya 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni wakati wa kuwaondoshea wananchi kero zile ambazo walikuwa wanahitaji ziondolewe. Kwa hiyo, napendekeza tuendelee katika uchaguzi utakaokuja wa Serikali za Mitaa na hii Tume Huru iundwe kabisa isiwe tu

tumepitisha jina. Iundwe kabisa, iendelee kufanya kazi ili tuweze kuwapatia wananchi haki waliyokuwa wanaitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, tumepitisha Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, sasa basi kule Zanzibar, Tume Huru hii ya Taifa ya Uchaguzi ilikuwa inawakilishwa na Tume ya Taifa ya Zanzibar *(ZEC)*. Kwa hiyo sasa kule hakuna Tume Huru ya Zanzibar. Sasa iwe ni marufuku kutumia wakala yule kwa sababu wale siyo huru, tunataka huru. Kama ikiwa hapa ni huru, Tanzania ni huru basi na Zanzibar iwe huru. Kwa vile haijawa huru basi uchaguzi unaokuja, *ZEC* isiwe ni wakala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia mchango wangu, naomba niguse suala la Bwawa la Mwalimu Nyerere...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Uchaguzi unaofanyika upande wa pili wa Muungano ili kuthibitisha uhuru wake ni pamoja na yeye kuwepo ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, sioni sawa kama Mheshimiwa Mbunge anatoa tuhuma kwamba uchaguzi uliofanyika kule siyo huru na Tume kule siyo huru. Misingi ya sheria iliyobadilishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inahusu Tume ya Uchaguzi ya Tanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, taarifa hiyo.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yake siipokei...

**NAIBU SPIKA:** Ukiendelea sana utakuwa unajitoa kwenye Kiapo cha Bunge hili...

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sipokei taarifa na ndiyo maana tulibadilisha sheria ya kuwa Tume Huru ya Uchaguzi. Kama na yeye anakataa siyo Tume Huru ya Uchaguzi, tungebakia kule kule kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kwa maana hiyo, kule Zanzibar wakitaka iwe Tume huru na wao wabadilishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea na mchango wangu. Jambo la pili ni suala la Bwawa la Mwalimu Nyerere. Wananchi wa...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa, dakika tano zako zimekwisha.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, aaaahhha, haijafika. *(Vicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa *Sheikh*...

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haijafika mbona nimeangalia.

**NAIBU SPIKA:** Sasa una...

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi nimalizie mchango wangu kidogo dakika moja...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed, mimi nakwenda kwa mujibu wa kanuni. Dakika tano zako ulizoziomba zimekwisha.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie mchango wangu dakika moja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed, kaa chini tafadhali. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa hotuba nzuri kutoka katika ofisi yake. Pia niwapongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa Jenista Mhagama; Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi; pamoja na Manaibu wao Mheshimiwa Ummy Nderiananga na Mheshimiwa Patrobass Katambi kwa kazi kubwa wanazofanya kulijenga Taifa letu. Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake wanafanya kazi kubwa kwenye majukumu yao ya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita kwenye tatizo la ulevi kwa vijana na mchezo wa kamari katika sehemu nyingi hapa nchini Tanzania na hususan Mkoani Kilimanjaro. Vijana ni nguzo ya Taifa katika nyanja za uchumi, michezo, maadili na uongozi na wakiachwa kujitumbukiza katika ulevi na utumiaji wa dawa za kulevya kama ilivyo sasa hivi tutalifanya Taifa letu kuangamia siku za mbeleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ulevi kwa vijana na kuongezeka kwa mchezo wa kamari Mkoani Kilimanjaro katika maeneo ya vijijini limekuwa kubwa na linaua kabisa uwezo wa kundi hili kuchangia kuijenga nchi yetu kupitia nguvu kazi yao kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukosefu wa ajira rasmi Serikalini kwa vijana wetu, sehemu kubwa ya vijana wamejiingiza katika ulevi wa pombe kali zilizotapakaa mitaani na kuvuta bangi na kutumia dawa za kulevya za aina mbalimbali. Kudhihirisha tatizo hili, akiongea katika hafla ya kuzindua Mbio za Mwenge tarehe 2 Aprili, 2024 katika Viwanja vya Chuo cha Ushirika Moshi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa alisema: "Siku za

hivi karibuni imeibuka aina mpya ya bangi inayotumiwa na vijana wetu yenye kiasi kikubwa cha kilevi inayofahamika kama 'cha Arusha' na 'Skanka'." Alieleza kuwa aina hii ya bangi yenye sumu nyingi huchanganywa kwenye sigara na wanaoitumia hubadilika na kuwa kichaa na kupoteza mwelekeo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Mkoani Kilimanjaro, viongozi wa dini mbalimbali wamelalamikia tabia ya vijana wengi wa kiume vijijini kubugia pombe kali, dawa za kulevya na bangi kitu ambacho kimesababisha athari mbalimbali. Vilevile, vijana wengi hushiriki kwenye kucheza kamari. Matokeo ya kamari hizi ni kwamba hela zote huishia kwenye kamari. Mabonanza ya Wachina yako hadi huko vijijini, mabonanza haya yamefilisi vijana wetu huko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla pombe kwa vijana wetu hawa ni sumu. Hatari zake hujumuisha vijana wetu kukosa nguvu za kiume na kushindwa kushiriki tendo la ndoa na kushindwa kuzaa watoto. Kasoro hii imelalamikiwa na viongozi wa dini na wale wa Serikali kwenye Mkoa wetu wa Kilimanjaro katika maeneo ya Rombo, Vunjo na Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari nyingine kubwa za pombe, dawa za kulevya na bangi ni ajali mbaya zinazosababishwa na ulevi, magonjwa ya ini, UKIMWI na aina nyingine nyingi za saratani. Pombe, bangi na dawa za kulevya husababisha umaskini na vinapelekea vifo vya haraka kwani vijana waathirika, kuwa maskini na huishi katika mazingira magumu na mara nyingi hushindwa kumudu matibabu. Vilevile, vilevi huwa ni chanzo cha magomvi yasiyo na msingi, ajali za uzembe, kujeruhiwa na kuuawa na vibaka na msongo wa mawazo. Tabia hii ya vijana wetu kujiingiza katika vilevi ni ya kusikitisha kwani nchi isipokabiliana nalo kwa nguvu zote, sote tutaathirika kwa namna mbalimbali ikiwemo usalama wa Taifa na familia zetu na mali tulizonazo huku nyumbani na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hii, zinahitajika jitihada za pamoja kati ya wazazi, viongozi wa mila, jamii,

vitongoji, vijiji, kata, wilaya mkoa na madhehebu ya dini na Serikali kwa ujumla katika kulishughulikia na kulimaliza tatizo hili la ulevi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu la wazazi kuhakikisha kwamba katika umri wa kijana kuna mambo ya msingi yanayopaswa kuangaliwa kwa umakini na kwa ungalifu mkubwa. Vijana wafundishwe na kutayarishwa namna ya kuishi katika jamii, namna ya kupambana na umaskini kwa kufanya kazi na mfano mzuri wa malezi ya vijana uko kwenye jamii ya Kimasai. Mpaka sasa vijana wa kabila hili ni mfano wa kuigwa kwani wamedumisha mila zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla tatizo la ulevi kwa vijana wetu vijijini (Mkoani Kilimanjaro na maeneo mengine nchini) ni kubwa sana na jambo hili ni letu sote. Ni vyema tukaweka nguvu pamoja ili kuitokomeza shida hii na kunusuru maisha yao kwani linatishia nguvu kazi ya Taifa letu ambayo inatokana na kundi la vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kupitia Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, iwasaidie vijana wa Kitanzania wawe na programu za kuweka vipaumbele katika mambo makuu matatu katika maisha yao ya kila siku ambayo ni utaifa, uchumi na kushiriki katika fani mbalimbali za kujipatia kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie mchango wangu kwa kusema kwamba Tanzania yetu ya leo na kesho inawategemea sana vijana. Hivyo basi ni vyema nchi yetu ikawekeza nguvu kubwa katika malezi ya vijana kwa kuhakikisha kuwa wanaachana kabisa na ulevi wa aina yoyote ile kwa sababu vijana ni tunu, hazina na thamani katika Taifa letu. Ni vyema jambo hili likasaidiwa na michakato ya kisheria katika ngazi za vijiji, kata, wilaya na Taifa. Uwepo wa sheria kali katika maeneo hayo kutasaidia sana kukabiliana na ulevi uliokithiri kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ya bajeti iliyojaa mambo muhimu ambayo yanaleta matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali kwa kutoa takribani shilingi bilioni 12 kulipa fidia kwa watu binafsi na taasisi zinazozunguka maeneo ya Bunge, wazo hili ni muhimu sana kwani linaenda kupunguza kero kwa Waheshimiwa Wabunge ya kukosa ofisi za kutendea kazi. Aidha, utwaaji huu wa maeneo utasaidia vyombo vyao vya usalama kuwa mahali salama. Ili zoezi liwe na tija nashauri zile taasisi za Serikali ambazo bado hazijaondoka zitafutiwe maeneo mbadala haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri ni vema kwa Serikali kutafuta eneo kubwa zaidi nje au mbali tukiamini idadi ya Watanzania inaongezeka na Waheshimiwa Wabunge watakuja kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali za ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na wananchi wa Jimbo langu la Mbulu Mjini kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ya kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi mwaka 2023/2024, hususan katika Jimbo langu la Mbulu Mjini. Tumepata fedha nyingi sana haijapata kutokea, hali iliyotuwezesha kutekeleza miradi iliyokwama kwa muda mrefu toka mwaka 1984. Mifano yake ni ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji Endayaya Tlawi na ujenzi wa Daraja la Gunyoda na barabara unganishi katika wilaya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi na wananchi wa Mbulu Mjini kwa pamoja tunamwombea Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu

Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kheri na baraka tele kwa Mwenyezi Mungu na tunamuahidi ushindi wa kishindo katika Uchaguzi Mkuu mwaka 2025, kwa kuwa matokeo ya utendaji wake na Serikali katika utatuzi wa kero na changamoto zilizowakabili wananchi wetu kwa muda mrefu tunayaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kuishauri Serikali kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na mapendekezo na maoni ya Kamati zetu zote nne:-

(i) Tunaiomba Serikali iangalie upya utaratibu wa kuboresha maslahi ya wastaafu nchini kwani kwa sasa kiwango kinacholipwa kwa wastaafu kila mwezi ni kidogo sana kulingana na hali halisi ya maisha kiuchumi;

(ii) Tunaiomba Serikali ijitahidi sana kutoa fedha za bajeti ya maendeleo tunazopitisha kila mwaka kwa kila Wizara kwani kitendo cha fedha nyingi kutopelekwa kwenye malengo yaliyokusudiwa kinakwamisha maendeleo ya nchi kwa ujumla;

(iii) Tunaiomba Serikali iangalie upya utaratibu wa kusimamia uendeshaji wa mashirika yanayojiendesha kwa hasara ili kuleta ufanisi zaidi kupata gawio kama ilivyotarajiwa; na

(iv) Tunaiomba Serikali iangalie utaratibu wa kuanza kujadili upya suala la kikokotoo cha pensheni ya wastaafu. Kwa kweli kila unapofanya mikutano ya hadhara na mikutano ya watumishi popote pale wamelalamikia jambo hili. Hivyo basi kuna haja ya Serikali kukaa meza moja na vyama vya wafanyakazi ili kupata maridhiano ya pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ludewa lina wananchi wenye moyo wa kujitolea sana kwenye maendeleo hivyo wanaiomba sana Serikali iwaunge mkono katika kumalizia maboma ya vituo vya afya. Kata zilizojenga na kuezeka jengo la utawala ni Lugarawa, Ludewa, Luana, Madilu, Lupanga, Ludende, Madope, Lumbila, Mkongobaki, Lupingu, Kilondo na Masasi. Naomba sana Serikali isiwavunje moyo wananchi hawa kwa kuja na mpango wa kuvimalizia japo kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa kutoa shilingi bilioni 2.6 kwa ajili ya Barabara za Tarafa ya Mwambao kwani Kata nne za Kilondo, Lumbila, Makonde na Lifuma hazikuwahi kuunganishwa kwa barabara, naomba fedha ziongezwe kwenye Barabara za Ludewa - Nsisi; Mbwila - Lifuma; Lumbila - Kijyombo; Mawengi – Kitewele – Kimata - Makonde; na Madunda – Liunji – Ifungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoa fedha nyingi kwenye Barabara ya Itoni – Ludewa - Manda pamoja na shukrani nyingi, tunaomba *Lot III* inayoanzia Mawengi hadi Makao Makuu ya Wilaya ya Ludewa imaliziwe kujengwa kwa kiwango cha zege ikiwezekana hadi Nkomang'ombe ili kuweza kusafirisha makaa ya mawe mengi na kuongeza mapato ya nchi na wananchi.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza miaka mitatu kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii. Pia, naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya Ushindani wa Kimataifa *(National Competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni: "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi chake akiwa Waziri Mkuu, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimazi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu. Katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2023 ukuaji wa uchumi wa Taifa ulikuwa asilimia 5.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kutokana na mwendelezo huo mzuri wa kiuchumi, kampuni ya Moody's imechapisha matokeo Machi, 2024 ambapo Tanzania imepanda kutoka daraja la chini la *B2 (with Positive Outlook)* na kwenda ngazi ya juu ya *B1 (with Stable Outlook)*. Matokeo hayo ni ya juu kabisa katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki na hivyo hatuna budi kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake mahiri uliowezesha Taifa kupata mafanikio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kukua hadhi kimataifa, bado kuna kigugumizi kwa baadhi ya taasisi za kifedha nchini kuelekeza mikopo kwenye sekta muhimu za kiuchumi ikiwemo kilimo. Serikali kupitia Benki Kuu *(BoT),* ilitenga shilingi trilioni moja kuwezesha benki kutumia dirisha hili kukopesha sekta ya kilimo kwa riba isiozidi 10%. Kwa muda mrefu sasa hilo dirisha halijaonesha mafanikio ya kuchochea benki kupunguza riba kwenye mikopo ya kilimo na hata taasisi za Serikali zinazonunua mazao ya kilimo bado zinahangaikia kupata hiyo fursa na badala

yake kulazimika kukopa kwa riba za juu. Kilimo kama ilivyo kwa madini na utalii, zinaliingizia Taifa asilimia kubwa ya fedha za kigeni, Serikali iweke mkakati wa kuvutia uwekezaji ikiwemo mikopo ya benki ili kuongeza tija na ushindani katika masoko ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2023 mpaka Machi, 2024 Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kimkakati kwa mafanikio mkubwa sana na utekelezaji huu unaonekana mpaka kwenye ngazi ya halmashauri zetu. Mafanikio makubwa yamejikita kwenye uboreshaji wa miundombinu ya barabara, reli, bandari, mtandao wa mawasiliano na uboreshaji wa usafiri wa anga. Napongeza Serikali kwa hatua nzuri za utekelezaji wa mradi wa kihistoria wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* na ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (megawati 2,115). Miradi hii miwili ya *SGR* na umeme ni nguzo imara ya kiushindani katika uchumi wetu na Nchi za Maziwa Makuu na hata za Kusini mwa Afrika na Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatakiwa kuendelea kuchukua hatua za kibajeti kukabiliana hasa na mfumuko wa bei na kuporomoka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani na sarafu kuu zingine. Kwa kuzingatia kuyumba kwa uchumi wa dunia, bajeti hii ijielekeze kuchukua hatua za kuchochea uzalishaji wa ndani ili kupunguza nakisi ya urari wa biashara *(Balance of Payment – BOP),* kuimarisha pato la Taifa kupitia sekta za kilimo, madini, utalii na uchukuzi. Hatua hizi ziende sambamba na kuimarisha mazingira ya uwekezaji hasa kwenye sekta ya kilimo na madini. Pia, Serikali iendelee kusimamia sera ya fedha na bajeti ikiwemo kuimarisha mifumo na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utekelezaji wa miradi ya kimkakati, kunapelekea mahitaji makubwa ya fedha za kigeni na hivyo msukumo uwepo kwenye kuongeza uzalishaji wa madini na mazao ya kilimo. Hatua hizi ni muhimu kuhakikisha utulivu wa thamani ya shilingi na pia kuimarisha uhimilivu wa deni la Taifa hasa kwenye kigezo za ulipaji wa deni la nje kwa kulinganisha na uuzaji wa bidhaa nje (mapato ya fedha za kigeni).

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto za tabianchi, bado kuna fursa kubwa kwa Tanzania kwenye uzalishaji wa ziada wa nafaka ukilinganisha na nchi za ukanda huu. Serikali iimarishe upatikanaji wa pembejeo bora kwa bei nafuu na kuimarisha upatikanaji wa masoko ya uhakika kupitia *NFRA* na Soko la Bidhaa *(TMX)*. Kutokana na ruzuku kwenye mbolea na jitihada walizofanya Wizara ya Kilimo kuwapatia vitendea kazi Maafisa Ugani, ichochee kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo kutoka uzalishaji wa sasa wa kilo 1,000 za mahindi kwa eka mpaka kilo 4,000 kwa eka ya mahindi. Tanzania ina fursa kubwa ya biashara ya hewa ukaa *(carbon credit)* ikiwa ni pamoja na kuwa chanzo cha uhakika wa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na msukumo kwenye kilimo, madini na utalii, Serikali inatakiwa kuwekeza hasa kwenye miundombinu ya usafirishaji ikiwemo barabara, reli, bandari na usafiri wa anga hasa kwa mizigo. Kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha zimesababisha uharibifu mkubwa kwenye miundombinu ya barabara na hata reli. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, barabara zinazohudumiwa na *TARURA* kwa asilimia zaidi ya 80 zipo kwenye hali mbaya sana kutokana na mvua kubwa na pia kwa kukosa matengenezo ya mara kwa mara. Maeneo mengi ya vijijini barabara hazipitiki kutokana na ufinyu wa bajeti ukilinganisha na mtandao wa barabara zinazohudumiwa na *TARURA*. Naomba Serikali ichukue hatua za haraka kunusuru hali hii ili wananchi waweze angalau kusafirisha mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuidhisha ujenzi wa barabara ya njia nne kuanzia Nsalaga (Uyole) mpaka Ifisi jirani na Uwanja wa Ndege wa Songwe. Kipande hiki cha barabara ambacho ni sehemu ya barabara kuu ya TANZAM, ni muhimu sana kwa kuinua uchumi wa Tanzania na hata kupunguza ajali za mara kwa mara zinazotokea katika mteremko wa Mlima Iwambi kuelekea Mji wa Mbalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa usafirishaji wa mazao yetu kwa soko la ndani na nje ikiwemo fursa za biashara ukanda wa *SADC* na uzalishaji mkubwa kwa Mikoa ya

Nyanda za Juu Kusini, napendekeza mwendelezo wa uboreshaji wa Barabara za TANZAM kipande cha Igawa - Tunduma; Barabara ya *bypass* ya Uyole - Songwe; Barabara ya Mbalizi – Shigamba – Isongole kutokana na uzalishaji wa mazao ya kilimo; Barabara ya Mbalizi – Galula – Makongosi kutokana na uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo na madini; na pia Barabara ya Isyonje – Kikondo – Makete.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya kazi kubwa kuhakikisha ujenzi wa *SGR* unaendelea kwa kasi ile ile na pia napongeza jitihada za kuendelea kutafuta vyanzo vya fedha vya masharti nafuu kugharamia ujenzi huo. Pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa, Serikali imefanya maboresho makubwa ya miundombinu na huduma katika bandari zetu hususani Bandari ya Dar es Salaam ili kukabiliana na ushindani mkubwa wa bandari zingine za ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika. Bandari ya Dar es Salaam inakumbana na ushindani mkubwa toka Bandari za Mombasa (Kenya), Beira (Msumbiji), Nacala (Msumbiji), Durban (Afrika Kusini), Lobito (Angola) na *Walvis Bay* (Namibia).

Mheshimiwa Naibu Spika, maboresho ya bandari zetu iendane na kuondoa changamoto zingine ambazo zinasababisha gharama kubwa za usafirishaji kwa bandari zetu na kusababisha kupoteza biashara ya usafirishaji kwa bandari shindani. Ufanisi wa bandari unategemea pia maboresho ya barabara, Reli ya Kati *(TRL)*, Reli ya *TAZARA*, utendaji wenye tija wa wadau wote wa bandari na hata watumishi ili kupunguza gharama za usafirishaji kwa wateja wa bandari zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa zilizopo zaidi ya 70% ya mzigo wote wa nchi za nje unasafirishwa kwa kupitia *Dar es Salaam Corridor* inayohudumia Nchi za DR Congo, Zambia na Malawi. Pamoja na fursa za kijografia ya bandari zetu, mzigo unaopita sasa kwenye Bandari ya Dar es Salaam, ni 50% tu ya biashara yote ambayo kwa sasa inashikiliwa na bandari shindani. Kwa ajili ya kunusuru biashara hii inayopotea kwa bandari shindani, Serikali ichukue hatua za haraka kuboresha huduma za *TAZARA* ikiwa ni pamoja ya maboresho ya miundombinu ya reli, ununuzi wa vichwa vya reli, mabehewa na vitendea kazi vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali kwa haraka ishughulikie maboresho ya Mkataba wa *TAZARA* na kisha kutafuta mbia mwenye uwezo wa kifedha na uendeshaji. Katika kipindi hiki cha ushindani mkubwa usafirishaji wa reli ni mojawapo ya suluhisho kubwa kupunguza mzigo wa bei kubwa kwa wateja wa bandari zetu na hata wananchi. Pamoja na maboresho ya reli ya *TAZARA*, napendekeza kuendelea na ujenzi wa bandari kavu Mbeya ambayo ina fursa kubwa katika kipindi hiki katika kuwezesha kupunguza gharama za usafirishaji kwa wateja wa bandari na hata kupunguza bei za mafuta ya petroli, pembejeo na mazao ya kilimo. Bandari kavu ya Mbeya ni njia panda kwa wateja wa Nchi za Malawi, Zambia, DRC Lubumbashi na hata kwa Zimbabwe na Msumbiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lengo la kuvutia wawekezaji na kuongeza pato la fedha za kigeni, napendekeza Serikali kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa madini ya kimkakati kidunia, ikiwemo na gesi ya *Helium* na madini ya *Niobium*. Serikali iweke msukumo kuanza kwa uzalishaji wa gesi ya *Helium* na uzalishaji wa madini ya *Niobium* ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kiwanda cha *Ferroniobium (FeNb)* ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja na reli ya *SGR*, kuna mahitaji makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa kimataifa. Kwa kutumia Sheria zetu za Uwekezaji, Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani ili yaongezwe thamani hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi zingine ili yachakatwe hapa kwetu. Tanzania imebahatika kuwa na madini ya *Niobium* ambayo inapatikana milima ya *Panda Hill,* Songwe Wilaya ya Mbeya na mahitaji ya *Ferroniobium (FeNb end product)* ni makubwa duniani na hapa kwetu pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia rasilimali zetu za madini, Serikali inaweza kutengeneza fursa nyingi na kupitia Mradi wa *Niobium* na Kiwanda cha *Ferroniobium*, ajira 2,000 zitakazozalishwa wakati wa ujenzi na pia kutakuwepo ajira za

kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs* 7,000. Mradi utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 *(USD 220 million)* ambapo mapato kwa Serikali kila mwaka shilingi bilioni 50 *(USD 22 million),* uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kisasa cha kwanza Afrika (*modern manufacturing plant and smelter)*. Pamoja na kuingiza teknolojia hii adimu na *ujuzi (skills transfer)* pia itakuwa inachangia huduma za kijamii *(Corporate Social Investment in Community)* na chanzo cha fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza nyote, Ofisi ya Waziri Mkuu, Waziri Mkuu mwenyewe, Mawaziri wote wanaomsaidia Mama Jenista Mhagama, Kaka Ndejembi, Dada Ummy na Kaka Katambi pamoja na wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu ikiwa ni pamoja na Makatibu Wakuu wote wawili, Wakurugenzi, Maafisa na watumishi wote; ikiwa ni pamoja na *Private Office* ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Baada ya pongezi, naomba kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na kazi na ajira, ushauri wangu hususani kuhusu kukuza na kulinda ajira chache hasa katika sekta binafsi, nashauri taratibu za vibali vya kazi ziweze kuzingatiwa. Kwa ilivyo sasa kuna wimbi kubwa la raia kutoka China ambao wamegeuka wachuuzi, siyo Kariakoo tu, bali hata katika miji midogo kama Mafinga, Makambako na kadhalika. Suala hili tusipokuwa makini iko siku litazua tafrani kati ya jamii ya Wachina na Watanzania wazawa japo ni neno lisilopendwa kusikika, kuna kitu kitatokea siyo tu katika nyanja ya uchumi lakini hata kijamii na kidplomasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilivyo sasa kunajengeka chuki siyo dhidi ya jamii ya Wachina bali wananchi dhidi ya Serikali, wanasema kuwa Serikali kwa nini inaachia Wachina kushindana na Watanzania kwenye ajira za chini ambazo kimsingi zinapaswa kufanywa na wazawa. Ushauri wangu, tukiliacha jambo hili bila kulidhibiti iko siku litaleta mgongano ambao

utatuingiza katika shida ya kimahusiano ya kidplomasia na marafiki zetu wa muda mrefu China.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *BBT;* programu hii ambayo inasimamiwa na Wizara ya Kilimo inaweza kuwa msaada mkubwa katika kuongeza ajira kwa vijana. Napongeza hatua zote za awali ambazo zimeanza kuchukuliwa, ushauri wangu, washirikiane na Kilimo na JKT katika kuhakikisha kuwa vijana wanaojitolea JKT wanakuwa sehemu ya wanufaika wa *BBT*. Naamini watakuwa na mchango mkubwa sana si kwao binafsi tu, lakini na kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuimarisha Idara ya Tathmini na Ufuatiliaji wa Shughuli za Serikali; kwanza napongeza uamuzi wa Serikali katika kuanzishwa kwa Idara hii muhimu ambayo itasaidia sana hata katika kupunguza hoja za *CAG*, lakini zaidi katika kuimarisha utendaji Serikalini hususani katika kukamilika miradi kwa wakati. Hata hivyo ili kuwa na matokeo chanya na kutimia kwa malengo ya kuanzishwa kwa Idara hii muhimu, rasilimali fedha na rasilimali watu ni muhimu sana. Katika kipindi kifupi toka kuanzishwa kwa Idara hii imethibitika kuongezeka kwa umakini wa kiutendaji ndani ya Serikali kwa sababu Idara imekuwa kama *watch dog* ndani ya Mawizara na Taasisi zetu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na manufaa haya na kwa faida ya kuokoa gharama kama vile miradi kuchelewa kukamilika ambapo mara kadhaa Serikali imelazimika kuongeza fedha kwa miradi ambayo ilichelewa kukamilika kutokana na kushindwa kufuatilia utendaji wakati miradi inaendelea. Kwa hiyo kuimarisha Idara hii ni sawa na ile tunasema *prevention is better than cure* kwa maana kwamba kupitia Idara ya Tathmini na Ufuatiliaji tunaweza kuzuia kabla madhara makubwa hayajatokea, ushauri wangu Idara hii itazamwe kwa macho mawili kwa maana ya *financing* na *human resources.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *EPC+F;* Serikali ilisaini mikataba kadhaa na wakandarasi wa kujenga barabara kwa kiwango cha lami kwa Mfumo wa *EPC+F*. Mikataba hii ilisainiwa Juni, 2023 na ni zaidi ya kilometa 2,000, mpaka sasa bado

hatujaanza hata kilometa moja. Tatizo tunaambiwa wakandarasi wanaomba kulipwa angalau *advance payment* ya 10%.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu Serikali ifanye kila linalowezekana ili walau wakandarasi walipwe hii 10% kwa kuwa pamoja na sababu za kiuchumi suala hili kisiasa linaweza kuwa na shida kutokana na ukweli kwamba kama Serikali tulilitangaza sana na kuwapa matumaini wananchi, hivyo kutokuanza kwa miradi italeta ugumu katika chaguzi zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba upelekaji wa umeme kwenye maeneo ya mijini yenye sura za vijiji, lifanyiwe kazi maeneo hayo yapate umeme. Mfano maeneo ya Mitaa ya Ugele, Msisina, Mtalagala, Mosi, Ulonge, Machinjio ya Nguruwe ndani ya Manispaa ya Iringa. Umeme upelekwe kwa gharama za upelekaji wa umeme vijijini, kwa kuwa mazingira yao ni sawa na vijiji tu, ingawa vinatambulika viko mjini.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza uchangiaji sasa tunaingia kwa Mawaziri, tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kutupa nafasi ya kuchangia. Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wamechangia sana kwenye Eneo la Wizara ya Afya. Wamechangia Waheshimiwa Wabunge nane na sasa hivi amechangia pia dada yangu Keisha amekuwa wa tisa na mambo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasema kwa asilimia kubwa ni masuala ya sisi kwenda kuyafanyia kazi na wala hayatakuwa na sababu ya sisi kupitia moja baada ya lingine. Tutakwenda kuyafanyia kazi na ninyi mtaona matokeo kule ambako mnafanya shughuli zenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme machache. Moja ambalo dada yangu Keisha amelizungumzia sasa hivi lakini pia lile alilozungumzia Mheshimiwa Ester Bulaya, la waraibu kwa maana wenzetu ambao wanatumia madawa ya kulevya. Kwanza

niwaambie Waheshimiwa Wabunge, kwa mwaka jana hospitali zetu zote nchini zimetibu waraibu 61,605 na wote wamekuwa wakipata huduma. Kwa kweli tuishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu imekuwa ikitusaidia na ikitupa maelekezo, lakini tumshukuru Kaka yetu Kamishna Lyimo, anafanya kazi kubwa sana kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie tu kwenye eneo la waraibu kwa Muhimbili hili niseme tu ni kazi kubwa ya Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambayo anaifanya na kuboresha kila kitu na ametoa maelekezo. Kwenye eneo la Muhimbili pekee yake kwenye *database* wako waraibu 5,000 na katika hao waraibu, Hospitali yetu ya Muhimbili haijaishia kwenye kuwatibu tu, wale ambao wamekuwa *cleared*, wanaajiriwa pale Muhimbili. Kwa hiyo, unakuta sasa hivi tunao zaidi ya 50 ambao wameajiriwa pale wanafanya shughuli mbalimbali za kusukuma wagonjwa, wengine wanafagia na wanalipwa mshahara wakiwa pale. Kwa sababu hao wengine wanaweza wakapona lakini wanapopona wakirudi mtaani wanapokuta maisha ni magumu wanaendelea kuwa waraibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunataka kuanzisha *to roll out* kwenye hospitali zetu zote, kwamba kila mahali tutengeneze *incentive* ambayo wale ambao wamekuwa *cleared* na hawatumii tena madawa ya kulevya wanatengenezewa shughuli za kufanya ndani ya hospitali zetu. Nafiriki kwa kushirikiana na Wizara mbalimbali tunaweza tukafanya vizuri zaidi. Kwa mfano, kaka yangu Mheshimiwa Bashe hapa ameanzisha *BBT*, wale wafanyakazi waliokuwa *cleared* kwenye eneo la vibarua wakaingia pale *(BBT)* na wakafanya kazi, tunaweza tukafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Muhimbili tunaona zaidi ya 1,000 kwa siku, lakini Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu ametoa maelekezo na tayari ametutafutia wadau pamoja na mbia, ametupa eka 160 kule Vingunguti. Sasa pale kinajengwa kiwanda ambacho kitatengeneza vifaa tiba lakini kita-*assemble* hizi bajaji. Mle tunategemea waraibu 500 waweze kuwa *absolved* na kufanya kazi hiyo ndani ya hilo eneo na *donor* tayari, *visibility*

imeshamalizika sasa ni ujenzi unaanza. Kwa hiyo itakuwa kazi vifaa vya hospitali vinazalishwa, kiwanda kinaendelea, vifaa tiba vinazalishwa lakini hawa wenzetu ambao tunawatibu pale Muhimbili na wanakuwa *absolved* pale kwa kushirikiana na kaka yangu Lyimo, tuone namna ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu wametoa michango mizuri sana sisi tunakwenda kutekeleza lakini niwaombe Waheshimiwa Wabunge, Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya kazi kubwa sana kwenye eneo letu la afya na kwenye majimbo ya Wabunge yamefanyika mambo makubwa sana. Imefanyika *revolution* kubwa sana ya teknolojia kule kwenye majimbo yao. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wasisahaulishwe wakati huu na matatizo madogo madogo yaliyoko huko wilayani wakaacha ku-*focus* kwenye makubwa ambayo tayari yamefanyika na Mheshimiwa Rais wetu amefanya na tukaacha kuwafanya watu wa-*focus* kwenye yale mambo makubwa, tukaanza ku-*focus* kwenye madogo madogo yanayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwa teknolojia aliyoipeleka Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kule chini kwenye wilaya zao, zahanati na kwenye mikoa yao, leo utaona kwamba tulikuwa tukitembea na Kamati zetu kwenye mikoa yetu; tuki-*compare* na Kamati za Wabunge kwenye mikoa yetu, tukienda *Ocean Road* tunakuta asilimia zaidi ya 90 mpaka 100 ni wagonjwa wa kansa, wako *terminal stage*, ni wale wanaongojea kufa. Kwa sababu ya hizo teknolojia wamekuwa wanagunduliwa mapema na wakienda mapema hospitali na wengi wamekuwa wanapona kwa sababu ya teknolojia ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kule kwenye majimbo yetu kila mwaka walikuwa wanakufa akinamama 556. Leo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutengeneza vile vituo vimeshuka kwenu, teknolojia imeshuka kwenu na mafunzo yamefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alisimama hapa akasisitiza kwenye eneo la afya ya mama na mtoto. Leo tunapozungumzia *WHO* walitegemea mwaka 2025 yaani

mwakani walitegemea nchi hii tushushe vifo vya akinamama na watoto mpaka 250, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kushusha teknolojia kwenye vituo na kupeleka huduma karibu na wananchi leo idadi ya vifo vya akinamama imeshuka mpaka imefika 104. *WHO* sasa hivi wanajiuliza ni nini Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan anachofanya. Maana yake ni nini? Naendelea kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, tusisahaulishwe ni nini kimefanyika kipindi chetu tukiwa Wabunge na ni nini Mheshimiwa Rais wetu amefanya kwenye majimbo yetu na ni nini Rais wetu amefanya kwenye nchi yetu yanapotokea matatizo madogo madogo kama haya mengine yanayotokana na mafuriko na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mheshimiwa Rais wetu amefanya mapinduzi makubwa sana kwenye teknolojia na tiba. Asilimia 97 ya tiba tulizokuwa tunafuata nje na asilimia 97 ya teknolojia tulizokuwa tunafuata India, Ulaya na Marekani, leo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, amenunua tiba hiyo iko Tanzania na tunatibiwa hapa hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wanakumbuka tulipokutana naye wakati wa UVIKO pale kwenye Ukumbi wa Jakaya Kikwete, alisema kwa nguvu kabisa; "Nunueni vifaa na teknolojia za kisasa kabisa duniani lakini nunueni vifaa kwenye *reputable institute* ambazo tunaweza tukawa na *future* na hivyo vifaa." Akatuelekeza moja kwa moja, leo nataka kuwaambia tunaanza na Muhimbili. Vifaa vyote na maabara zetu zile za kupima mambo mengi na vile vifaa ambavyo Mheshimiwa Rais wetu ametununulia vina uwezo wa kutumia *artificial intelligence*. Tunaenda kuanza na Muhimbili, tutaweka *software*. Kwa hiyo ukifika Muhimbili ukiingia pale anatumika binadamu lakini pia *artificial intelligence* na ubora wa kuweza kuona magonjwa utaongezeka. Huyo ndiyo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, anafanya *revolution* kwenye hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alipokwenda Marekani, alikutana na Chuo Kikuu cha South Carolina...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri...

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia hili moja tu la mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu alikwenda Marekani akakutana na Chuo Kikuu cha *South Carolina*, imefanya *revolution* kubwa sana. Kesho kutwa tunaanza Muhimbili wagonjwa wote wa sukari hawatatobolewa tobolewa tena. Inakuja teknolojia kwa kushirikiana na *South Carolina* na sasa wataanza tu kupimwa kwa kuchukua mate, wanaangalia sukari bila kuhitaji kujitoboa kila siku. Tukishafanya hiyo *test* tunaanza sasa ku-*roll out* na wagonjwa wote wa sukari watakuwa wanatumia teknolojia ya kisasa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yao, tutaendelea kufanya kazi, lakini naendelea kuwasisitiza, watu wameamka kule majimboni kwetu na watu wameamka huku Taifani wasitusahaulishwe mambo ya msingi ambayo Mheshimiwa Rais wetu amefanya. Wasitusahaulishe mambo ya msingi ambayo tumefanya kwenye majimbo. Tujikite kwenye makubwa ambayo yametokea kwenye majimbo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Nimeshuhudia juzi Muhimbili, watoto wakifanyiwa operesheni bila kupasuliwa. Kwa hiyo, mnafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kihenzile, ajiandae Mheshimiwa Kitandula.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja ya hotuba ambayo imetolewa na Mheshimiwa Waziri wetu Mkuu, ambayo imebeba vitu vingi sana kwa maslahi ya Taifa letu. Naomba nichangie mambo machache pengine kwa haraka haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza iliyowekezwa kwenye Wizara yetu ni kuwezesha Mamlaka ya Bandari ili kuongeza wigo wa kukusanya mapato. Serikali ya Awamu ya Sita

inaenda kuingia katika rekodi ya Serikali ambazo zinafanya mapinduzi makubwa sana kwenye upande wa bandari. Ukianza kabisa tunao mradi mkubwa wa *DMDP* ambao tumeboresha gati namba moja mpaka gati namba saba na gati namba nane mpaka namba 11. Mradi huu ni wa shilingi trilioni moja. Pia, juzi tarehe 26 Mwezi wa Pili, 2024 tumesaini mkataba mkubwa wa kujenga matenki ya kuhifadhia mafuta. Hili ni moja kati ya mambo ambayo tuna kila sababu ya kutembea kifua mbele kwa sababu yanagusa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matenki haya yanakwenda kuhifadhi *cubic litre* 420,000, una gharama ya bilioni 680. Faida zake ni nini? Nitasema kwa ufupi. Moja, inapunguza siku za ushushaji wa mafuta katika meli kutoka siku saba mpaka siku mbili. Pili, inapunguza gharama za meli za kukaa bandarini. Tatu, inapunguza gharama za mafuta yenyewe kwa watumiaji. Hivyo ni mradi mkubwa ambao Serikali yetu imeelekeza nguvu kubwa sana na kuhakikisha tunafanya pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maboresho makubwa kwenye Bandari ya Dar es Salaam, pia tumefanya uwekezaji. Tumempa mtu ambaye atatusaidia kufanya uwekezaji pale ndani, kuendesha ili kuongeza mapato zaidi. Sambamba na Bandari ya Dar es Salaam, tumefanya uwekezaji. Tunakwenda kufanya maboresho Bandari ya Kisiwa Mgao – Mtwara ambayo ni maalum kwa kusafirisha makaa ya mawe, *cement* na bidhaa chafu kutoka nchini kwetu kwenda mahali pengine. Tunafanya maboresho makubwa *Mbamba Bay* na mkataba umeshasainiwa na mkandarasi yuko *site*. Tunafanya maboresho makubwa Bandari ya Kemondo, Bukoba na *North Mwanza*, Ziwa Victoria kote huko ni kuongeza matumizi makubwa ya bandari zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, inakwenda sambamba na ujenzi wa meli zetu. Tumesaini mkataba wa zaidi ya bilioni 600 hapo majuzi Kigoma ambao tunajenga kiwanda kikubwa cha kutengeneza na kukarabati meli pale Ziwa Tanganyika *(ship yard)*. Pia, tunajenga meli mpya ya tani 3,500 ya mizigo Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria. Yote haya kwa umoja

wake ni uwekezaji mkubwa kwenye upande wa bandari pamoja na vifaa ambavyo vinatusaidia kwa ajili ya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwepo pia na hoja ya Bandari yetu ya Lindi, ambayo ni bandari inaendelea kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi wetu na sisi tunaendelea kuiboresha hatua kwa hatua ili matumizi yake yaweze kuendelea kuwa makubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja nyingine kuhusu kuboresha na kupunguza changamoto mbalimbali ambazo zipo kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam, tunaiagiza Mamlaka ya Bandari kuendelea kukaa chini na kutazama changamoto ndogo ndogo ambazo ziko pale kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wananufaika nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa Viwanja vya Ndege. Serikali hii ya Awamu ya Sita, kupitia bajeti iliyopita na zinazoendelea tumeona uwekezaji mkubwa sana kwenye Viwanja vya Ndege. Kwa mara ya kwanza, karibu viwanja vyote vya ndege nchini vinajengwa, vinakarabatiwa ama vinaboreshwa kwa namna nyingine. Tuna Uwanja wetu wa Msalato mpya unajengwa hapa Dodoma, tuna Uwanja wa Mbeya upo hatua za mwishoni umeshakamilika, tuna uwanja wa Kigoma, Mpanda, Tabora, Mtwara na maeneo mengine. Uwanja wa Arusha *(TAA)*, uwanja wa Mwanza (Jengo la Abiria), uwanja wa Shinyanga Mkandarasi yupo *site*, Simiyu tupo katika hatua ya kutwaa ardhi na maeneo karibu yote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo la kutembea kifua mbele na kujidai kwa sababu kazi hii inakwenda kutunufaisha Watanzania, *specifically* kwa maana ya Mwanza kuifanya iwe ya kimataifa na nazingatia kengele yako ya kwanza imeshagongwa, tayari tunatoa wavamizi ili kutwaa eneo, tunaendelea na taratibu zetu za kisheria ili uwe wa kimataifa pamoja na kujenga jengo la abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana ya eneo la mwisho la reli, tunafahamu reli ni roho ya uchumi wa Taifa letu. Serikali hii

ilipoingia madarakani tulikuwa na Reli ya *TAZARA* pekee yake kutoka hapa mpaka Kapiri Mposhi, Zambia iliyojengwa kipindi cha ukoloni miaka hiyo kilomita 1,600. Tunajenga reli takribani mpaka sasa hivi kilomita 2,300 kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza, kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma na kutoka Uvinza, Buhigwe mpaka Msongati, huu ni uwekezaji mkubwa ambao tunaufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo imejengwa hoja kuhusiana na lini tutaanza ujenzi wa Reli ya Kusini. Tunatambua kama Serikali umuhimu wa Reli ya Kusini *(Mtwara Corridor)* ndiyo maana moja, tumeanza kujenga bandari ya *Cargo* kama nilivyosema. Pili, tumeshamaliza upembuzi yakinifu, hatua iliyopo kwa sasa hivi tumeanza kutafuta Mwekezaji wa kuweza kuingia naye *PPP* ili kuweza kuanza kujenga reli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, ipo hoja ambayo imejengwa na Mheshimiwa Mbunge wetu wa Ifakara kuhusiana na Mlimba. Moja, tulikwenda eneo husika tumeona mafuriko yaliavyoathiri watu wa Ifakara pamoja na Mlimba kwa ujumla. Hatua ya kwanza, tulipeleka helikopta kupeleka vyakula, hatua ya pili, treni ya Mwakyembe inafanya kazi sasa hivi kutoka Dar es Salaam kwenda mpaka Mlimba, hatua ya tatu tunaendelea kufukua ili reli ile ibaki safi. Pia, ushauri wake kuhusu maboresho ya sheria tumeupokea. Mwisho katika eneo hilo, mabadiliko ya sheria tuko kwenye hatua mbalimbali tutayafanyia kazi na tukikamilisha tutaleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Venant Protas pia amezungumzia habari ya fidia na ujenzi wa shule, tunamuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tunakwenda kujenga shule katika eneo lake kama ambavyo tulikuwa tumeahidi hapo nyuma na makaburi yale aliyoyaeleza kwenye Kata nne kama sehemu ya fidia, pia tutakwenda kukamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, fidia ya majengo na makazi kama ilivyoahidiwa tutakwenda kukamilisha na naiahidi Mamlaka ya Reli, wenzetu wa *TRC* waende wakafanye mchakato waharakishe ili kuhakikisha kwamba fidia katika maeneo ya pale Igalula yanakamilika sambamba na kuanza mchakato wa

kujenga shule hiyo kama ilivyoahidiwa na Viongozi wetu Wakuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na habari ya *SGR* kuhusiana na malalamiko ya wananchi wa kule Itigi wanaolipwa shilingi 200,000 kwa heka. Tunaiagiza Mamlaka yetu ya Reli pia iende ikafuate sheria, kwa mujibu wa sheria ndiyo wananchi wetu waweze kulipwa hizo fidia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge Genzabuke, anaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita na namshukuru sana kwa kupongeza ni wachache sana wanaoweza kutambua kazi kubwa na uwekezaji mkubwa unaofanywa, Mheshimiwa Mbunge amelitambua hilo na ameiambia Serikali, juhudi ziongezeke. Tunamhakikishia kwamba tutaongeza zaidi juhudi kwa sababu tunafahamu namna pekee ya kujenga uchumi wa Taifa letu …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kengele ya pili hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kitandula, ajiandae Mheshimiwa Hamad Chande.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi ambavyo wamechangia kwenye eneo la Sekta ya Maliasili na Utalii kupitia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nawashukuru kwa sababu michango hii imezidi kuboresha yale ambayo tunakusudia kuyafanya katika Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge kama wanavyofahamu, tumejitahidi sana katika kipindi hiki kuwa karibu nao, kufungua milango kwa kila mmoja wao ili tuweze kusikia kutoka kwao nini changamoto wanazokabiliana nazo kwenye Majimbo yao ili nasi tuweze kukidhi mahitaji na matarajio yao. Niwaahidi tutaendelea kuwa karibu nao na kuwasikiliza ili kuweza kutatua changamoto zinazotukabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda hoja zilizoibuliwa ni nyingi, lakini nitajibu chache kwa ujumla na kwa sababu tunaelekea kwenye hotuba ya bajeti yetu huko mbele ya safari, basi majibu mengi tutayapata kule, vilevile tutaandaa majibu ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie hoja chache ambazo zimejitokeza. Eneo la kwanza ni jambo kubwa linalofanywa na Serikali yetu la kufanya uhamishaji wa wananchi kwa hiari kutoka Ngorongoro kwenda kwenye maeneo mengine ya nchi yetu. Jambo hili ni muhimu kwetu sote, ni jambo ambalo linakwenda kuboresha au kuimarisha utu wa Mtanzania, kwa hiyo sisi sote kama viongozi tuna wajibu wa kuliunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa sababu jambo hili linafanyika kwa umakini mkubwa na amekuwa karibu sana kutoa miongozo na maelekezo ya jinsi ya kuliendea jambo hili. Kazi kubwa imefanyika kwa wale ndugu zetu ambao wamehamishwa kwa hiari kutoka Ngorongoro kwenda Msomera na maeneo mengine, uhamasishaji mkubwa sana unafanyika wa kuwaonesha ndugu zetu faida ya wao kukubali kuondoka kwa hiari kwenye eneo hili na kwenda kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Msomera wote tunafahamu kazi kubwa imefanyika ya kujenga makazi ya wananchi, ya kujenga nyumba, ya kuwapatia wananchi wanaokubali kuhama ardhi ekari tano kwa kila kaya, lakini vilevile wamekuwa wakipewe fedha takribani shilingi 10,000,000 kwa ajili ya maendelezo waliyoyafanya kwenye maeneo wanapoondoka. Nafurahi kusema kwamba mwitikio wa wananchi kuhamia Msomera ni

mkubwa na sisi ndani ya Serikali tunapata faraja kwamba jambo hili litakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwepo hofu kwamba pengine wapo watu hawatakubali kuhama. Sisi tunaolisimamia jambo hili faraja tunayoipata ni kwamba kuna mwitikio mkubwa, kwa hiyo hakuna sababu ya kuwa na hofu kwamba watu hawatahama. Wananchi wanaelezwa, wanaelewa na mwitikio ni mkubwa. Niwaombe viongozi wenzangu tujitahidi kuhakikisha kwamba tusiwe na tamaa ya kuvuka mto kabla hatujafikia daraja, tusubiri tufikie daraja, tutajua namna gani tunavuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hoja zilizojaribu kuonesha kwamba wananchi waliopo kule wamesahaulika, hawapati huduma za kijamii, jambo hili siyo kweli. Zipo hoja zimejaribu kujengwa hapa kwamba kuna baadhi ya shule hata vyoo havijengwi, nataka niseme nini kinachotokea. Serikali kwa umuhimu wa eneo lile ilipata ushauri wa kitaalam kwamba pengine siyo busara kuendelea kujenga vyoo kwenye maeneo yale. Kwa hiyo, nini ambacho Serikali imefanya? Serikali tulichofanya ni kuja na utaratibu mahsusi wa kuhakikisha vyoo vyote vinavyotumika sasa kuwe na utaratibu wa kuvinyonya ule uchafu uliopo ili uende ukahifadhiwe kwenye shimo moja pekee yake ili vyoo vile viweze kuendelea kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza zoezi hili limefanyika katika Shule ya Msingi ya Endulen limekamilika kwa 80%. Tunaendelea na zoezi hili kwenye shule za msingi, tunaendelea na zoezi hili kwenye vituo vya afya, tunaendelea na zoezi hili na kwenye zahanati zetu. Niwasihi sana Waheshimiwa kama kuna jambo halieleweki milango yetu ipo wazi, waje tutapeana maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo limejaribu kuoneshwa hapa kwamba hata lile jambo la kutoa misaada ya kielimu kwa wanafunzi wanaotoka kwenye eneo hili, ambao wanatoka kwenye kaya ambazo hazina uwezo sasa limesitishwa. Jambo hili nalo siyo kweli. Tangu tumeanzisha utaratibu huu, Serikali imekwishalipia ada wanafunzi takribani 14,000. Hivi

ninavyozungumza kwa mwaka huu wa fedha mpaka kufikia mwezi Machi, tayari Serikali imelipa zaidi ya shilingi 925,051,120. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kinachoendelea sasa? Kinachoendelea sasa ni kwamba utaratibu wa kuwalipia wanafunzi hao unasimamiwa na Baraza la Wafugaji wenyewe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante, mengine utatoa taarifa ya maandishi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri na majibu sahihi. Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, ajiandae Mheshimiwa Mathew Kundo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fusa hii. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Rahim*, mwingi wa rehema, mwenye kurehemu kwa kutuwezesha kuwepo katika Bunge hili na mijadala yetu tukiwa katika hali ya uzima na afya. Pili, nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia, wametoa ushauri mzuri, wametoa hoja njema za kujenga, lakini sitoweza kujibu moja baada ya nyingine, naomba uniruhusu niweze kutoa maelezo kwa hoja chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo hoja kwanza ambayo imetolewa na Ndugu yetu Mheshimiwa Kilumbe, katika hoja yake anashauri kwamba, wakandarasi na wazabuni Serikali iwalipe kwa wakati, tunalitambua hilo na Serikali inaendelea kulipa madeni ya wakandarasi na wazabuni siku hadi siku. Hivi ninavyoongea sasa hivi mpaka kufika leo tayari bilioni 882.5 zimeshalipwa kwa

wakandarasi. Hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine kwamba kadri fedha zitakavyopatikana, basi madeni hayo yatalipwa kwa wakandarasi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ilikuwa ni hoja ya Mheshimiwa Kilumbe, anasema kwamba *PPRA* waimarishe mfumo wa *NeST*. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wenzangu kwamba Mfumo wa *NeST* uko vizuri sana, ni mfumo wa kizalendo, ni mfumo ambao taarifa zetu ziko salama ikilinganishwa na mfumo uliokuwepo nyuma *TANePS*, kwamba taarifa zetu zilikuwa zipo nje ya mawanda yetu, leo kupitia *NeST* taarifa zetu zipo salama na bahati nzuri wanaosimamia mfumo ule ni wazalendo yaani ni wananchi wa Tanzania wenyewe, hakuna mtu mgeni ambaye anausimamia mfumo ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mfumo huu utaendelea kutoa mafunzo mazuri kwa wazabuni wote nchini, hivi ninavyozungumza sasa wazabuni 2,170 tayari wameshapatiwa mafunzo na milango iko wazi. Katika hili nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwa fedha nyingi ambayo ameiweka pale kwa ajili ya utekelezaji na ujenzi wa mfumo huu. Hapa Mkurugenzi Mkuu, Ndugu yetu Maswi apewe maua yake kwa usimamizi mzuri wa *PPRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine imetolewa na Mheshimiwa Mariam Nyoka, kwamba fedha bilioni moja itolewe kwa ndugu zetu wenye ulemavu, fedha hii tayari imeshatolewa na imeshafika kunapohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ambayo nitazungumza ni hoja ya Mheshimiwa Innocent Bilakwate, anasema kwamba Serikali iendelee kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kudai risiti wakati wa manunuzi. Kwa kweli suala hili ni changamoto, naomba niwaombe Wabunge wenzangu na wananchi wote, tuwe na utamaduni wa kudai risiti tunaponunua na wale wafanyabiashara wawe na utamaduni wa kutoa risiti, yaani iwe kama ni utamaduni wetu kama vile mtu akiamka

asubuhi anatafuta maji kuosha uso ama kuoga basi akifanya manunuzi lazima atoe risiti na mteja adai risiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo kaulimbiu inayosema tuwajibike. Ni lazima tuwajibike, suala la ukusanyaji wa kodi lisiwe ni suala la Serikali na *TRA* peke yake, suala hili liwe ni wajibu na jukumu la kila mtu hapa nchini kwa sababu maendeleo yetu yanahitaji makusanyo yetu ya fedha. Leo kila Mbunge tunatoa hoja kwamba barabara yangu imefanya hivi, barabara yangu imebomoka zinahitajika fedha, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuwajibike.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tumetengeneza kwamba mteja wajibu wake ni kudai risiti halisi na thamani ya kile alichokinunua, lakini mfanyabiashara wajibu wake ni kutoa risiti, tena risiti halisi na thamani ya kile ambacho amekiuza. Nini wajibu wa *TRA? TRA* wajibu wake ni kukusanya kodi kwa ufanisi, kwa uhalisia bila kutumia nguvu na fedha hiyo kuirudisha Serikalini na wajibu wa Serikali unaonekana ni kupeleka maendeleo kila sehemu, kujenga miradi ya maendeleo na mwenye macho haambiwi tazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila jimbo, kila wilaya inaonekana miradi ya maendeleo iliyofanyika kama siyo afya, basi miradi ya elimu kama siyo elimu basi miradi ya barabara. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kwa yale ambayo hatujayajibu, basi tunayachukua na tutajibu kwa maandishi na tunaenda kuyafanyia kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mathew Kundo jiandae Mheshimiwa Anthony Mavunde.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu. Kwa upekee kabisa niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa namna ambavyo wamegusia katika Sekta yetu ya Maji, nasimama hapa nikiwa naelewa kabisa kwamba Sekta ya Maji, inagusa nyenzo muhimu sana katika uhai wa binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia ni zaidi ya sita, lakini wote kwa umoja wao wameonyesha namna ambavyo wanataka kuharakisha miradi ya maji na kuboresha namna ambavyo Wakandarasi wetu wanafanya. Miradi ya maji inayoendelea nchini iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji, lakini vilevile ipo katika hatua ambazo zinaenda kuleta huduma ya maji kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba miradi hii itakamilika kabla ya muda, kwa sababu wiki iliyopita Serikali imetoa fedha bilioni 60 kwa ajili ya kuanza kulipa Wakandarasi ambao wanatekeleza miradi ya maji vijijini. Leo asubuhi nimejulishwa na Katibu Mkuu, Mfuko wetu wa Maji pia tumeweza kupata bilioni 18. Kwa hiyo, kwa ujumla tuna bilioni 78 kwa ajili ya kuhakikisha miradi yetu ya maji huko vijijini inaendelea kutekelezwa na ili iweze kukamilika kwa wakati. Hizi ni dalili tosha kabisa za kuonesha kwamba tunaye Rais, ambaye anajali Watanzania, tuna Rais ambaye amejikita katika utoaji wa huduma za msingi kabisa kwa Watanzania, hivyo tuendelee kumuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika yale ambayo yameongelewa na Waheshimiwa Wabunge, naomba nigusie jambo ambalo ameongea Mheshimiwa Issa, Mbunge wa Kibamba kuhusu bwawa la Kidunda. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Mheshimiwa Rais, ametoa fedha takribani bilioni 49 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba bwawa hili ambalo ndilo linaenda kutoa uhakika wa maji katika Mto Ruvu ambao ndiyo chanzo cha maji yanayopatikana katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa hili limefikia katika 20% ya utekelezaji wake na litakapokamilika litaweza kutoa lita bilioni 190 ambapo zitakuwa zina uwezo wa kuhudumia mikoa ya jirani pamoja na Dar es Salaam. Vilevile katika ujenzi wa bwawa hili, kuna ujenzi wa kituo cha kufua umeme ambapo takribani *Megawatt* 20 zitazalishwa pale. Pia kuna njia kuu ya msongo mkubwa wa umeme kutoka Kidunda mpaka Chalinze takribani

kilometa 101. Maana yake ni kwamba tunaenda kuwa na uhakika wa huduma mbalimbali unaotokana na bwawa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuongelea Bwawa la Farkwa. Mheshimiwa Kunti amejaribu kuligusia katika kuchangia kwake na ameonyesha hofu yake, lakini nimhakikishie kwamba Serikali iliingia makubaliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika na takribani dola za Kimarekani 125 zilitolewa. Tunafahamu kabisa kwamba bwawa hili limekuwa na changamoto kidogo kwa sababu ya kubadilika kwa mahitaji ya maji na kubadilika kwa wingi wa watu katika Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumepata mtaalamu mshauri ili aweze kupitia ule usanifu wa bwawa na kuhakikisha kwamba anapitia mpango wa kulinda na kutunza mazingira ambayo ndiyo chanzo cha maji kitakachokuwa kinapeleka katika lile bwawa. Kwa hiyo, tunaamini kwamba akishapitia huu usanifu, maana tumempatia muda mpaka mwezi wa Tisa awe amekamilisha ili ujenzi wa bwawa hili uanze mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Waheshimiwa Wabunge tunafahamu kwamba miradi ya maji ni miradi muhimu sana. Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imejikita kuhakikisha kwamba miradi hii inakamilika kama ambavyo imepangwa na hili bwawa pamoja na mabwawa mengine, kwa sababu mabwawa yapo mengi ambayo yanaendelea katika hatua mbalimbali. Tuna uhakika kwamba kwa sababu tunaenda kwenye bajeti ijayo, Waheshimiwa Wabunge watatuunga mkono ili tuweze kuhakikisha kwamba miradi hii tunaisimamia ili iweze kukamilika na iweze kutoa huduma ya maji kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba changamoto ya maji katika Jiji la Dodoma inaendelea kuwepo, lakini tuna miradi 15 inayoendelea katika Jiji la Dodoma. Vilevile tuna miradi 78 ambayo inaendelea katika Mkoa wa Dodoma ambapo miradi hiyo ina takribani shilingi bilioni 54 na watu takribani 400,900 wanaenda kunufaika na huduma hii ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba changamoto ya Dodoma hatuwezi kuitatua kwa mpango wa muda mrefu peke yake. Serikali imejipanga katika mpango wa muda mfupi, muda wa kati na vilevile muda mrefu. Mpango wa muda wa kati kwa Jiji la Dodoma, tayari tuna miradi midogo midogo 15 ambayo inaendelea kujengwa katika maeneo ya Nzuguni, Nala na maeneo mengine ili kuhakikisha angalau wananchi wanaokuja katika Jiji la Dodoma na wananchi wanaoishi katika Jiji la Dodoma hawapati changamoto yoyote ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo tunaomba muwe na subira, pale ambapo kutakuwa na changamoto, tunaamini kwamba kila changamoto tutaichukua kwa uzito wake kwa sababu tunaamini kutatua changamoto na kuhakikisha huduma zinazidi kuimarishwa na kuboreshwa, ndiyo mafanikio ya Taifa letu na ndiyo mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu, na Waheshimiwa Wabunge, niwahakikishie kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Sekta ya Maji ameendelea kufungua kapu lake na ameendelea kuonesha kwamba kumtua ndoo mama kichwani...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, muda wako umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo kipaumbele katika kuhakikisha kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, mengine yajibu kwa maandishi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Yaliyobakia jibu kwa maandishi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mavunde, halafu Mheshimiwa Bashe jiandae.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na ninaunga mkono hoja. Moja kati ya hoja ambazo zilizungumzwa wakati wa kuchangia bajeti hii ni hoja ya mradi wa Nyanzaga pale Sengerema ambapo Mheshimiwa Mbunge alichukua fursa hii kutamka mbele ya Bunge hili kutaka Serikali itoe ufafanuzi wa hali ilipofikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Tabasam kwani amekuwa ni sehemu muhimu katika mradi huu ambao utawanufaisha wananchi wa Sengerema na Tanzania kwa ujumla. Mradi wa Nyanzaga upo chini ya Kampuni ya Ubia ya *Sotta Minning* ambapo Kampuni ya *Ore Corp* ina 84% na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina 16%.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo katikati ilijitokeza kampuni ambayo ilikuwa inaitwa *Silver Corp* ambayo walionesha nia ya kununua hisa za *Ore Corp* na hatua hii ilisababisha kufungua *scheme of arrangement* katika nchi ya Australia kwa mujibu wa Sheria za makampuni ya Australia katika kuzipata hizo hisa za *Ore Corp*. Katikati ya mchakato ilitokea kampuni nyingine ya *Perseus* ambao wao walikuja na *superior offer* na wakanunua hisa za kampuni ya *Ore Corp* ambayo mchakato wote huo hauathiri hata kidogo ubia kati ya Serikali na Kampuni ya *Ore Corp* katika Kampuni ya *Sotta Minning*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niwatoe hofu Watanzania kwamba baada ya kukamilika mchakato wote huo wa *Ore Corp, Silver Corp* na *Perseus*, hivi sasa kampuni ya *Persus* wao ndiyo wamekuwa na *offer* kubwa nao ndio watanunua hisa za *Ore Corp* na itakuwa sasa ni Serikali 16% kama ilivyokuwa awali na *Ore Corp* 84%.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyozungumza hivi sasa, tayari wale ambao wameshinda *offer* Kampuni ya *Perseus* wanaingia nchini tarehe 18 na tarehe 19 nitakutana nao hapa Dodoma kwa ajili ya mazungumzo. Nchi itanufaika kama ifuatavyo na ndiyo ilikuwa hoja ya Mheshimiwa Tabasamu: Kwanza, kabla ya mchakato wote huu sisi kama Wizara ya Madini tuliwaandikia *TRA* kuufuatilia mchakato huu na nchi itapata *capital gain tax* baada ya mchakato huu kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa sababu Sheria inataka kampuni yoyote ya Australia ambayo inafanya *acquisition* ya *shares* lazima ipate *approval* ya taasisi muhimu ya nchi husika na hapa ilikuwa ni *FCC,* kwa mujibu wa Sheria ya Madini, kifungu Na. 10 kinasema, "Serikali itakuwa ina hisa zisizopungua 16% ambazo hazififishwi;" baada ya kampuni ile *Perseus* kuja hapa nchini tulikaa nao na kuzungumza nao. Katika majadiliano Serikali inatoka katika umiliki wa hisa 16% mpaka 20%, yaani tumeongeza hisa nne. Haya ni manufaa makubwa sana katika uchumi wa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho katika hoja hii ya Mheshimiwa Tabasam ilikuwa, ni lini mradi unaanza? Kwa mujibu wa *timeline,* nusu ya pili ya mwaka 2025 Kampuni ya *Perseus* wanapaswa waanze kutoa dhahabu ya kwanza katika mgodi pale Sengerema. Kwa hiyo, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Mbunge mahususi kwamba jambo hili linakwenda kufanyika na litafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ambayo ilizungumzwa hapa ndani, ni kuhusu utafiti wa *Helium* ambao unaendelea katika Bonde Rukwa. Ni kweli katika Bonde Rukwa tuna utafiti wa kampuni kubwa mbili ya *Helium One* na *Noble Helium.* Wamefanya utafiti katika eneo hili na imepatikana *Helium* nyingi na ya kutosha sana na *Helium* hii inakwenda kuiweka Tanzania katika ramani ya dunia kati ya nchi chache ambazo zitakuwa zina uwezo wa kuzalisha *Helium* ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwaondoa Marekani na Urusi, Tanzania sisi, tunafuatia kwa kuwa na kiwango kikubwa cha

*Helium*. Kwa hiyo, ni jambo ambalo kama Serikali tumelichukulia kwa uzito mkubwa na kama inavyofahamika kwamba katika *Helium* hii ni mahususi sana kwa ajili ya vifaa vya kielektroniki na *MRI,* kwa hiyo, nchi itakuwa imepata faida kubwa kutokana na jambo hili ambalo linaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mwisho ni kuhusu maeneo kwa wachimbaji wadogo. Nataka niwaondolee wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, tumekuwa na changamoto ya watu wengi hasa wawekezaji wakubwa kushikilia maeneo makubwa pasipo kuyafanyia kazi. Wiki tatu zilizopita nimefuta maombi na leseni 2,648 kwa ajili ya kuyafanya maeneo haya yabaki wazi na tutayapanga vizuri na tutawapatia wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuja na *program* kama ile ya kilimo ya *BBT,* lakini ya kwetu ni *MBT (Mining for a Brighter Tomorrow)* ambapo tutawapanga vizuri akina mama na vijana na maeneo haya watayafanyia kazi na mwisho wa siku nchi yetu itanufaika na *program* hizi. Sambamba na hilo, pia tumejipanga kukamilisha ule utafiti wa kina kabisa kwa maana ya *High Resolution Airborne Geophysical Survey* ili tuweze kufahamu ni kiasi gani cha madini tulichonacho chini ya ardhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi cha bajeti yangu nitasema hatua ambayo tumeifikia, ni hatua ambayo inapendezesha sana. Ni hatua nzuri, kwani tunakwenda kuikomboa nchi yetu katika rasilimali ya madini na Watanzania hawatachimba tena kwa kubahatisha, tutawaongoza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bashe, ajiandae Mheshimiwa Ulega na Mheshimiwa Afande Sillo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Jambo la pili, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba yake nzuri. Vilevile niseme naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge zaidi ya 21 wamechangia na kutoa maoni mbalimbali. Yale ya ushauri tumeyapokea na tutaendelea kuyafanyia kazi na mengine tutayajibu tutakapokuja kwenye Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya eneo ambalo wameliongelea Waheshimiwa Wabunge ni matumizi ya rasilimali za maji katika Bonde la Mto Rufiji. Nataka nilitaarifu Bunge lako Tukufu, upembuzi yakinifu wa hekta 67,000 wa Bonde la Mto Rufiji umekamilika na tarehe 20 mwezi huu tunatangaza *tender* ya kwanza ya ujenzi wa mabwawa makubwa mawili ambayo yatakuwa na uwezo wa kukusanya maji *cubic meter* 269,000,000 na ujenzi wa hekta 17,000 zinatangazwa tarehe 20 mwezi huu na mabwawa mengine yatafuatia katika mwaka ujao wa fedha kadri ambavyo bajeti itakuwa inaturuhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nataka nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba *Kilombero Valley* tayari mkandarasi ameshapatikana. Kwa hiyo, kazi inayofanyika katika eneo la Kilombero ni ukamilishaji wa upembuzi yakinifu kwa ajili ya *flood control* na ujenzi wa mabwawa chini ya Kihansi ili maji yanapofunguliwa yaweze kuhifadhiwa na wakulima wa maeneo yale waweze kutumia rasilimali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ya Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ni kuhusu *NFRA*. Waheshimiwa Wabunge wa maeneo ya kilimo cha mahindi nataka niwahakikishie na niwaambie wakulima wasiwe na hofu. Serikali itanunua mahindi na tutanunua kwa bei nzuri. Hivi sasa tupo kwenye hatua za mwisho za majadiliano na nchi ya Zambia, Mozambique na Namibia kwa ajili ya kununua mahindi kutoka *National Food Reserve Agency*. Tunamaliza nao mazungumzo na *NFRA* itaanza kununua na tutaanza kuuza mahindi tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwatake wakulima wa maeneo ya mahindi ambao baadhi ya maeneo wameanza kuvuna, msikimbilie kuuza mahindi yenu kwa bei rahisi, Serikali itakuja kununua. Nimewaambia wafanyabiashara wa mahindi

wote tunawaruhusu kuuza mahindi katika nchi zinazotuzunguka ambazo zimekuwa na matatizo ya chakula. Hatutawaruhusu kwenda kuuza mahindi kwa bei ya kutupa kwa sababu siku ya mwisho atakayepata hasara ni mkulima. Kwa hiyo, tumewaelekeza haya na tumeshaanza kuwapa *export permit*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubaliana na *WFP* ambao wamepata mkataba kutoka Malawi, tutawauzia unga badala ya kuwauzia mahindi, na hivi sasa vinu vyetu vya *CPD* vimeanza kusaga jumla ya tani 30,000. Kwa hiyo, hizi ni hatua ambazo tunachukua. Nataka niwahakikishie wakulima, msiwe na hofu na *bumper harvest* mliyonayo. Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia ipo na tumeshapata *approval* kutoka Wizara ya Fedha. Tunachukua fedha kutoka *Commercial Bank* kuwa ku-*supported* na mikataba tunayoingia na hizi nchi na tutanunua mahindi ya wakulima yote bila hofu yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine Waheshimiwa Wabunge wameongelea suala la *BBT*. Nataka nirudie tena, *BBT* ni *program* ya muda mrefu. Katika bajeti ya mwaka kesho 2025/2026 tutapeleka *program* ya *BBT* katika halmashauri, kwa kila halmashauri na tutaanza na halmashauri 100 za kwanza, mtuvumilie. Serikali itapeleka fedha ya kujenga miundombinu ili halmashauri zianze kuandaa maeneo kwa ajili ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali katika *program* ya *BBT* sasa hivi, jumla ya vijana 118 wamepewa jumla ya shilingi milioni 917 na Serikali ya Awamu ya Sita ambao wanajishughulisha katika shughuli za kilimo katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu. Serikali itaendelea kufanya hivyo na mwaka kesho katika bajeti tutaweka shilingi bilioni 10 ku-*support* vijana walioko huko vijijini wanaofanya shughuli za kilimo kwa ajili ya kupewa fedha kutoka mfuko wa pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni la upimaji wa afya ya udongo. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, tumeshasambaza vipima afya ya udongo 142 katika halmashauri zetu. Sasa hivi mfumo wa upimaji wa afya ya udongo ni *real time*

na wakulima watapewa *certificate*. Ni huduma ya bure. Ninachotaka kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, wote sisi ni Wajumbe wa Baraza la Madiwani. Twendeni tukawaulize Wakurugenzi wa Halmashauri, umeletewa mashine ya kupima afya ya udongo katika halmashauri yako, umepimia wakulima wangapi? Tupe taarifa na sisi mtusaidie kusimamia katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni hoja ya mbegu. Bila kutatua tatizo, kwanza tuna changamoto ya mbegu. Huu ni ukweli kwamba kwa muda mrefu kama Taifa hatujawekeza katika eneo hili. Kwa mara ya kwanza mwaka huu tumeweza kujitosheleza 50% ya mahitaji ya mbegu zetu na zimezalishwa ndani ya nchi yetu jumla ya tani 60,000. Ni matarajio ya Serikali kufikia mwaka 2025/2026 tuweze kujitosheleza kwa 100%, lakini tunawagawia wazalishaji wa mbegu wa ndani, mashamba ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote mashamba yetu yamekuwa yakibaki pori, hayaendelezwi, kwa hiyo tunawapanga Watanzania nao wanazalisha katika mashamba tuliyonayo. Nataka niwahakikishie kwamba tunapokea maoni sasa hivi. Tunashukuru hoja ya wakulima...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Bashe. Kengele ya pili hiyo, mengine jibu kwa maandishi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Mheshimiwa Ulega, jiandae Mheshimiwa Sillo.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuungana na wenzangu wote waliotangulia kuipongeza hotuba hii ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri

Mkuu. Vilevile naomba nichukue fursa hii kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa pole kwa mafuriko yanayoendelea nchini kote ambapo tumeshuhudia na kwa upande wa Mkoani kwetu Pwani Wilaya ya Rufiji na Wilaya ya Kibiti zimepata changamoto hii kwa mapana sana. Tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa zoezi kuratibiwa vyema na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tumeshuhudia namna ambavyo Serikali imekuwa imara katika kusimamia vyema changamoto zozote zinazotokea katika Taifa letu. Ni wazi na sote tumeshuhudia kwamba kipimo cha uongozi ni wakati wa changamoto, na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amelithibitisha jambo hili kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, sisi kule kwetu tumepokea misaada ya kiutu ya kutosha ambapo mpaka hivi sasa wananchi wa wilaya hizi wako salama wakiendelea kutazama hali inavyoendelea. Ni ukweli usiopingika kwamba mvua zimenyesha mfululizo na hata sasa zinaendelea kunyesha. Kila siku inayokwenda tunapata mvua. Kwa hiyo tunashukuru Wilaya yetu ya Mkuranga hatuna mafuriko lakini tunajua kwamba iko changamoto kubwa ya uharibifu wa miundombinu. Tunaomba tuendelee kuiunga mkono Serikali yetu inapoangazia jambo hili kwa ukaribu sana. Mheshimiwa Rais amethibitisha ucha Mungu wake, amethibitisha umahiri wake, amethibitisha uchapa kazi wake. Nasi tunaendelea kumwombea aendelee kuwa na afya njema aendelee kulijenga Taifa letu bila ya kikwazo chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepata michango kadhaa, takribani Wabunge 10 wamechangia hoja za mifugo na hoja za uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jambo lililochangiwa hapa ni juu ya uhitaji wa majosho na chanjo kwa ujumla wake. Katika bajeti yetu tunayotarajia kwenda kuisoma hapa Bungeni

tutakuwa na majosho ambayo tumeyaweka tena kama ambavyo tumekuwa tukiyaweka katika bajeti zilizopita. Ni matarajio yetu kwamba halmashauri zetu ambazo zimeleta maombi ya majosho zitapata majosho hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mpango kabambe ambao sasa badala ya kuacha wafugaji wawe wanafanya zoezi la kuchanja mifugo wao wenyewe kwa utaratibu ambao wamejipangia, sasa tunakwenda na zoezi la pamoja. Tutakuwa na ratiba maalum ambayo itasimamiwa vyema na Wizara na hatimaye chanjo ikachanjwe kwa pamoja. Hii itatuepusha sana na wale makanjanja ambapo hata leo asubuhi nimemsikia Mheshimiwa Mbunge mmoja akiuliza swali juu ya dawa *fake*. Kwa hiyo sasa tunataka tuliratibu suala hili sisi wenyewe kama Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, habari njema; kwenye uratibu huu itatusaidia hata kutoa ajira za muda mfupi kwa vijana wengi sana wa Kitanzania waliosoma masomo haya ya mifugo na wako mtaani. Vijana hao tutawachukua na watakuwa ni *part and parcel* ya *programme* hii ya uchanjaji wa mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Waheshimiwa Wabunge wametupa ushauri juu ya kunenepesha mifugo ili kuongeza chachu ya biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi yetu. Ni ukweli usiopingika kwamba, sote tunashuhudia biashara ya nyama inakwenda vizuri sana na hasa wakati huu wa Serikali ya Awamu ya Sita, tunafanya vizuri mno katika uuzaji wa nyama nje ya nchi yetu na *record* ziko wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni biashara ambayo inavutia na tunawakaribisha wawekezaji mbalimbali kwenye eneo hili na sisi Serikali tumejiweka mguu sawa, ndio maana tunayo *programme* yetu ya *BBT* ambayo inafanya vizuri na tunakwenda kuongeza vituo katika Mwaka huu wa Fedha wa 2024/2025. Miongoni mwa vijana watakaotoka katika *programme* hii ya *BBT* tayari tumewaandalia vitalu katika maeneo yetu ya mashamba ya Serikali ya *NARCO* ambayo yatasaidia kuwafanya vijana hawa wawe ni wafanyabiashara *proper* wa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa uvuvi kilichozungumzwa ni suala la maboresho ya sheria. Tuko katika mkakati wa kuhakikisha kwamba sheria na kanuni zetu tunaziboresha na tunapokea maoni ya wadau wote kusudi tuzifanyie marekebisho zile sheria ambazo zinaonekana kuwa ni tatizo kwa wavuvi wetu ili tuweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia iko rai ya kulitumia Bwawa la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa ajili ya upandikizaji wa samaki…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili hiyo.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sillo, Mheshimiwa Profesa Mkenda ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa ufafanuzi wa hoja chache ambazo zimeelekezwa kwenye Wizara yetu ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na timu nzima kwa hotuba nzuri ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko hoja ilitoka kwa Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo ambayo ilihusu changamoto ya upatikanaji wa vitambulisho vya uraia kwa wananchi wanaoishi kwenye mikoa ya mipakani. Sote tunafahamu kwamba vitambulisho vya Taifa hutolewa kwa raia wa Tanzania, lakini pia kwa wageni wenye vibali vya makazi hapa nchini ambao wanakidhi sifa ambazo zimeainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto ya mikoa ya mipakani kuwa na wahamiaji haramu pamoja na walowezi wengi, lakini kati ya mwezi Oktoba, 2023 hadi Machi, 2024, kati ya waombaji 802 ambao waliwasilisha taarifa zao katika Ofisi za Uhamiaji Biharamulo, waombaji 112 walibainika kuwa na matatizo ya uraia. Hivyo pamoja na changamoto hizo ambazo tunakabiliana nazo katika mikoa ya mipakani, nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba waombaji wote ambao wana sifa zinazostahili wanapatiwa vitambulisho vya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili lilikuwa ni eneo la usajili wa vijana hasa baada ya matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022. Mheshimiwa Mariam Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum alitoa hoja kwamba kuna baadhi ya watu ambao bado hawajasajiliwa. Ni kweli tunakubali kwamba wapo vijana wengi na watu ambao wana sifa hasa baada ya matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, wanatakiwa wasajiliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanza kwa zoezi baada ya utambuzi na usajili wa mwaka 2012 hadi tarehe 30 Machi mwaka huu 2024, wananchi ambao tayari wametambuliwa na kusajiliwa ni 24,388,715, lakini namba za utambulisho ambazo zimezalishwa ni 20,920,172, vitambulisho ambavyo tayari vimezalishwa ni 20,548,067.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitambulisho ambavyo vimesambazwa kwa wananchi kwa tarehe tajwa ni 19,734,367. Kwa hiyo, nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, usajili wa watu takribani 7,000,000 na zaidi ambao tayari wametambuliwa hasa baada ya matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 utaendelea kufanyika kwa awamu tatu kuanzia mwaka huu wa fedha 2024/2025. kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 tunatarajia kutambua na kusajili wananchi wapatao milioni mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naunga mkono hoja. Ahsante kwa fursa hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Mkenda.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa fursa hii ya kuchangia…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ashatu ajiandae.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**…hotuba ya Waziri wetu Mkuu na vilevile naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na hoja mbalimbali kuhusu Sekta ya Elimu kwa ujumla wake na mapendekezo mbalimbali. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, mapendekezo haya kwa ujumla wake tunayachukua na tutayafanyia kazi. Hata hivyo, ningependa baadhi niyatolee maelezo kidogo na mojawapo ni kuhusu mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ni kwamba, Serikali ijikite kwenye kuongeza bajeti ya mikopo kwa ajili ya elimu ya juu. Tunapokea ushauri huo na kwenye bajeti yetu tutaona jitihada hizi zikiendelea. Hata hivyo, ningependa tujikumbushe tumetoka wapi katika jambo hili ili vilevile tujipongeze kwa kazi ambayo imeshafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya shilingi bilioni 450 zilitumika kama mikopo kwa elimu ya juu na mwaka wa fedha 2020/2021, fedha ziliongezwa kufikia bilioni 464 kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu, lakini Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alivyoingia madarakani mwezi Machi, muda mfupi tu baada ya kuapa kama tulivyoelezwa hapa wakati ule, aliagiza nyongeza kubwa zaidi kupata kutokea kwenye mikopo ya elimu ya juu na hivyo kuongeza kiasi cha fedha kutoka bilioni 464 kwenda bilioni 570 kwa mkupuo. Kwa kweli nyongeza hiyo ni kubwa katika historia ya mikopo ya chuo kikuu na tumeendelea kuongeza kutokana na maelekezo yake kwa sababu tulivyofika mwaka wa fedha 2022/2023 tulitumia bilioni 654. Mwaka ambao sasa hivi tunaenda nao tuna bilioni 731 na katika bajeti ijayo tutaona tena nyongeza ambayo tutaipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo pamoja na ukweli kwamba bado tunahitaji kuongeza, lakini jitihada iliyofanyika ni kubwa sana. Kwa kweli tumpongeze Rais wetu kwa sababu yeye binafsi ndiye aliyeona umuhimu wa suala hili la mikopo ya elimu ya juu. Si hivyo tu alikutana na viongozi wa wanafunzi wa vyuo vikuu, akawasikiliza hoja zao na kuwaongezea kitita ambacho wanakipata kwa ajili ya kujikimu siku hadi siku. Nyongeza hiyo siyo kwamba inaongeza idadi ya wanafunzi wanaopata mkopo tu, lakini inaongeza kiasi ambacho wanafunzi wanapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa tuliyonayo ni kuhakikisha kwamba hizi fedha bado tunazigawa kwa haki kwa kutumia vigezo vilivyo wazi vinavyotabirika ili mtu anapokosa mkopo anaweza kukata rufaa, hata ikifika kwa Waziri, kazi yetu ni kuangalia tu vigezo tulivyoviweka kama vimetumika sahihi au siyo sahihi. Bodi ya Mikopo bado ina maelekezo ya kuhakikisha kwamba inazidi kuwa *transparent* kwa kuweka vigezo wazi, kuvitumia inavyotakiwa na kuondoa aina yoyote ya upenyo wa mtu kumpenyeza mtu kupata mkopo ambaye hastahili ili angalau kama fedha hazitoshi, basi ziwafikie wale ambao wana mahitaji makubwa zaidi kuliko watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo tunaendelea kuwekea mkazo katika marejesho ya mikopo, kwa sababu huu ni mkopo. Waliopata ajira wana wajibu wa kurudisha fedha hizi kwa ajili ya kuhakikisha watu wengine zaidi wananufaika. Mkazo mkubwa unawekwa na mkakati maalum umeandaliwa na bodi ya mikopo kuhakikisha kwamba tunaongeza marejesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya hivyo, chini ya uongozi wa Rais wetu aliagiza na nakumbuka Bunge lako Tukufu lilipitisha kwamba tutoe *scholarship* kwa mara ya kwanza. Tangu tuanze *cost sharing* Serikali ilikuwa haitoi *scholarship* kwa *degree* ya kwanza, lakini Rais wetu alipoingia madarakani aliagiza kwamba sekta iandae *scholarship* kwa ajili ya wanafunzi ambayo hatimaye Bunge lilipitisha na sisi tumeita *Samia Scholarship,* ambayo inafanya vizuri zaidi na sasa hivi wanafunzi wengi wamenufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakumbuka bajeti hii tunayotekeleza tulipewa maelekezo kutoka Ofisi ya Rais kwamba Mheshimiwa Rais amesema anataka kuona mikopo inaongezwa kwa vyuo vya kati. Kwa hiyo tulianza kwa kutenga bilioni 48 kwa ajili ya wanafunzi wanaosoma vyuo vya kati ili nao waweze kujipatia mikopo na tumeanza ku-*administer* kwa kuangalia maeneo ya vipaumbele. Tutaendelea kuona utekelezaji wake unaenda vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa taarifa kwako na kwa Bunge lako Tukufu kwamba wapo wadau mbalimbali ambao wameiunga Serikali mkono na wengine wamekuja wamesema tunataka kumuunga mkono Rais wetu. Kwa mfano, *KCB Bank,* yenyewe imeamua kutoa *scholarship* kwa wanafunzi wanaosoma kwenye vyuo vya *VETA*. Wanatoa fedha kwa kila mwanafunzi 100%. Wametuambia kwamba wanafanya hivyo kwa sababu wanataka kuunga mkono jitihada za Rais wetu za kutoa mikopo na kuongeza *scholarship* kwa wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika *NBC Bank* nao wametoa kitita ambacho kinatoa ufadhili *(scholarship)* si mkopo kwa wanafunzi wanaosoma kwenye *VETA* ni kuwasaidia baada ya kusoma ili kuanzisha biashara ambazo zitawasaidia kujikimu katika maeneo hayo. Kama tulivyotangaza katika bajeti yetu wakati ule *NMB Bank* wametoa bilioni 200; lakini hii ni mikopo kwa watu ambao wana miamala inayopitia kwenye benki kwa ajili ya kusaidia watu kwa ajili ya masuala ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa wito kwa wadau wengine mbalimbali wajitokeze kuunga mkono juhudi hizi nzuri za Serikali na kumuunga mkono Rais wetu kwa ajili ya kusaidia vijana wetu kujenga uwezo wao wa kujisomea na kujiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa muda unaenda ningependa nizungumze suala lingine moja muhimu ambalo lilizungumzwa na Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza kuhusu kuangalia *school dropout*. Kwanza ningependa kutoa taarifa kwamba tunaimarisha sana takwimu za elimu sasa hivi.

Kwa mara ya kwanza sasa hivi ile inayoitwa *Basic Education statistics of Tanzania*, ile *basic* haitakuwa *basic* ya *education* tena itakuwa *basic statistics,* sasa hivi itakuwa inaanza elimu ya awali mpaka vyuo vikuu. Sasa hivi Tuna kazi kubwa inafanyika kushirikiana na TAMISEMI, *TCU, NACTVET* na taasisi nyingine zote na kuhakikisha kwamba wanafunzi wanaosoma shule binafsi ambazo zinatumia mitaala ya nje siyo mitaala ya ndani, nao tunawa-*capture*. Kwanza tujue wanafunzi wetu wanaosoma ni wangapi, wako wapi na umri wao ukoje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo tuna kazi kubwa ambayo tunafuatilia wanafunzi wote ambao waliacha shule kwa sababu mbalimbali. Leo timu yetu iko Geita kwenda kuangalia *re-entry programme* kwa wale wanafunzi waliopata ujauzito wakati wa kusoma, lakini tunaangalia na *boys* ambao wametoka shuleni…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, mengine utaleta kwa maandishi.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ashatu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba ya bajeti ya Ofisi yake ambayo ameiwasilisha, ambayo imetoa mwelekeo kwa Wizara nyingine zote ambazo tunakuja baada yake. Pia niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri chini ya Ofisi yake kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwenye hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao waligusa Wizara yetu ya Viwanda na Biashara. Naomba nikiri kwamba tumepokea mawazo yao, miongozo yao pamoja na ushauri wao na

tutakwenda kuifanyia kazi, tunapokuja na bajeti yetu ya Wizara ya Viwanda na Biashara tutayasema yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kwa sababu ya muda niruhusu niseme mawili tu. Nianze na suala la siku zote ambalo ni suala la Mradi wa Mchuchuma na Liganga. Mheshimiwa Yustina Rahhi aliuliza ni wapi tumefika kwenye utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya na hasa kwa kuonesha mwelekeo chanya kwenye utekelezaji wa Mradi huu wa Mchuchuma na Liganga. Mheshimiwa Rais alitupatia shilingi bilioni 15.42 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wetu 1,142 ambapo mpaka leo tayari tumeshalipa shilingi bilioni 15.38 kwa wananchi 1,129 na hakuna malalamiko yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshalipa 98.86% ya wafidiwa wote ambao walifanyiwa tathmini na wamebaki 13 tu. Hawa 13 hawajajitokeza na sisi kama Wizara tunaendelea kufanya kazi kwa karibu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Ludewa kuwatafuta hawa 13 ili tuweze kuhitimisha kuwalipa fidia yao na mradi wetu uweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishahitimisha ulipaji wa fidia ndipo sasa tunaweza kusema eneo hili ni la Serikali. Nimshukuru tena na kumpongeza tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miongozo yake anayoendelea kutupatia. Tayari tunafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Ardhi, ambapo sasa tunakwenda kutwaa lile eneo baada ya kuwa tumeshawalipa wananchi wetu wote kwenye hili eneo, ili sasa mwekezaji yeyote yule anayepatikana aweze kutekeleza mradi huu kwa kuwa eneo sasa ni la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majadiliano; kama nilivyosema Bunge la bajeti lililopita, tunaendelea kujadiliana na mwekezaji yule wa *Sichuan* kwa umakini mkubwa ili tusiliingize Taifa letu kwenye hasara yoyote kutokana na mikataba ambayo ilishasainiwa kabla. Kwa hiyo tunaendelea kushughulika pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Mambo

ya Nje ili tuwapate watu sahihi na tuhitimishe majadiliano na mwekezaji wa *Sichuan Hongda* na ardhi ile iweze kurejea mikononi mwetu na tuweze kupata mwekezaji mwingine atakayefanya kazi nzuri au yeye kama atarudi atakuwa amejipanga sawasawa, basi afanye kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili eneo la Mchuchuma na Liganga, naomba kusema maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo linaloshindaniwa ambalo tuko kwenye majadiliano ni asilimia 15 tu ya eneo kubwa la Mchuchuma na Liganga lenye madini. Hivyo, sisi kama Wizara kupitia miongozo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumeamua eneo lingine 85% lililobaki tumetangaza ili waje wawekezaji tufanye utafiti na tuweze kuchimba makaa ya mawe pamoja na chuma kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwaambia Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu taarifa njema kabisa, kwamba tayari tumepata wachimbaji ambao ni wazawa watano, tumeshasaini nao mikataba kwa ajili ya vitalu vidogo na wawili wameshakamilisha utafiti wa kijiolojia, wanaanza uchimbaji wa makaa ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeimba sana kuhusu Liganga na Mchuchuma na sasa Serikali imeamua kutekeleza mradi huu na tunakwenda kuutekeleza na wanaanza Watanzania wazawa wenyewe ambao wameshamaliza utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye hoja ya pili, napenda kuitolea ufafanuzi, nayo ilitolewa na Mheshimiwa Kunti Majala kuhusu mikakati ya kulinda wakulima wa alizeti ikiwa imepunguza tozo ya mafuta yanayotoka nje ya nchi ili kulinda wakulima wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliweka sawa jambo hili. Serikali haikupunguza kodi yoyote. Waheshimiwa Wabunge naomba niwakumbushe, mwezi Desemba, 2022, mwezi Januari, 2023 mpaka tulipofika mwezi Februari hali ya bei ya mafuta ilikuwa

ni ya juu sana ndani ya Taifa letu, ni kwa sababu tulifanya mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2021. Jambo hili lilipoonekana kwa dhamira njema ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema turudi pale tulipokuwa ili Watanzania wasiumie na bei kubwa ya mafuta ya kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, dhamira ya dhati ya Serikali yetu chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni njema sana na nimpongeze sana hasa uwekezaji wake kwenye kilimo. Anawekeza kwenye kilimo na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ametoka kusema hapa. Tunachotakiwa kukifanya ni wazalishaji wetu ambao ni wakulima wa mbegu za mafuta kuzalisha kwa ufanisi ili ziweze kuchakatwa kwenye viwanda vyetu ambapo kwa sasa viwanda vinazalisha kwa muda wa miezi miwili tu na mbegu zote zinakuwa zimekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiweza kuongeza ufanisi kwenye uzalishaji wa alizeti, nina uhakika hata bei yetu kwa wakulima itakuwa nzuri na bei ya mafuta nayo itakuwa nzuri, tutakuwa tunawalinda watu wetu wote…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante, mengine yajibu kwa maandishi.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Bashungwa, Mheshimiwa Dkt. Jafo na Mheshimiwa Profesa Kitila.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, nilikwishamtaja Mheshimiwa Bashungwa, wajiandae Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Profesa Kitila.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze na niungane na waliotangulia kuchangia na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri na bajeti nzuri ambayo imesheheni miradi na mambo mazuri kwa ustawi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika pongezi, nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Mheshimiwa Deo Ndejembi kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, bila kuwasahau Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Katambi na Mheshimiwa Ummy. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yao mizuri na ushauri ambao wametupatia na nitajikita kwenye hoja ya Ujenzi. Niwashukuru sana kwa maeneo ambayo wamechangia hususani yanayohusu Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamechangia Wabunge wasiopungua 37 hasa kwenye masuala ya barabara na madaraja na michango ya Waheshimiwa Wabunge inaonesha taswira ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi ambayo inakuja. Vilevile, inaonesha uhalisia kwa sababu Waheshimiwa Wabunge ni

wawakilishi wa wananchi na wote tunaona namna mvua za *El-Nino* zilivyonyesha nyingi kuliko namna ambavyo tumezoea kwenye historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mvua hizi zimeharibu miundombinu, hakuna barabara hata moja iwe ni ya *TANROAD* au *TARURA* ambayo haijaharibiwa na mvua za *El-Nino*. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge michango yao iko kwenye uhalisia na upande wa Serikali pamoja na wananchi, tunaona mvua hizi kubwa ambazo ziko nje ya uwezo wetu na uharibifu mkubwa wa miundombinu ambao zimeufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na changamoto hizi ameendelea kutuwezesha *TANROADS* na *TARURA* ili kuendelea kuweka jitihada za kurudisha mawasiliano pale yanapoharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais, katika Bunge hili; Bunge lililopita mwezi Februari, tulikuwa tumeomba bilioni 66, hivi ninavyozungumza Mheshimiwa Rais na Serikali ya Awamu ya Sita anayoiongoza, tayari ametupatia bilioni 66 ili kuendelea kupambana kurudisha mawasiliano katika maeneo mbalimbali ya nchi hii ambayo yamekatika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mvua za *El-Nino* zimeharibu miundombinu nchi nzima. Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea na kila aina ya jitihada ili kurudisha hali ya mawasiliano ya barabara za lami na zile za changarawe, naomba kuzungumzia mafanikio makubwa ambayo tulikuwa tumejipanga nayo na tunaendelea kuyafanya. Hata hivyo, kwa sababu mvua hizi zimebomoa madaraja na barabara, zipo changamoto lakini lazima tumtendee haki Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kumshukuru kwa barabara 25 ambazo zimekwishakamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Bunge la Bajeti linaendelea pia tuko kwenye maazimisho ya miaka mitatu toka Mheshimiwa

Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameingia madarakani. najivunia kuripoti kwenu kwamba, ndani ya miaka mitatu tumekamilisha ujenzi wa barabara 25 kwa kiwango cha lami, zenye urefu wa kilometa 1198.5. Vilevile, tumekamilisha madaraja makubwa nane, pia sasa hivi barabara 57 ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi ambazo mpaka kukamilika kwake tutakuwa tumejenga barabara zenye urefu wa kilometa 3,794. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada hizi yapo pia madaraja matano ambayo yako katika hatua mbalimbali za ujenzi, likiwemo Daraja la Kigongo – Busisi *(John Pombe Magufuli Bridge)* ambalo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati anaingia madarakani, ujenzi ulikuwa umefikia 25% na hivi sasa uko asilimia 85 na kazi inaendelea. Matarajio yetu, kufikia Desemba, 2024 daraja hili liwe limekamilika ili liendelee kutoa huduma kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, jitihada hizi na barabara hizi ambazo zimekamilika, barabara 57 ambazo tunaendelea kujenga na madaraja ambayo tunaendelea kujenga, mvua za *El-Nino* zimeharibu ujenzi huu pamoja na barabara ambazo zilikwishakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti ambayo Wizara ya Ujenzi tutaleta, tutaelezea kwa kina namna ambavyo tumejipanga. Kwa mfano, barabara 49 tayari tulikuwa tumekwishafika hatua ya kusaini pamoja na zile barabara 57 ambazo ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi. Barabara 30 tulikuwa tuko katika hatua za manunuzi kwa maana ya kupata wakandarasi. Vilevile, bila kusahau barabara ambazo ziko chini ya mikoa yetu (barabara za changarawe) ambazo kila mwaka tunatumia kiasi kisichopungua bilioni 550.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo tutakuwa tunaona jitihada hizi nzuri ambazo tayari tulikuwa tuko kwenye mwelekeo mzuri, lakini tukapata changamoto hii ya mvua za *El-Nino* ambazo zimenyesha kupita kiasi. Kwa hiyo, mpaka hivi sasa kwa tathmini ambayo tumefanya wakati wa Bunge la Mwezi Februari, tulifanya tathmini ya uharibifu wa miundombinu. Kipindi kile hasara ilikuwa

ni bilioni 200, mpaka kufikia jana miundombinu imeharibika na ili tuweze kuirudisha tunahitaji kiasi kisichopungua bilioni 500 (nusu trilioni).

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo bajeti ambayo ingekwenda kwenye miradi ambayo iko katika hatua za ujenzi wa kiwango cha lami, barabara ambazo tumesaini na barabara ambazo ziko kwenye manunuzi. Sasa hivi tutalazimika kukaa na kujipanga upya ili kuhakikisha Watanzania wanaendelea kuwa na mawasiliano ya hizi barabara ambazo zimeharibika huku tukiendelea na mkakati wa kudumu wa kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania, wote tunaona namna ambavyo miundombinu imeharibika, lakini ndani ya Serikali tunaendelea kujipanga kwa kadri inavyowezekana ili kuhakikisha miradi hii inaendelea. Vilevile, tukiwa tunafahamu kwamba tunaweza tukalazimika ku-*review* baadhi ya maeneo ili kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mkoa wa Lindi kuna kipindi Wilaya ya Nachingwea, Liwale pamoja na Ruangwa zilikuwa hazifikiki kwa njia ya barabara. Ililazimika kutafuta fedha za *emergence* ili kwenda kuhakikisha wilaya hizi zinapata mawasiliano na kuchelewa kwake utakuta bei ya vyakula inapanda, mafuta yanakosekana. Kwa hiyo, yapo masuala mengine ambayo hayawezi kusubiri kesho, lazima tuyafanye sasa hivi ikiwemo suala la barabara hizi ambazo zimeharibika. Pia, tunaendelea kutumia hela za dharura ili kurudisha mawasiliano yake…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bashungwa, ahsante kwa mchango mzuri na tathmini uliyoifanya…

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na tutaelezea kwa kina wakati wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Jafo, Mheshimiwa Profesa Kitila ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mola ambaye kwa mara nyingine ametuingiza katika Bunge hili la Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika sisi tunajivunia sana kuwa naye, kwa sababu yeye ni kama zile nyavu za wale ndugu zangu, watani zangu Wasukuma, nasema eneo analoongoza kama ni nyavu ni kokolo (ana mambo mengi). Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameendelea kuitendea haki Serikali ya Awamu ya Sita ili kuhakikisha majukumu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuwahudumia Watanzania yanaendelea vizuri. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa kweli dada tunamchosha sana. Hata hivyo, ameendelea kuwa imara akipamba katika eneo lake kama *Chief Whip,* lakini kuhakikisha mambo yote yanakwenda vizuri na naomba watu wa Peramiho wamwangalie kwa jicho la mara mbili, mbili. Vilevile, nimpongeze sana ndugu yangu Mheshimiwa Deo Ndejembi, kwa kupata fursa hii katika eneo hili jipya, kwa kweli hii ni fursa kubwa sana ambayo imani yangu na imani ya Watanzania ni kwamba, ataendelea kuhudumia na kumsaidia Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba eneo hilo la Kazi, Vijana na Watu Wenye Ulemavu linatendewa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Katambi, tunafahamiana vizuri sana tokea siku nyingi sana na

nafahamu weledi wake katika kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mungu ambariki sana. Vilevile, dada yangu na shemeji yangu Ummy, anaupiga mwingi bila kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya. Katika upande ninaouongoza, niliopewa dhamana ya kusimamia, Ofisi ya Makamu wa Rais, nimeona Mheshimiwa Rais anaitendea haki sana nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaja katika hoja ambayo Wabunge watatu wamezungumza, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu yeye ndiye amepewa dhamana ya kushughulikia sherehe za kitaifa. Jana tulikuwa kule Zanzibar na Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, maandalizi aliyoyafanya Mheshimiwa Waziri Mkuu yamekwenda vizuri sana. Pia, nina imani ya kutosha kwamba siku ya uzinduzi wa Kitabu cha Miaka 60 ya Muungano, tarehe 23, halikadhalika siku ya tarehe 26 ya kilele, Watanzania watashuhudia mambo makubwa ya Muungano wetu yaliyofanikiwa katika kipindi hiki, Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika hili kwa kweli namshukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Mawaziri waliokwenda katika vyombo vya habari kuzungumza mambo makubwa ambayo yamefanyika katika hii miaka 60, hakika kama Serikali uratibu wa Mheshimiwa Waziri Mkuu umetusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja zilizojitokeza katika upande wa biashara ya *carbon*. Ni kweli kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakumbuka mwaka 2022, tulianza kutengeneza Kanuni na Mwongozo wa Biashara ya *Carbon*. Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakumbuka kipindi kile alienda kule Katavi kutoa gawio kwa Halmashauri ya Katavi. Hata hivyo, kipindi kile tulikuwa hatuna kanuni wala mwongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maelekezo yake sasa tumepata kanuni na mwongozo. Naomba nimtoe mashaka ndugu yangu Mheshimiwa Justine Lazaro Nyamoga, kule wana misitu ya kupandwa kwa

kiwango kikubwa, lakini, tulizungumzia jinsi gani katika wataalam wa halmashauri wataweza kupata elimu. Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushirikiano na *UNEP*, tumeweka mpango kwa ajili ya kufanya *capacity building* kwa wataalam wetu wa mazingira katika halmashauri zote nchini. Kwa hiyo, katika hili ni imani yetu kwamba, tutaendelea kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika ndugu yangu Sebastian Simon Kapufi, alizungumzia jinsi gani hata Wabunge wanahitajika kupata uelewa wa kutosha. Katika *package* yetu, tunakwenda kugusa wote kwa lengo la kuhakikisha tunakuwa na uelewa wa pamoja kuhusu biashara ya *carbon*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunaanza mchakato huu, nchi yetu ndani ya kipindi hiki tayari imekwishasajili miradi 42. Katika miradi hiyo, Miradi 22 inahusisha Sekta ya Misitu, Miradi 13 inahusisha Sekta ya Nishati, Miradi minne ni Sekta ya *Agroforest* na Miradi miwili ya *Waste Management.* Katika hili naomba niwambie Watanzania kwamba hakika katika hiki kipindi kifupi, haya ni mafanikio makubwa sana. Kwa mfano, Halmashauri ya Katavi siyo muda mrefu watapata gawio lenye wastani kati ya shilingi bilioni 10 mpaka bilioni 14.7, kwa mwaka huu peke yake, haya ni mafanikio makubwa sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera kule kwa ndugu yangu Mheshimiwa Bashungwa, kule Karagwe, Kyerwa, Muleba na Bukoba, eneo hili zaidi ya bilioni 1.6, kupitia kampuni ya *KADERES* ambayo inakwenda kuwakilisha katika eneo la *agroforest*. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, hapa tumejipanga vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika siku za awali kwamba, siyo muda mrefu tumepata mafanikio haya makubwa, haya makampuni takribani 42 yote yatakapokuja kutekeleza ambayo kati yake makampuni 12 yameshapata *no objection,* yamepata fursa kwa ajili ya kwenda kutekeleza miradi hii ya *carbon* na mengine yako katika mchakato wa kupitia yale maandiko yao, imani yetu ni kwamba, eneo hilo litakuwa ni fursa

kubwa sana ya kupata mapato katika halmashauri, halikadhalika katika nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaombe Watanzania katika eneo hili kuhusu suala kubwa la utunzaji wa misitu. Leo hii tunapozungumza suala zima la mabadiliko ya tabianchi na hata tukiangalia hizi mvua zinazoendelea kunyesha, athari yake imekuwa ni kubwa. Katika hili ni meseji tosha kwamba, Watanzania tuna kila sababu ya kuhakikisha tunaizingatia ajenda ya mabadiliko ya tabianchi kwa kujitahidi sana katika utunzaji wa mazingira. Bila kufanya hivyo madhara yake yatakuwa makubwa sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba athari ya mabadiliko ya tabianchi ikiwemo mafuriko na mvua zisizotabirika ni kubwa, ndiyo maana leo hii tunaomba Mungu tu, kwa sababu kwa mujibu wa takwimu za Mamlaka yetu ya Hali ya Hewa, huenda kutakuwa na siku kumi za ziada za mvua kubwa, maana yake madhara yake yatakuwa makubwa sana. Sisi Ofisi ya Makamu wa Rais, tumewatuma wataalam wetu wa *NEMC* waende nchi nzima ili watupatie taarifa ya kutosha kuhusu mazingira hasa baada ya kujitokeza kwa hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwaombe Watanzania, kwa upande wetu wa mazingira, waliopo kwenye maeneo hatarishi, waweze kutoka kwenye maeneo hayo kwa sababu hili ni janga kama majanga mengine. Ni imani yetu kwamba, tutaendelea kutekeleza hilo kwa sababu suala la mazingira ni jukumu letu sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na maeneo machache tu kwa ajili ya biashara ya *carbon,* kubwa zaidi tumwombee sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, *that is my message*. Juzi nilikuwa nawaambia watu tulipokuwa tunaelekea katika siku ya Pasaka na Eid, kuna mtu mwingine familia yake alikuwa anapanga awanunulie Abaya “ile Abaya eeh?”

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo, Abaya.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siku zinaisha abaya haijapatikana. Wewe fikiria kama ni kawaida mtu kupata Abaya ya mama na nguo za mtoto inashindikana, je, kuongoza nchi ni jambo la mchezo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu anafanya kazi kubwa, ukiangalia hii *investment* anayoifanya katika Sekta ya Elimu haijawahi kutokea. Sekta ya Miundombinu *for the first time,* leo hii ndiyo tumepata athari ya miundombinu na ukiangalia kazi iliyokuwa imefanyika ni kubwa. Hili Watanzania walifahamu, japo miundombinu imeharibika, lakini Serikali ilikuwa imefanya kazi kubwa. Hili ni janga kama majanga mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunatolewa mfano, kwa mfano, katika suala la uwekezaji, tukiwa katika mikutano mbalimbali tunaambiwa; "Tanzania ni nchi ya mfano yenye kutengeneza Mradi wa *Green Energy* kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya *Standard Gauge*" haijawahi kutokea Barani Afrika. Zaidi ya kilometa 2,100 ni kazi kubwa na ni *investment* ya fedha nyingi, Watanzania lazima tumwombee Rais wetu, tusipofanya hivyo, tutapata dhambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwambie kazi aliyofanya Rais wetu imekuwa ni kazi ya mfano. Siyo Tanzania tu bali na nchi nyingine. Tuna kila sababu ya kumwombea sana Mheshimiwa Rais wetu kwa sababu na yeye ni binadamu, anataka maombi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba anaipeleka nchi yetu katika eneo salama zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyoona hii bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, sidhani kama leo hii mtu atashika shilingi, sina mashaka, nimeona bajeti imedadavua mambo mengi na sisi kazi yetu ni kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu, watu waje kushika shilingi katika maeneo yetu na siyo kwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu halali, hapumziki na anahangaika kwa ajili ya Watanzania na ame-*present* vizuri bajeti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani, tutashirikiana katika Bajeti ya Waziri Mkuu na imani kubwa kwa mtu aliyepewa dhamana na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, bajeti yake ipite kwa kishindo. Sisi Wazaramo tunasema hiki ndicho *kingilambago*. Waheshimiwa Wabunge, ndiyo tumeanza hapo, kwa hiyo, tuanze vizuri. Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania, ibariki bajeti hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Kitila wajiandae Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Kapinga.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ingekuwa Kanuni inaruhusu, tungekwenda moja kwa moja kupiga kura, hata hivyo, acha nichangie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naungana na wenzangu kumpongeza sana kiongozi wetu, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa bajeti yake nzuri sana na kwa jinsi anavyotusimamia. Nawashukuru na kuwapongeza Mawaziri wenzangu katika Ofisi yake kwa jinsi ambavyo wanatuongoza vizuri. Namshukuru sana dada yangu, Mheshimiwa Jenista Mhagama. Yeye ni zaidi ya kiongozi na ni mlezi, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia maeneo mawili tu ambayo yamejitokeza katika eneo langu. La kwanza, ni hoja kutoka kwa Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini ambaye alihoji na kutoa ushauri kuhusu Taarifa za Sensa. Ameuliza ni namna gani Serikali inatumia taarifa hizi kwenye mipango ya maendeleo ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima nikiri, ni kweli kwamba, Taarifa za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 imesheheni takwimu muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Taarifa ile inatupa muundo mzuri wa kuangalia aina ya watu ambao tunao kwa maana ya idadi ya watu. Tuna mifano mitano ambayo inaweza kusaidia, moja, ni 76% ya Watanzania, kwa mujibu wa taarifa hiyo, wapo chini ya miaka 35; 42.8% ya Watanzania wote wapo chini ya miaka 15; 19% ya Watanzania

wote hawa wana umri wa kwenda shule kwa maana ya miaka saba na kuendelea; na 65% ambayo ni theluthi mbili ya Watanzania wanaishi maeneo ya vijijini na ya mwisho katika muundo huo ni 36% ya kaya zote hapa Tanzania zinaongozwa na akinamama, yaani mama ndio mkuu wa kaya. Hii maana yake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuzingatia takwimu hizi ni lazima ichague vipaumbele kwa umakini na kipaumbele cha kwanza ni lazima uwekeze katika elimu kwa sababu Taifa lina idadi kubwa. Kimsingi Taifa letu ni Taifa la watoto na vijana, kwa hiyo, ni lazima uwekeze katika elimu na kwa sababu hiyo, sera zetu zimeweka kipaumbele katika elimu, katika afya na katika lishe kwa sababu, ni lazima hawa watoto na vijana waandaliwe vizuri. Kwa hiyo, ni lazima matumizi ya takwimu yatuelekeze huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa sera za Serikali ya Awamu ya Sita ni kukazania sana maendeleo vijijini kwa sababu, kwa takwimu hizi idadi kubwa ya wananchi wetu ipo kule. Ndio maana utaona kwa sasa sekta za kilimo zinapewa msukumo mpya na ndio sababu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo asubuhi ameeleza jinsi ambavyo bajeti imeongezeka. Pia ndio maana Sekta ya Mifugo na Uvuvi inapewa msukumo mkubwa, lakini ndio maana tunazungumzia habari ya miradi ya umeme vijijini ili kuhakikisha wananchi wetu wanapata unafuu wa maisha na hii sababu tunawekeza sana kwenye maendeleo ya miundombinu ya barabara vijijini kupitia *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yote hiyo inaonesha kwamba, tunazitumia takwimu hizi kwa ajili ya kuweka vipaumbele vyetu sawasawa. Nawaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba, katika Dira ya Maendeleo ambayo tunaiandaa, takwimu hizi zitatumika kikamilifu kwa ajili ya kutuelekeza kwa miaka 25 mingine ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita pia inaendelea kuwajengea uwezo wanawake kwa sababu, kwa takwimu ambazo nimezieleza hapa ile hoja ya zamani kwamba,

baba ni kichwa cha familia inaanza kupitwa na wakati. Kwa sasa baba na mama wote ni vichwa vya familia na katika kila familia 10 hapa Tanzania familia nne mama ndio kichwa cha familia. Kwa hiyo, maana yake ni lazima sera zetu zituelekeze kwenye eneo hilo. Hivyo, namhakikishia Mheshimiwa Mwakasaka na Wabunge wengine kwamba, Taarifa na Takwimu hizi za Sensa tutazitumia vizuri kwa ajili ya kupanga mipango yetu ya maendeleo ya muda mfupi na muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo napenda kuchangia ni hoja ya Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, ambaye alihoji na kushauri kuhusu umuhimu wa kuimarisha sekta ya uzalishaji viwandani. Kwa kweli, aliongea kwa uchungu sana kwamba, tunaagiza karibu kila kitu na hatuuzi sana nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kueleza, pamoja na changamoto zilizopo ukweli ni kwamba, mwelekeo wetu wa sera kwa sasa tunapozungumzia ukuaji wa Uchumi, tunataka uchumi wetu ukue, lakini uakisi mambo ya msingi manne. Moja, uchumi huu ukue na uwe jumuishi na siyo ukue kwa baadhi ya watu; Pili, uchochee ajira kwa vijana na akinamama; Tatu, uchumi wetu utuelekeze kwenye kupunguza umaskini; na Nne, tunataka uchumi wetu tuwekeze kwenye kuongeza mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi. Kwa hiyo, suala la *value addition* ni suala la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Mheshimiwa Hasunga ni ya msingi na tunaizingatia, ndio maana ukiangalia katika miaka mitatu iliyopita kuanzia mwaka 2021 hadi 2023, utaona kwamba, katika sekta ya uwekezaji miradi mingi ambayo tunaivutia ni katika sekta ya uzalishaji viwandani. Ukiangalia katika miaka hii mitatu tumekuwa na miradi 1,400, lakini miradi 456 ambayo ni 45% ni katika sekta ya uzalishaji viwandani. Kwa hiyo suala la uzalishaji viwandani tunalipa kipaumbele kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, siyo tu *data* za kwenye makaratasi bali hata ukienda kwenye uhalisia utaona. Nitoe mifano michache, Septemba, 2023 Mheshimiwa Rais amezindua

kiwanda kikubwa cha kampuni moja inayoitwa *Sapphire* pale Mkuranga. Hiki ni kiwanda ambacho kinatengeneza vioo vya kisasa vya ujenzi wa nyumba, *floating glass.* Kiwanda hiki kimewekeza pale takribani shilingi bilioni 832, kinaajiri vijana wa Kitanzania 1,600 na hiki ni kiwanda kikubwa kuliko vyote hapa Afrika Mashariki na ni kiwanda cha nne kwa ukubwa katika Afrika, viwanda viwili vipo *South Africa,* kimoja Nigeria na cha nne kipo Tanzania na 75% ya mazao yanayozalishwa pale yanauzwa nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie Mheshimiwa Hasunga na Waheshimiwa Wabunge kwamba, suala hili la kukazania uzalishaji wa viwandani, ni suala la kisera, lakini pia kiutekelezaji linakwenda vizuri. Kwa hiyo mwelekeo wetu unakwenda vizuri ndio maana ukisoma takwimu za Benki Kuu ya Tanzania za Mwezi Machi zinaonesha kwamba, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi zimeanza kuongezeka na zimeongezeka kwa 14.7%. Mwezi Februari mwaka huu, tupo Dola za Kimarekani bilioni 14.3 na zinakwenda zikiongezeka. Kweli tuna changamoto, lakini mwelekeo ni mzuri. Tunapojadili masuala haya tusiangalie tu umbali uliobaki katika kusafiri, pia tuangalie tumesafiri umbali mrefu kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda vizuri, kwa usimamizi wa sera hizo nasema mwelekeo wetu ni mzuri na tunaamini kwamba, mauzo ya bidhaa ambazo zimeongezwa thamani kutoka viwandani yataendelea kuimarika kwa sababu ndio sera yetu na katika miaka ijayo sekta hii itaendelea kutiliwa mkazo mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nichangie maeneo hayo mawili, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Simbachawene, ajiandae Mheshimiwa Kapinga.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo

anaendelea kuifanya. Pili, nampongeza msaidizi wake Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wote waliopo katika ofisi yake wakiongozwa na dada yetu shupavu, Malkia wa Nchi ya Ruvuma, Mama yetu Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na ndugu yangu, rafiki yangu, Mheshimiwa Deo Ndejembi. Kwa kweli, kazi nzuri inafanyika na sisi tunaendelea kuwaombea kwa Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu michango nane imeelekezwa katika Wizara yetu na hasa katika eneo la utumishi na pia katika eneo la Mfuko wa Kunusuru Umaskini *(TASAF)*. Katika hii michango nane, saba ilielekezwa moja kwa moja katika eneo la utumishi, lakini mmoja ambao ulichangiwa na dada yangu Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, uliekezwa katika eneo la *TASAF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine, naomba nianze kwa kuwashukuru sana wale wote ambao walitoa ushauri na sisi, kama Serikali, tumeuchukua ushauri wao na tutakwenda kuufanyia kazi. Katika watu waliotoa ushauri nawatambua wanne, akiwemo mjomba wetu Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate na wengine waliopata nafasi ya kuchangia Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge Neema Lugangira alitaka kujua Serikali ina mkakati gani katika kuhakikisha kwamba, inaendelea kutambua na kuwasajili watu wanaoishi katika kaya maskini wanaostahili kunufaika na Mradi wa *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge kwamba, Serikali imeendelea kufanya hivyo. Nataka nilikumbushe Bunge kwamba, katika Awamu ya Kwanza ya Utekelezaji wa Mradi wa *TASAF* utambuzi ulifanyika katika wilaya tatu ambazo ndiyo zilitekeleza mradi huu. Baada ya mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizojitokeza katika awamu ya kwanza, Serikali imeendelea kuboresha utaratibu wa utambuzi na sasa Wabunge wanaweza kushuhudia kwamba, katika awamu ya kwanza tuliweza kutambua watu kwa 70% ya makazi yao. Sasa hivi mradi

huu umefikia 100% ambapo vijiji vyote, mitaa yote na shehia zote zimeingizwa ndani ya mradi na mambo yanakwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya hali ya walengwa waliodumu kwenye mpango huu katika kipindi cha kwanza imefanyika kwa lengo la kuwabaini walengwa ambao wameimarika kiuchumi na kuwafanyia *graduation,* ikiwa ni katika utaratibu wa kuwaondoa ili wengine ambao wanatakiwa waingie nao tuwaingize katika kutimiza lengo la mapambano ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo pia, nataka nitambue mchango mzuri wa Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara ambaye, ushauri wake umelenga katika kuboresha mishahara ya watumishi wa vyuo vikuu ili kuendana na majukumu yao. Nalihakikishia Bunge lako pamoja na wananchi wanaotusikiliza kwamba, Serikali imeendelea kuboresha mishahara ya walimu wa vyuo vikuu pamoja na watumishi wengine kwa kadri ya uwezo wa Serikali kibajeti unavyoruhusu. Katika kufanya hivyo, taratibu za kimsingi na miongozo ya kiutumishi imeendelea kuwa ndio kiongozi mkuu katika kufanya uhakiki wa mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge Athuman Almas Maige naye ameomba Serikali iendelee kuboresha Sheria za Kazi ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na mazingira ya kufanyia kazi. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, pamoja na kazi nzuri ambayo imeendelea kufanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu, kazi ya kuendelea kuangalia mifumo na taratibu za Sheria ya Kazi, ili kuendana na taratibu za sasa, sisi kama Ofisi ya Rais, Utumishi tumeendelea nayo. Tunaangalia na kupitia miongozo na Sheria mbalimbali zilizopo za utumishi wa umma ili ziendane na matakwa ya Sheria ya Kazi na kuondoa vilio ambavyo vimekuwepo mara kwa mara kwa watumishi wetu hasa linapofika suala la kupandishwa madaraja na kuweka vizuri mambo ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Mbunge Nicholaus Ngassa ambaye ametumia nafasi yake

kuishauri Serikali iangalie mifumo mizuri ya uhamisho wa watumishi ili kuweka vipindi vizuri vya kushughulikia masuala ya utumishi. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kipindi maalum cha miaka mitatu kama kilivyowekwa kwa ajili ya watumishi wetu kimeendelea kuangaliwa, lakini Sheria hiyo ya miaka mitatu haimbani mwajiri kumhamisha mfanyakazi endapo mazingira yaliyopo yanakwamisha utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kushughulikia masuala ya kiutumishi kwa kupitia njia mbalimbali za kimtandao. Kwa sasa matatizo yote ya kiutumishi yamewekewa siku 30 yaweze kushughulikiwa na kukamilika ili kuondoa kero za watumishi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru mchango mzuri uliotolewa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ambaye ameikumbusha Serikali iendelee kuboresha maslahi ya watumishi wake, hasa katika Sekta ya Umma na Binafsi ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Hasunga kwamba, hii Serikali ni pana, lakini Ofisi ya Rais inayosimamia Sekta ya Umma imeendelea kuangalia maslahi ya watumishi na kuyawekea msisitizo mkubwa. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilipandisha kima cha chini cha mshahara hadi kufikia 23%. Watumishi wote waliongezewa mishahara kwa viwango tofauti kadri bajeti ilivyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuweka kumbukumbu sawasawa, mwezi Julai, 2022, Serikali ilihuisha Waraka wa Posho ya Kujikimu kwa Safari za Kazi za Ndani na Waraka wa Posho za Kufanya Kazi kwa Muda wa Ziada. Mpaka sasa tunapozungumza, kwa upande wa Taasisi za Umma, Serikali imeendelea kuidhinisha mipango ya motisha ili kuwawezesha Watumishi wa Umma katika Taasisi za Umma kuweza kujikimu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Anastazia Wambura ametaka kuona Serikali inaweka mikakati ya kupunguza uhaba wa walimu nchini, ili kuendana na mitaala mipya ya elimu. Serikali

imeendelea kufanya zoezi hilo na katika kutatua changamoto hiyo watumishi katika Sekta ya Umma wameendelea kuajiriwa na pia tumeendelea kuboresha mishahara yao ili iwe kama *motivation* kwa watumishi wetu wote Serikalini. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imeajiri walimu 10,505 ili kupunguza changamoto ya upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalihakikishia Bunge lako kwamba, kabla ya mwaka huu wa fedha kumalizika kazi hii itakuwa imekamilika. Katika mwaka ujao wa fedha ambapo bajeti yake tutaiwasilisha mbele yako hivi karibuni wiki hii, Serikali imetenga nafasi 10,590 za ajira mpya kwa ajili ya Kada ya Elimu ambayo nina hakika kwa asilimia kubwa inakwenda kutatua kero zilizo katika eneo hili hasa ya walimu, lakini pia katika maeneo mengine ndani ya ya halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na michango mizuri iliyosemwa, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge, hasa waliochangia katika eneo hilo la utumishi kwamba, Serikali itaendelea kuangalia masuala ya kiutumishi na pia Mheshimiwa Rais ameeleza nia yake ya dhati wakati alipokuwa analihutubia Bunge. Katika kipindi hiki cha miaka mitano Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba, maslahi ya Watumishi wa Umma yanaendelea kufanyiwa kazi katika kuyaboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya ambayo yalielezwa au yaliombwa na Waheshimiwa Wabunge, tuyatolee maelezo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kapinga, ajiandae Mheshimiwa Ummy Mwalimu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya chini ya Serikali ya Awamu ya Sita. Kipekee nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo ameisoma hapa wiki iliyopita na pia nampongeza kwa kazi kubwa anayofanya ya kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, dada yangu Jenista Mhagama na kaka yangu Deo Ndejembi pamoja na Waheshimiwa Naibu Mawaziri, kaka yangu Patrobas Katambi na dada yangu Ummy Nderiananga.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja na kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa dhati ya mioyo yetu kwa ushauri, maono na mapendekezo mbalimbali ambayo wamechangia katika Sekta yetu ya Nishati na hususani katika Sekta Ndogo tunazozisimamia za Umeme, Mafuta pamoja na Gesi. Tumepata jumla ya wachangiaji 13 na yamkini naweza nisijibu hoja moja baada ya nyingine, lakini nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, kila hoja ambayo imezungumzwa hapa tumeipokea kwa uzito wa kipekee sana na zile ambazo zinaweza kutekelezeka, tunapenda kuwahakikishia kwamba, tutazitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na nishati safi ya kupikia. Waheshimiwa Wabunge wameeleza umuhimu wa kupunguza bei ya nishati safi ya kupikia, hususani gesi ili kuwawezesha Watanzania wengi zaidi waweze kutumia nishati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha matumizi fanisi ya nishati safi ya kupikia na ili kuweza kuchagiza matumizi ya nishati safi ya kupikia ni lazima nishati hii iwe na sifa kuu nne. Moja, ni lazima ipatikane kwa urahisi; Pili, ni lazima matumizi yake yaweze kuwa rahisi; Tatu ni lazima iwe na unafuu wa bei; na Nne, ni lazima iwe nishati salama ambayo inalinda usalama wa watumiaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha masuala yote haya na hususan suala la unafuu wa bei, Serikali ya Awamu ya Sita imeshaanza kutekeleza mikakati mbalimbali kuhakikisha Watanzania wengi zaidi wanatumia nishati safi ya kupikia. Mojawapo ya mikakati hiyo ni kupunguza gharama za awali ambazo zinahusiana na kuanza matumizi ya nishati safi ya kupikia hususan vifaa pamoja na majiko ya gesi. Hii ni kwa sababu changamoto kubwa ilikuwa ni kwa wananchi kuanza kufanya

matumizi kwa sababu gharama za awali huwa ni kubwa kwenye kupata vifaa pamoja na majiko. Jambo hili tayari tumeshaliwekea mikakati mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, tumeshaanza kutoa ruzuku ya mitungi ya gesi kwa ajili ya watumiaji mbalimbali wa Tanzania. Pili, kupitia miradi tunayoitekeleza na wabia wetu wa maendeleo hususan Umoja wa Ulaya pamoja na Wakala wetu wa Nishati Vijijini tayari tumeanza kuwawezesha mawakala wanaouza gesi mijini na vijijini kwa kuwapa ruzuku ili gesi inayoenda kwa mtumiaji wa mwisho iweze kuwa na gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mradi tunaoutekeleza na Umoja wa Ulaya, wananchi wataweza kupata unafuu kwa 45% mpaka 60%. Vilevile, kupitia miradi ya Wakala wa Nishati Vijijini wananchi wataweza kupata unafuu kati ya 25% mpaka 30%. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwenye suala la kuanza matumizi ya nishati safi ya kupikia Serikali imejizatiti kupunguza gharama ili Watanzania wengi waanze matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunayo mikakati ikiwemo kuboresha upatikanaji wa malighafi na miundombinu ya uzalishaji, upokeaji, uhifadhi na usambazaji wa nishati safi ya kupikia. Tunafanya hivi kwa sababu tukiboresha upatikanaji wa malighafi na miundombinu nishati safi ya kupikia itakuwa na bei rahisi kwa sababu tutakuwa tume-*balance economic scale*. Pamoja na mikakati hiyo kwa sasa hivi tunafanyia kazi kuhuisha na kuoanisha sera, sheria, kanuni na miongozo wezeshi itakayofanikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni mikakati michache ambayo tunayo kuhakikisha kwa kadri ya maoni ya Mheshimiwa Rais ambaye ndio *champion* namba moja wa nishati safi ya kupikia, ikifikia 2033 Watanzania wengi wawe wanatumia nishati safi ya kupikia. Niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge *agenda* hii ya Mheshimiwa Rais ipo katika mikono salama sana ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili uweze kuzalisha tani moja ya mkaa unahitaji kuchoma magogo kati ya tani 10 mpaka 12. Ndio maana ni lazima tulinde mazingira yetu kwa wivu mkubwa sana na ndio maana ni lazima Waheshimiwa Wabunge na wananchi tuhamasishane kwenda kwenye nishati safi ya kupikia ili tuweze kutunza mazingira haya kwa manufaa yetu sisi na manufaa ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hoja hiyo Waheshimiwa Wabunge wamezungumza hapa kuhusiana na hoja ya kupeleka umeme kwenye vitongoji. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo tumefanya kwa ufanisi mkubwa sana Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini na mpaka leo hii tumebakisha vijiji 468 tu kati ya vijiji 12,318, ndiyo hivyo tutahakikisha vitongoji vyote ambavyo ni 31,532 visivyo na umeme vitapata umeme ndugu zangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitongoji hivi ni vingi, jumla ya vitongoji tulivyo navyo ni 64,359 na mpaka leo hii kwa kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita tumeweza kupeleka umeme kwenye vitongoji 32,827. Kwa hiyo, utekelezaji wa kupeleka umeme kwenye vitongoji unaendelea. Niwahakikishie kama Mheshimiwa Rais anavyosema, maendeleo ni hatua tutaenda hatua kwa hatua kuhakikisha umeme kwenye vitongoji unapelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ummy.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia kufika siku ya leo na kutujalia kumaliza salama Mwezi Mtukufu wa Ramadhan na kuipata Iddi vizuri na leo tuko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kubwa kwangu na kuendelea kuchapa kazi. Miaka mitatu ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan sote tunaona kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya, tunampongeza sana. Niendelee kuishukuru familia yangu ikiongozwa na mume wangu Rashidi pamoja na wanangu na wasaidizi wangu wote kwa kuendelea kunisaidia na kunipa utulivu ulioniwezesha kuendelea kufanya majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wanasema ni malikia na mimi ameendelea kuwa ni mlezi wangu. Watu wa Peramiho siku zote nimeendelea kuwaambia nawashukuru sana kwa tunu hii, waendelee kumtunza Mheshimiwa Waziri. Tunampongeza Mheshimiwa Waziri na tunamshukuru kwa malezi, kwa *mentorship* na kila kitu, Mwenyezi Mungu ambariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro, mabosi wangu kwa kuendelea kuniamini na kuniunga mkono, nawahakikishia tuko pamoja. Mimi ni mtoto wao, nitaendelea kuwa mnyenyekevu kwao. Wanawake wa mikoa mingine ukijumuisha na Zanzibar naendelea kuwaambia nitaendelea kuwa mnyenyekevu na kuwasaidia majukumu, lakini Jumuiya yetu ya UWT chini ya Mama Chatanda na Mama Shomari tunaendelea kuchapa kazi na tunaendelea kuwatia moyo tuendelee kufanya kazi, tusikatishwe tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti na kwa malezi mazuri. Kipekee namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza kwa kunipokea katika ofisi yake. Kwa kufanya kazi katika ofisi yake nimeendelea kupata malezi mazuri na miongozo ambayo imeendelea kunijenga kama kijana. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na tunawashukuru Wanaruangwa kwa imani kubwa kwake, lakini tunamshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Deo, kaka yangu na Mheshimiwa Patrobass na Makatibu Wakuu wetu wote, Dkt. Jim Yonazi, lakini na Naibu Katibu Mkuu Mutatembwa na Wakurugenzi wetu wote katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa na nzuri wanayoendelea kufanya. Niseme tu jambo hapa pia kwa Mheshimiwa Spika, dada yetu Dkt. Tulia tunampongeza sana kwa kazi kubwa na nzuri, ameendelea kuwa *role model* wa mabinti wengi, hata akinababa wameendelea kumwamini na kumuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakupongeza pia kwa miongozo yako na namna ambavyo umeendelea kutu-*lead*. Tunawapongeza pia watu wa Ilala kwa imani kubwa wanayoendelea kukuonesha. Sasa niendelee kuwapongeza na Waheshimiwa Wabunge wenzetu wote kwa ushauri, maoni na mapendekezo na Kamati zetu zote zile ambazo zimetupa maoni na ushauri, tumezingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye hoja za Waheshimiwa Wabunge. Niruhusu nianze na takwimu, kwa sasa dunia inakadiriwa kuwa na watu bilioni 7.9, kati ya hao watu milioni 39 wanaishi na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa mujibu wa *Global Trend on HIV,* huko unaweza kupata takwimu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina watu milioni 61, kati ya watu 61 watu milioni 1.5 wanakadiriwa kuishi na Virusi vya UKIMWI. Kwa hiyo, unaona katika janga hili bado tuna kazi ya kufanya. Tunamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu alituzindulia *Tanzania HIV and AIDS Impact Survey,* mwaka jana pale Morogoro ambayo ilitupa hali halisi na picha kwa sisi kama Tanzania tunaenda wapi kwenye mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye 95% tatu za mapambano dhini ya Virusi vya UKIMWI, kwa Tanzania 95% ya kwanza ya kuhakikisha watu wote wamejua hali, Tanzania tumefikia 82%. 95% ya pili ambapo watu hao wamejua hali zao na wameanza dawa, tumefikia 97%, ya watu ambao wanatumia dawa. Hapa

tuendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri. Tunaendelea kutoa dawa za *ARV* bure katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya. 95% ya tatu watu hawa sasa wawe wamefubaza Virusi vya UKIMWI, hapa tumefika 94%.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema nini kutokana na takwimu hizo? Utaona 95% ya kwanza ya watu wanaojua hali tuko 82% tunataka kufika 95%. Tunakubaliana na maoni ya Kamati na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wenzetu, tunaenda kufanya *programme* mbalimbali. Tunaenda kurejesha Kampeni ya Furaha Yangu ambayo mwanzo ilikuwa inafanyika chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na uliona imezaa matunda makubwa. Kwa hiyo, tunaenda kuirejesha Furaha Yangu awamu ya pili ili kuendelea kuwahamasisha wanaume kuendelea kujitokeza kupima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya kazi kubwa na nzuri kwenye eneo la vijana hasa mabinti. Takwimu zilituonesha vijana miaka wa 15 hadi 24 wanapata maambukizi mapya kila mara. Kwa hiyo, tukajielekeza tufanye kwa wasichana, kwa nini? 80% ya maambukizi hayo yalikuwa yanaenda kwa mabinti. Tukaamua kuanzisha *programme* kwa kushirikiana na wadau wetu. *Programme* ile inaitwa *Dreams* katika mikoa mitano, *programme* hiyo imeendelea kufanya vizuri. Tumepita na Waheshimiwa Wabunge kwenda maeneo mbalimbali tumeona namna ilivyofanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubaliana na Waheshimiwa Wabunge wenzetu kwamba, tunaenda kuiongeza wigo *programme* hii kutoka mikoa mitano ambayo iko sasa hadi kufikia mikoa 21. Kadri tutakavyoendelea kupata fedha tutaendelea kuiongeza *programme* hii. Nataka niwaambie vijana wa kiume na wenyewe tutaenda kuwajumuisha katika *programme* hii na ni kwa mara ya kwanza tutaenda kuwajumuisha kwa ukubwa vijana wa kiume, kwa sababu imeonekana tunawaacha nyuma, tuna-*focus* zaidi na wanawake. Kwa hiyo sasa hivi tutawajumuisha na vijana wa kiume kwenye *programme* mpya ambayo itaenda kwa jina la *Enabling Dreams. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie vijana hatuwalaumu kwenye maambukizi ya Virusi vya UKIMWI ila Serikali ya Awamu ya Sita ya Chama Cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunaenda kuchukua hatua kuwafanya washiriki katika miradi hii kama wadau wa kwanza na wanufaika wa kwanza. Sisi kama viongozi, tutawajengea uwezo washiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *programme* hizi tutaendelea na *programme* za kuwawezesha watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI katika maeneo ya kujikwamua kiuchumi. Tutashirikiana na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, liko Ofisi ya Waziri Mkuu. Hivi juzi Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko alizindua makubaliano kati ya *PPRA* na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwamba sasa twende kufungamanisha maeneo haya mawili ili manunuzi ya umma katika maeneo yetu mbalimbali 30% ya manunuzi hayo yaende kwa makundi ya vijana, wanawake, wazee na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kuwajengea uwezo ili watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI, waweze kupata fursa hii na waweze kunufaika. Nimesema kwenye *programme* hii ya vijana tutaendelea kuwajengea uwezo kwenye maeneo ya ujasiriamali. *Programme* hii hatutawaachia njiani, tumepokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kwa unyenyekevu mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafunzo ya ujasiriamali tutawapa *start up kits.* Kama mtu amesomea pengine ufundi cherehani anatoka na cherehani yake na ana mafunzo anajielewa na kila kitu na tutaendelea ku-*monitor.* Niseme Mfuko wa Udhamini na Udhibiti wa UKIMWI Tanzania *(ATF),* 10% ya fedha za Mfuko zinazotengwa zitaendelea kuwawezesha kiuchumi watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushauri na maoni yao ambayo kwa kweli yametusaidia kuimarisha eneo hili la mapambano dhidi ya VIRUSI vya UKIMWI. Tutaendelea kufanya kazi kwa ukaribu sana na wao ili tuendelee kupokea maoni kwa sababu janga hili

linahitaji *approach* mbalimbali za namna ya kwenda nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niseme kwamba mimi pamoja na Mheshimiwa Waziri wangu Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa unyenyekevu mkubwa, tunaendelea kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi zao na kwa kutuunga mkono na sisi tunasema tuko pamoja nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Katambi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa nafasi hii, lakini pia nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia afya njema sisi sote. Pili, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwa na imani nami ya kumsaidia katika kutekeleza majukumu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika masuala ya Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niwapongeze sana wasaidizi wa Mheshimiwa Rais ambao ni Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Isdor Mpango, Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais na kutusaidia sana sisi katika kutupa miongozo na maelekezo ambayo yanatusaidia kuweza kutekeleza Dira ya Maendeleo na Mpango wa Maendeleo. Pia kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kupitia ofisi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Tulia Akson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye yeye pia amekuwa akifanya kazi kwa weledi

mkubwa kuliongoza Bunge hili pamoja na wewe, lakini pia Katibu wa Bunge pamoja na uongozi wote wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie pia fursa hii kumshukuru sana kwa namna ya kipekee Mheshimiwa Waziri wangu Deogratius Ndejembi na kumpongeza pia kwa uteuzi wake kwa nafasi hii waliyoipata pamoja na Katibu Mkuu wangu kuhudumu katika Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba naye, tunaye Mheshimiwa Jenista Mhagama, amefanya kazi kubwa, *Chief Whip* tunakushukuru sana kwa miongozo na maelekezo yako. Sisi pamoja na Mheshimiwa Ummy kwa kweli tunanufaika kwa kufanya kazi nanyi za kumsaidia Mheshimiwa Rais, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru Wenyeviti wa Bunge, lakini pia wa Kamati za Bunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa hoja zao ambazo siku zote zimekuwa kiongozi pia kielelezo cha kutusaidia sisi katika kutekeleza majukumu ambayo yamekusudiwa na Serikali kuweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze moja kwa moja katika hoja ambazo zimezungumzwa au zilizoelezwa na kutolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kutusaidia sisi kutekeleza majukumu yetu. Kwa hoja ambazo zimeelezwa, kwanza nitambue Wabunge ambao wamechangia kwenye ofisi yetu, kwenye maeneo ambayo yametugusa, ni Wabunge zaidi ya 36 na kwa sababu ya muda, naomba uniruhusu kuzieleza hoja hizi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuunga mkono hoja ya Hotuba ya Waziri Mkuu pamoja na pendekezo hili la bajeti lililoko chini ya ofisi yake. Zaidi niseme maelezo yote, mapendekezo, ushauri na maoni yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge lakini pia na Kamati za Kudumu za Bunge, tunayachukua kwa ajili ya kwenda kuyafanyia kazi ili kuboresha jukumu hili la utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, lakini pia na Dira ya Maendeleo pamoja

na utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ili wananchi wetu katika makundi hayo ambayo tumepewa fursa ya kuwahudumia, tuhakikishe kwamba tunawahudumia ipasavyo, kwa kuhakikisha tuna mikakati na mipango endelevu ambayo itawasaidia katika kuwahudumia na kufikia azma ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo amejiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo ambalo naweza kujielekeza na kwa kueleza kwa ujumla ni kwamba, tumeyachukua maoni na mapendekezo. Lipo eneo la watu wenye ulemavu ambalo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mapenzi ya dhati aliyonayo kwa watu wenye ulemavu, alidhihirisha hilo alivyowaita Ikulu ya Chamwino tarehe 16 Machi, 2022 na akasema kwamba; "Leo sina jambo lolote zaidi ya kuwasikiliza na mnieleze changamoto zote zinazowakabili, ziwe za kisera, kisheria, au changamoto zozote," ambazo yeye kama Mkuu wa Nchi alitaka kuzipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais aliwasikiliza lakini pia akatoa maagizo mahususi kwamba twende kutekeleza. Mbali na mambo mengine ambayo aliyasikiliza, mojawapo ilikuwa ni changamoto ya mafunzo ya watu wenye ulemavu ambayo Waheshimiwa Wabunge wameeleza kama moja ya changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo taarifa kueleza kwa furaha kabisa kwamba Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mapenzi ya dhati aliyonayo alitoa fedha zaidi ya shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ukarabati wa vyuo ambavyo zaidi ya miaka kumi vilikuwa havifanyi kazi. Kikiwemo Chuo cha Masiwani Tanga, Sabasaba pale Singida, Lwanzari Tabora na Mtapika kule Masasi Mtwara ambapo tayari vimeshakarabatiwa na vinafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Chuo cha Yombo pale Dar es Salaam vinafanya kazi kwa ajili ya kutoa elimu kwa watu wenye ulemavu ya utengemao na kuhakikisha kwamba hawabaki mitaani bila kupatiwa elimu ili na wao waweze kujitegemea na kuchangia kwenye ujenzi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais pia alitoa fedha nyingine zaidi ya shilingi bilioni 3.4 kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vipya vya watu wenye ulemavu. Hayo ndiyo majibu ya hoja ya Waheshimiwa Wabunge waliyosema kwamba watu wenye ulemavu waangaliwe, sasa hizo ndiyo hatua ambazo Mheshimiwa Rais alizichukua kwa kutoa zaidi ya shilingi bilioni 3.4 ambazo tumejenga na tunaendelea na ujenzi wa chuo pale Ruvuma kwa Dkt. Mama Mheshimiwa Jenista Mhagama. Tumesema Dkt ni sahihi, tumwombee kwa Mwenyezi Mungu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia chuo kingine kinajengwa pale Mwanza ambacho ni mbadala wa Chuo kile tulichokuwa nacho cha Milongo. Tuna chuo kingine ambacho tunakijenga Kasulu - Kigoma kwa Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako ambapo tayari ujenzi unaendelea na hali ni nzuri. Tunajenga Chuo kingine cha Watu Wenye Ulemavu kule Songwe. Lengo la Dkt. Samia Suluhu Hassan ni nini? Lengo ni kuhakikisha watu wenye ulemavu pia tunawajumuisha katika ujenzi wa uchumi wa Taifa hili, tunahakikisha watu wenye ulemavu hawawi barabarani tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akasema asilimia mbili za mapato ghafi ya halmashauri nazo ziende kwa watu wenye ulemavu, zaidi ya asilimia mbili za fedha hizi sasa zinakusanywa, zitatolewa kwa watu wenye ulemavu ili waweze kunufaika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa tena fedha shilingi 1,000,000,000, tumefungua akaunti maalum *BOT* kwa ajili ya ruzuku ya watu wenye ulemavu ambapo watapata vifaa saidizi vya kuwasaidia na pia vifaatiba, zaidi ya hapo hata kuwasaidia kwenye masuala ya elimu na changamoto walizonazo. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa fedha *cash* na sasa hivi tunasubiri shirikisho la vyama vya watu wenye ulemavu na vikao vinavyohusika viweze kuvipangia matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye eneo la watu wenye ulemavu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mapenzi ya

dhati ameendelea kuangalia katika maeneo ya ajira, tumetunga mwongozo ambao ameuidhinisha na ametoa ruhusa hiyo kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, tayari asilimia tatu ya ajira zote zinazotoka nchini iwe kwa watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, kama ni watu 20 lazima angalau watu wawili au zaidi waweze kupata nafasi hiyo kulingana na masharti na vigezo ambavyo tumeviweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika eneo hilo la watu wenye ulemavu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amezidi kuwatendea haki. Tumeenda kwenye miongozo ya ujenzi wote unaofanyika nchini uzingatie mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu. Ukijenga ghorofa lako lazima uzingatie kuna *lift* au kuwe na *ramp* ambayo itawasaidia watu wenye ulemavu ili kuweza kupata huduma katika sehemu wanayohitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ameendelea kuupiga mwingi Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa watu wenye ulemavu, yeye mwenyewe kwa kujua kwamba walikuwa hawana ofisi ya kitaifa ya kupata huduma, alitoa fedha zake mwenyewe zaidi ya shilingi milioni 36.7 kwa ajili ya kupata eneo la ujenzi wa Ofisi ya Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu, ninavyozungumza tayari hati hiyo wameshakabidhiwa watu wenye ulemavu na wanaendelea kwenye hatua ya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la watu wenye ulemavu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya mengi, pamoja na kuhakikisha kwamba hata kwenye zile kandarasi ambazo zinatolewa kwenye halmashauri na wao waweze kupewa *share* yao. Tunaendelea kuwaunganisha hata mikopo iliyokuwa ikitoka kwa kikundi cha watu watano, tumebadilisha mwongozo mwaka 2022 na sasa mtu mmoja mmoja mwenye ulemavu anaweza kupata mkopo wa shilingi milioni 10 mpaka shilingi milioni 50. Huyo ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuwa shahidi pamoja na Waheshimiwa Wabunge, watu wenye ulemavu sasa hivi wamepungua barabarani. Tulikuwa na kesi nyingi za ombaomba

na tulikuwa na kesi nyingi za watu wenye ulemavu kudhalilishwa. Sasa hivi mtu mwenye ulemavu ukimkuta barabarani ni amechagua mwenyewe kwa sababu sikio la kufa wakati mwingine halisikii dawa, lakini kwa sehemu kubwa tayari watu wenye ulemavu tumewaweka kwenye utaratibu wa kupewa nafasi hizi, hata maeneo ambayo yanafanyika ujenzi wa masoko tunawapa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Sekta ya Afya pia hata kwenye huduma zinazotolewa hospitali, watu wenye ulemavu wamepewa kipaumbele pamoja na wajawazito, watoto na wazee katika kupewa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amejipambanua kuwa rafiki mzuri na mwema kabisa kwa watu wenye ulemavu, tuendelee kumwombea Mwenyezi Mungu, aendelee kudumu ili watu wenye ulemavu waendelee kupata manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliona hatua nyingine ya kuhakikisha tunapunguza ulemavu, kwa sababu wapo wanaozaliwa na ulemavu na wapo ambao wanaupata baada ya kuzaliwa. Tumeweka utaratibu na mikataba ya lishe imesainiwa kupitia Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ili wahakikishe kunakuwa na lishe bora, imekuwa ajenda ya kudumu kwenye Mwenge wa Uhuru ili kuhakikisha watu wakizaliwa wasiwe na ulemavu, hata wale ambao wanapata madhila yanayotokana na kazi katika maeneo mbalimbali na kupata ajali, ameweka Mfuko wa *WCF* wa fidia kwa mfanyakazi ili kuweza kuhakikisha wanapata huduma pale ambapo wanaweza kupata madhila yanayowapelekea kwenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo lingine ambalo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya vizuri, kupitia Bunge lako Tukufu, ameendelea kutengeneza utaratibu mzuri wa kufanya kaguzi kwenye maeneo ya kazi kupitia Wakala wa Kazi *(OSHA)* ili kuhakikisha tunapunguza madhila, tunakuwa na kazi za staha na ajali ambazo zinatokea kwenye viwanda

zinazosababisha ulemavu wa kudumu na vifo zinafanyika. Amewezesha OSHA kwanza kwa kupunguza tozo na kuwawezesha, amewapa magari zaidi ya 13 ili waweze kufanya kaguzi kwenye viwanda kwa lengo la kupunguza ulemavu na ajali ambazo zinatokana na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la maendeleo ya vijana, zipo fedha ambazo zinatolewa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana za *SDL* ambapo katika fedha ambazo tumekuwa tukipata ni zaidi ya shilingi bilioni moja. Waheshimiwa Wabunge wamechangia hapa fedha hizo zipatikane, ni kweli tunaendelea na mazungumzo na Serikali na ahadi iliyopo ya Serikali kwa sasa kupitia Wizara ya Fedha ni kwamba, fedha hizi watatupatia, tayari hatua ya awali tumekwishakopesha zaidi ya shilingi bilioni 1.7 ambazo zimeenda kwa vijana kama *revolving fund*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaenda kwenye hatua nyingine, katika mikopo hii ambayo imetolewa, miradi zaidi ya 56 ya vijana ilitolewa fedha kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na tayari vijana wanufaika ni 392, walioweza kuunda makampuni kwa ajili ya kuweza kutumia fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia yapo mafunzo ya kukuza ujuzi ambayo fedha hizi za *SDL* zimekuwa zikisaidia. Pamoja na watumishi wapo vijana ambao wanafanya programu ya uanagenzi, tuliweza kupeleka vijana zaidi ya 9,593 katika mafunzo. mwaka huu wa fedha 2023/2024 ambapo tunaelekea mwaka wa fedha 2024/2025, tayari vijana 6,000 ninavyozungumza wako katika vyuo mbalimbali kwa ajili ya kupata mafunzo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya ajira ndani na nje ya nchi; katika kuzingatia hilo na maagizo mahsusi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na katika utekelezaji wake kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tumekwishaanza kuingia mikataba na nchi mbalimbali za ughaibuni ikiwemo Saud Arabia na Falme za Kiarabu. Tumekwishaingia *memorandum of understanding* na tayari tumeshaanza kupeleka wafanyakazi kule,

*lot* ya kwanza tulikuwa tumepata nafasi ya vijana 300 lakini walioenda ni zaidi ya 276. Tutaendelea pia kwenye nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshakaa na Nchi ya Austria tukafanya makubaliano. Kwa sasa tutaendelea kufungua maeneo haya ikiwa ni pamoja na kusajili mawakala wa ajira za nje ya nchi ili nchi yetu iweze kufunguka na tuweze kupata *remittance* ya fedha ambazo zinakuja ndani ya nchi ili kuongeza pato la Taifa kwa ajili ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado pia katika eneo hilo la ajira tupo kwenye kutekeleza maagizo mahsusi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Wizara zote za kisekta zimeelekezwa mahsusi ziweze kila mwaka kwa fedha zinazopewa zizalishe ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja. Kwa kufanya hivyo tayari baadhi ya Wizara zimekwishaanza kutekeleza agizo hilo ikiwemo Wizara ya Mifugo ambapo wana *BBT Life,* ambapo wajibu wao ni kunenepesha mifugo, Mheshimiwa Ulega anafahamu na ameshafanya kazi hiyo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Katambi, kengele ya pili hiyo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kuwakopesha hawa vijana, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Madini na Wizara nyingine tunategemea kwamba zitafungua fursa zaidi kwa ajili ya kuongeza wigo wa ajira ikiwemo miradi mikubwa ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aliyoyafanya Dkt. Samia Suluhu Hassan ni mengi, muda hautoshi, lakini naendelea kusema kwamba mchango wangu uweze kuingia katika kumbukumbu, naunga mkono hoja, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya makubwa na ndiyo maana maneno yanakuwa mengi kwa sababu mti wenye matunda ndiyo unaopigwa mawe.

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan achape kazi, tupo pamoja naye, maneno siyo kazi, kazi ni vitendo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Sasa namwita Mheshimiwa Ndejembi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mimi leo ndiyo mara yangu ya kwanza kusimama na kuzungumza mbele ya Bunge lako hili Tukufu tangu kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, napenda kutumia nafasi hii mbele ya Bunge lako kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka zake na afya njema ambayo anatujalia sote na kuweza kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kubwa aliyoionesha kwangu na kunipandisha kutoka kuwa Naibu Waziri ambapo aliniteua kuwa Naibu Waziri katika Ofisi mbili tofauti, Ofisi ya Rais, Utumishi na Naibu Waziri katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI, sasa amenipandisha kumsaidia kazi kama Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee namuahidi Mheshimiwa Rais, wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wabunge wote hapa ndani kwamba nitajitahidi kadri ya uwezo wangu na alivyonijaalia Mungu kuhakikisha najituma kuweza kufikia malengo ambayo yanategemewa kutoka kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, nawaahidi

kwamba miongozo yao na maelekezo yao tutayasimamia na kuyatekeleza kama vile ambavyo wanatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee natumia nafasi hii vilevile kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mabunge yote Duniani *IPU*, Rais wa 31, vilevile kwa kuliongoza Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa viwango vya hali ya juu. Aidha, nakupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee vilevile natumia nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati. Bahati nzuri Mwenyekiti wa Kamati hii ni Mbunge mwenzangu kutoka Wilaya ya Chamwino ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dodoma, Mama yangu Fatma Toufiq. Nakuahidi Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati na Wabunge wote kuwapa ushirikiano wa hali ya juu na pia maoni yenu, miongozo yenu na ushauri wenu tutauzingatia katika utekelezaji wa majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi hii ambayo naihudumu kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu chini ya Waziri Mkuu ni ofisi ambayo inafanya kazi kwa utatu kwa maana ya Serikali, Waajiri na Wafanyakazi. Natumia fursa hii mbele ya Bunge lako Tukufu kuwaahidi Muungano wa Waajiri *(ATE)*, vilevile Vyama vya Wafanyakazi kupitia Shirikisho lao la *TUTCA* kwamba tutakuwa pamoja, tutashirikiana katika kuhakikisha utatu wetu unafanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijikite kwenye hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge katika michango yao waliyokuwa wanachangia kwenye bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza ni suala ambalo ametoka kumalizia hapa Mheshimiwa Naibu Waziri, suala la ajira, kutafuta fursa za ajira kwa Watanzania. Nawaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba katika

hili tutafanya kazi usiku na mchana kwa ajili ya kumsaidia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kutafuta fursa mbalimbali ambazo zinaweza zikapatikana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari ofisi hii imeshaingia makubaliano na Serikali ya Saudi Arabia na Serikali ya *UAE* katika kuhakikisha Watanzania wanapata fursa mbalimbali, *skilled* na *unskilled labor* katika nchi hizi, vilevile tunaendelea kutafuta fursa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tumeona Serikali ya Japan imetangaza ajira zaidi 12,900 kwa wageni hasa wanaotokea Afrika. Tutahakikisha tunafanya kazi usiku na mchana kuweza kupata fursa hizo kwa ajili ya Watanzania kwenda kufanya kazi katika mataifa hayo. Tumeshuhudia South Korea ikitangaza ajira mbalimbali kwa ajili ya wageni, tutahakikisha tuna *tap-in* katika ajira hizo ambazo zimetangazwa ili vijana wetu wa Kitanzania waweze kufanya kazi zote za *skilled* na *unskilled*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Ofisi yetu hii ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, kazi yetu kubwa ni kuhakikisha tunaratibu fursa mbalimbali zinazotolewa na Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa vijana na watu wenye ulemavu, nawaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba tutafanya kazi kwa karibu sana pamoja na wenzetu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhakikihsa *4:4:2* zile fursa ambazo zipo kwa vijana basi zinawafikia na vijana wanaanzisha biashara ambazo zina tija. Tumezoea kuona zile *4:4:2* saa nyingine kila mmoja anakimbilia kwenye *trend* iliyokuwepo pale wakati huo, hawaangalii fursa nyingine zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, unakuta vijana wa Kagera kule kwa Mheshimiwa Bashungwa, wote wanakimbilia kuwa na bodaboda ilihali ukienda kilomita chache unaweza kukuta kuna Ziwa pale. Tunaweza kuangalia ni namna gani ile *4:4:2* inawasaidia kwa ajili ya kwenda kuwa wavuvi na kuzalisha katika maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta katika maeneo kama ile Mikoa ya *big five,* vijana wote wanatafuta fursa za mikopo za kwenda kuendesha bodaboda wakati kuna fursa katika mashamba, wana uhakika wa mvua. Serikali hii kupitia Wizara ya Kilimo imejitahidi katika kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima katika maeneo hayo. Tutakwenda kuratibu ili fursa hizi ziweze kuwafikia vijana kulingana na maeneo ambayo wanatoka ili ile *4:4:2* iweze kuleta tija na ikaonekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nafasi kubwa ya kuweza kunyanyua *entrepreneurs* kwenda kuwa mamilionea kutokana na fursa mbalimbali ambazo zinatolewa na fedha za Serikali hii ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ukiacha fedha hizi za *4:4:2* vilevile tumeona wenzetu wa Wizara ya Kilimo wakija na *BBT*. Tutahakikisha tunatoa fursa nyingi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kwa vijana wengi zaidi kuweza kuingia katika *BBT* ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni nimekuwa nikizungumza na Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, wanaenda kuanzisha *MBT*, *Mining for a Brighter Tomorrow*, ambayo tutahakikisha vilevile tunaratibu vijana wengi zaidi waweze kwenda kwenye fursa hizo. Hizo ndizo kazi ambazo zinaenda kufanywa na Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuhakikisha fursa hizi zinawafikia vijana wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hapa Waheshimiwa Wabunge walichangia kuhusu Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii. Kuna changamoto kubwa ambayo ipo, unakuta michango hukatwa kwa mwajiriwa lakini haifiki katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mwajiriwa pale anapokuwa amestaafu ama ameacha kazi anakwenda kwenye ile Mifuko ya Hifadhi ya Jamii anakuta asilimia yake aliyokatwa yeye ile 10% ilifika, lakini asilimia ya mwajiri haikufika, saa nyingine unakuta zote mbili zile 20% hazijakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nasema mbele ya Bunge lako Tukufu, tutakuwa wakali kwa waajiri wote ambao hawatapeleka

michango ya pensheni kwenye Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii. Ile ambayo inatakiwa kwenda *NSSF* na ile ambayo inatakiwa kwenda *PSSSF* ambayo inatoka kwenye halmashauri zetu na kadhalika, tutahakikisha waajiri wote wanapeleka michango ili wale Watanzania ambao wanafanya kazi waweze kupata fedha yao kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii kuwahakikishia kwamba hoja zote ambazo zimetolewa hapa tumezichukua, tumezipokea na tunakwenda kuzifanyia kazi. Majibu tutaleta kwa niaba ya Mheshimiwa Spika kwenye Kamati yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Fatma Toufiq juu ya yale yote ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge hapa na namna gani ambavyo tunakwenda kuyafanyia kazi. Nawaahidi ushirikiano wa hali ya juu Waheshimiwa Wabunge wote na Ofisi yetu na sisi ambao tunamsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu tutahakikisha yale malengo ambayo ameyaweka na yale atakayokuja kutuelekeza tunayatekeleza kwa haraka zaidi na kwa ushirikiano mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii vilevile kumshukuru sana Mheshimiwa *Chief Whip* Jenista Joachim Mhagama, Mbunge wa Peramiho kwa ushauri wake. Nimepata bahati ya kuhudumu kama Naibu Waziri wake. Nina imani yale aliyonilea na kunifundisha, ndiyo ambayo yamenisaidia kuweza kufika hapa nilipofika leo. Kwa hiyo namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, kwa ushirikiano mkubwa ambao ameendelea kunipa na hata sasa bado ananipa *on the job training* huku tunaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote, Waheshimiwa Naibu Mawaziri wote akiwemo Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Katambi na Mbunge wa Shinyanga Mjini, kwa ushirikiano na ukaribisho ambao amenipatia kwa muda ambao nimeripoti katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, mwisho kabisa na si kwa umuhimu, nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Chamwino kwa imani yao kubwa ambayo wanayo kwangu. Mpaka sasa, Jimbo liko salama, liko shwari na naendelea kufanya kazi kwa sababu wamenipa utulivu huo. Kwa hiyo nawashukuru sana Wanachamwino na nawaahidi nitaendelea kuwatumikia kadri ya vile ambavyo Mungu atanijaalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba kusema kwamba naunga mkono hoja iliyo mezani ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba kuwasilisha na Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndejembi. Sasa namwita Mheshimiwa Jenista Mhagama. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwanza kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliyetujalia kuifikia siku hii ya leo tunapokwenda kuhitimisha hoja yetu, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu. Vilevile nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Spika kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuliongoza Bunge letu Tukufu, tunampongeza sana sana Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Tulia Ackson. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru sana na wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika. Wewe kwa kweli ni Naibu Spika wa viwango vya hali ya juu. Kwa hiyo tunakushukuru sana na tunakupongeza na hata leo umekalia Kiti tunapokwenda kuhitimisha hoja yetu, tunakuombea kila la heri katika majukumu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na viongozi Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuwashukuru Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa wale wapya tunawapongeza kwa kuchaguliwa, lakini vilevile tunawapongeza kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuongoza Bunge hili na tunawashukuru sana kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tutakuwa hatujatenda haki kama mimi na wenzangu wenye hoja, hatutawashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge zilizojadili Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Joseph Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wote kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nampongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Nyongo kwa kazi nzuri aliyoifanya pamoja na Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wengine wote. Vilevile naomba kumshukuru aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, ndugu yangu Mheshimiwa Sillo ambaye sasa ameteuliwa kuwa Naibu Waziri na kwa kweli tulifanya kazi nzuri sana. Kwa Mheshimiwa Sillo tulikwenda kupeleka Mfuko wa Bunge. Mwenyekiti wa wakati ule Mheshimiwa Sillo, alisimamia sana kuhakikisha tunaelewana vizuri kwenye Mfuko wa Bunge. Kwa hiyo namshukuru sana sana Mheshimiwa Sillo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi na shukrani za dhati sasa kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa sana na kutoa maoni kwenye Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba kuungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu, mara nyingi, kipindi hiki amekuwa akitoa pole kwa wananchi ambao wamepata maafa na hasa katika kipindi hiki ambacho Taifa letu limekumbana na mvua kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kuwapa pole na naendelea kusema Ofisi ya Waziri Mkuu, chini ya uratibu wa Waziri Mkuu, lakini na maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tutajitahidi kila tunaloweza kuhakikisha tunawafikia wale wote waliopata madhara haya. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutoa taarifa za mafuriko na majanga mengine kutoka kwenye maeneo yao. Ofisi ya Waziri Mkuu iko wazi, nawakaribisha sana watuletee taarifa ili tuweze kuwahudumia Watanzania vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya pekee, namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini kuhudumu ndani ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba kusema kwa unyeyekevu mkubwa, nitaendelea kuyatekeleza majukumu haya kadri ya Mwenyezi Mungu atakavyotusaidia. Nampongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Mpango kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Dkt. Mwinyi kwa kazi nzuri anayoifanya na hasa katika kuwatumikia Wazanzibari. Naomba sasa kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndugu yetu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. Kwa kweli namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nimehudumu katika Ofisi yake kwa kipindi cha muda kadhaa, lakini amekuwa ni kiongozi na mlezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema namshukuru sana na ahsante sana kwa Wanaruangwa kwa kumchagua Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu kuwa Mbunge. Baada ya kuwa Mbunge, Mheshimiwa Rais amemwamini kuwa Waziri Mkuu na kwa kweli anatusaidia. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii pia, kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Dkt. Doto Biteko kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais. Naomba pia kumshukuru sana, toka ameingia kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, akiwa msaidizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, tumeanza kuonja karama za uongozi kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika Ofisi imeongezewa nguvu na Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko ameendelea kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sisi Waheshimiwa Mawaziri ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, pia tumeendelea kukaa na Mheshimiwa Dkt. Doto akitusaidia sana kutuelekeza jinsi ya kutekeleza majukumu yetu sawasawa. Kwa hiyo naomba kumshukuru na nampongeza

sana Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani za pekee ziende kwa Mheshimiwa Hamza, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, tulikuwa naye hapa asubuhi, kwa ushirikiano. Namshukuru sana sana na sasa hivi yuko hapa ndani, Mheshimiwa pacha Waziri Hamza tuko pamoja. Tutaendelea kudumisha Muungano na tutaendelea kuyasimamia majukumu yetu kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pacha wangu mwingine mpya, Mheshimiwa Deo, karibu sana Ofisi ya Waziri Mkuu naomba kumhakikishia ushirikiano. Namfahamu sana Mheshimiwa Deo, tumefanya naye kazi nikiwa Waziri wake Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Naomba kusema Wizara pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na dada yangu Mheshimiwa Joyce Ndalichako ambaye nimefanya naye kazi, namshukuru sana sana kwa kufanya naye kazi vizuri kipindi hicho ambacho alikuwa ameaminiwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwaambia wafanyakazi kwenye Ofisi hiyo ya Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, mdogo wangu Mheshimiwa Deo mmempata jembe la kutosha ambaye anakuja kuongeza kasi na nguvu katika shughuli zile zilizoanzwa na mtangulizi wake na naamini kabisa atakimbia na atamsaidia Mheshimiwa Rais. Karibu sana Mheshimiwa Deo na niko tayari kwa ushirikiano wa kutosha pamoja naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Ummy Nderiananga, hakika nimepata Naibu Waziri mwenye karama za kutosha. Wanawake wa Kilimanjaro hawakukosea kumchagua. Anafanya kazi kwelikweli, ananisaidia sana, hachoki na yuko mstari wa mbele kabisa. namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tuendelee kushirikiana. Hata hivi wanavyotuona leo tukifanana na mioyo yetu na utendaji wetu wa kazi uko pamoja, Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana mdogo wangu Mheshimiwa Katambi. Nimefanya kazi naye pia akiwa Naibu Waziri wangu, najua utendaji kazi wake, namshukuru sana kwa kazi nzuri. Hivyo basi, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu yuko Ofisini kwetu, tunamkaribisha Mheshimiwa Naibu Waziri, Judith kwa kumsaidia Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na tunamtakia kila la kheri na tumeona ameanza kazi kwa ushirikiano mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru Katibu Mkuu wangu Dkt. Jim na Naibu Katibu Mkuu. Hapa kipekee namshukuru Mkurugenzi pia wa Tume ya Uchaguzi ambaye Fungu lake liko kwetu, namshukuru Msajili wa Vyama, Mheshimiwa Jaji Mtungi na timu zao zote na wataalam wote ambao wako kwenye Ofisi yetu. Ahsante Katibu Mkuu kwa uratibu lakini ahsanteni sana Wakuu wa Taasisi na Taasisi zote na watendaji na wataalam wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa siwezi kuacha kuvishukuru vyama vya siasa, na leo Baraza la Vyama vya Siasa wako hapa wakiongozwa na Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa. Nawashukuru kwa sababu wameitikia vyema wito wa Mheshimiwa Rais wa zile *4Rs* na wameendelea kuzienzi na kuzisimamia vizuri. Vyama vyote vya siasa nchini, nawashukuru na Ofisi yetu itaendelea kusaidiana na Msajili wa Vyama katika kulea demokrasia ambayo sasa hivi kwenye mikono ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, analitendea vema na haki eneo hilo la mfumo wa demokrasia na hasa vyama vingi nchini. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Peramiho, ahsanteni sana Wanaperamiho. Mbunge wao nipo nachapa kazi, hakuna kulala. Tunajua mwaka huu tunalo jambo letu la Serikali za Mitaa na mwakani kazi ni ileile hakuna kurudi nyuma. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mbele, Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na mimi Mbunge wao nimo. Kwa hiyo nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Peramiho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kutimiza miaka mitatu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Waheshimiwa Wabunge wenzangu naungana na nyie, kila aliyesimama amesema utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni moto kweli kweli. Kwa hiyo naungana nao kumpongeza sana. Tunashukuru sana Serikali zilizotangulia na Marais waliotangulia, wamefanya kazi kubwa lakini miaka mitatu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeonyesha mageuzi makubwa sana ya maendeleo kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tunasema haikuwa rahisi watu kufanya yale ambayo ameyafanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa muda mfupi. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonyesha uzalendo, ukomavu, umahiri, ubobezi katika kuliongoza Taifa letu na katika maneno hayo hakuna mjadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tufikirie pale alipoamua kubeba dhamana na kufanya maamuzi magumu kwenye mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa na kuruhusu mikutano ya hadhara, haikuwa kitu chepesi hata kidogo lakini kwa sababu Mheshimiwa Rais wetu ni mkomavu, ana uwezo, aliweza kufanya maamuzi hayo. Mnafahamu alianzisha mazungumzo ya maridhiano na vyama vya siasa na kuanzisha mijadala huru ya wazi ya masuala ya demokrasia nchini. Tunamshukuru na tunamheshimu sana Mheshimiwa Dkt. Samia kwa jinsi alivyo na anavyoweza kuongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakumbuka alipofanya maamuzi ya kuruhusu maandamano ya vyama vya upinzani nchini hakusita, alikuwa na *courage* ya hali ya juu. Kwa hiyo kwa kweli tunampongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais wetu. Ndiyo maana naungana na Waheshimiwa Wabunge na nasema kwamba; sisi kwanza Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tutaendelea kumuenzi na kumthamini Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutasita kufanya hivyo na hatutasita kusema mahali popote. Wote tunafahamu maneno haya tunayoyasema Bungeni yanaungwa mkono na akinamama wa Tanzania waliokuwa hawana mahali pa uzazi salama, leo wana mahali pa uzazi salama. Wanajua alichowafanyia Mheshimiwa Rais wetu, wako nyuma yake, asisite, asonge mbele tuko pamoja naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wakulima, nitasema hata wakulima wa Jimbo la Peramiho na Mkoa wa Ruvuma na mikoa mingine nchini, wanafahamu Mheshimiwa Rais wetu alivyoondoa kero ya bei ya mbolea kwa kuipa ruzuku. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Rais, wananchi wa Jimbo la Peramiho na wananchi wa mikoa yote nchini, kwa hili la ruzuku, wako pamoja naye. Wataendelea kumuunga mkono kwa sababu amewaondolea mzigo mkubwa wakulima wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mheshimiwa Bashe amesema hapa, pamoja na kilimo hiki cha mwaka huu na hasa kwenye zao la mahindi, mavuno yatakuwa ni mengi. Mheshimiwa Rais wetu ameshahakikisha masoko ya uhakika, hao wakulima wanamuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu. Safari inaendelea na ushahidi utaonekana mwakani, Mheshimiwa Rais asonge mbele tuko pamoja naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wa kike ambao walikatishwa ndoto zao kwa kupata mimba, leo wamerudi shuleni na wengine wamekwenda vyuo vikuu, wako pamoja na Mheshimiwa Rais na wanamuunga mkono. Mheshimiwa Rais wetu, asonge mbele na hawa wote wanamwombea na ataendelea kubarikiwa. Amepeleka umeme vijijini, ameleta tiba za kibingwa, wako Watanzania hawakuweza kwenda kutibiwa nje kwenye tiba za kibingwa; Mheshimiwa Dkt. Mollel ameeleza hapa, Mheshimiwa Rais asonge mbele, hawa ndiyo watu wake, wanamuunga mkono na watakufa naye.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko miradi mikubwa ya kimkakati. Hebu fikiria Mheshimiwa Mavunde amesema hapa leo, migodi

mipya na mfumo mpya wa uwekezaji kwenye madini unakwenda kuwagusa wachimbaji wadogo wadogo. Hawa ndiyo watu wake Mheshimiwa Rais, asonge mbele na hao ndiyo watakaokuwa naye mpaka mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya kimkakati *SGR*, meli, viwanja vya ndege, hospitali za rufaa na mambo mengi yaliyofanyika katika Taifa letu. Tuna shida gani ya kuyasema haya hadharani na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan? Haya ninayoyasema nawaunga mkono Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri wamesema, kwa hiyo Bunge hili leo linainuka kwa makofi na kumwombea kheri Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba yuko kwenye mikono salama kwa sababu ya kazi anazozifanya na hasa kuwajali wanyonge. Hilo ni jambo kubwa na hata Mwenyezi Mungu atampa baraka tele kwa kazi hii nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza michango mingi wakati Wabunge wakichangia hapa, labda nianze na eneo hili la dawa za kulevya. Kwa takwimu tulizonazo sasa hivi ulimwenguni, 2011 waliokuwa waraibu wa dawa za kulevya walikuwa milioni 240, lakini mwaka 2020 hadi 2022, dunia nzima waliokuwa waraibu wa dawa za kulevya walifikia milioni 296, kwa hiyo kulikuwa na ongezeko. Sasa hapa nchini Tanzania waraibu ambao wana uraibu wa mambo mengi, si dawa za kulevya peke yake, ni pamoja na ulevi na uvutaji wa sigara uliopindukia, kwa mwaka 2020 walikuwa 169,269 na kwa mwaka 2022 walifika 854,134.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kusema nini? Tunataka kusema kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na kushughulika na miradi hiyo yote anapoamua kusimama na kushughulikia kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevya anafanya kitu cha msingi sana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1991 Serikali yetu ilianzisha mapambano ya dawa za kulevya kwa kutengeneza Kitengo

Maalum ndani ya Jeshi la Polisi; lakini tulivyofanya tathmini tukasema ni lazima tuongeze nguvu zaidi. Mwaka 1997 tukaanzisha Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, lakini vilevile tulifanya tathmini tukasema tusonge mbele. Mwaka 2015 tulianzisha sheria ambayo ndiyo imeunda mamlaka tuliyonayo na mwaka 2021/2022, Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema ni lazima tufanye marekebisho kwenye vifungu kadha wa kadha ili tuongeze nguvu kwenye mapambano dhidi ya biashara na matumizi ya dawa za kulevya. Naomba niwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba mwaka huu 2024 tunakuja na sera itakayotusaidia kutoa matamko makali ya kupambana na matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ziko changamoto ambazo tunaziona. Uzalishaji wa dawa humu nchini unazidi kuonekana upo na unashamiri. Tumeshuhudia mamlaka ikipambana kuteketeza mashamba ya bangi, kemikali bashirifu zikitumika na kuingizwa nchini kwa kificho ili ziweze kutengeneza dawa, vijana wadogo wakiathirika pamoja na matumizi ya *digital currency* katika kutakatisha fedha hizo ambazo zinatumika katika biashara haramu ya dawa za kulevya. Naomba niwahakikishie, chini ya uongozo mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumejipanga kuhakikisha vita hii inakuwa ni vita ambayo tutaiweza na tutafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeamua kuimarisha sheria na kutengeneza sera mpya itakayotusaidia kupambana na dawa za kulevya nchini. Sera na sheria hizo zinatakiwa zitupeleke katika kufanya utafiti, kujitambua tuko wapi hali yetu na kila kitu tunachotakiwa kufanya, udhibiti na kutoa elimu ya kutosha. Waheshimiwa Wabunge tuna kazi ngumu ya kutengeneza kinga kwa watoto wetu kutokujiingiza kwenye tatizo la matumizi ya dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia biskuti zikizalishwa zina kilevi cha dawa za kulevya na hasa bangi, ni hatari sana kwa makuzi na maadili ya watoto wetu. Kwa hiyo tunahitaji nguvu ya

pamoja Serikali na *private sector* tufanye kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Rais katika kipindi hiki kifupi tumeweza kuongeza *MAT Clinics* zile *Medical Assistants Therapy Clinics* kutoka 11 mpaka kufika 16. Hilo ni ongezeko kubwa Waheshimiwa Wabunge na tumeona waraibu karibu 16,000 wameanza kujitokeza ili kupata dawa. Ukiona waraibu wanaongezeka kwenye vituo vya kupata tiba maana yake ni kwamba mtaani sasa hivi dawa za kulevya zimepungua. Hongera sana kwa Mheshimiwa Rais kwa kuweza kudhibiti jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tuna *sober houses* 54 na nilimsikia Mheshimiwa Esther Bulaya akitu-*challenge,* kwamba kwa nini tuwe na hizo *sober house* na vitu vya namna hiyo. Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, historia ya *sober house* hapa nchini ina maneno yake mengi. Kitu kinachotufurahisha sisi Tanzania tumekuwa ni nchi ya kwanza kuanzisha tiba kupitia *sober house* katika Ukanda wa *South* Sahara na hii imetupa heshima kubwa sana. Kwa hiyo ni lazima wakati mwingine tuendelee kusifia mambo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hiyo tumeamua kujipanga kutekeleza mikakati ya kimataifa na mkakati wa kwanza wa kimataifa ni kuhakikisha kwamba tunashughulika na *supply reduction,* kwa maana ya kupunguza uingizaji wa dawa nchini. Pia tunashughulika na kupunguza uhitaji *(demand reduction),* tunashughulika na kupunguza madhara *(harm reduction)* na vilevile tunakwenda kushughulika pia na mahusiano ya kikanda na mahusiano ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa mafanikio ambayo tumeyapata kama Serikali, ongezeko la watumiaji hao wa tiba kwenye *MAT clinics* zetu. Hii inaonyesha ni kwa kiasi gani tumefanikiwa. Mpaka sasa tumekwishakamata kemikali bashirifu kilogramu 22,143 ambazo zingeingia mtaani zingetengeneza dawa na zingeharibu watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya vilevile ukamataji mkubwa wa dawa za kulevya za aina mbalimbali. Kwa mwaka mmoja tu wa 2023 mamlaka imeweza kukamata kilogramu milioni 1.9 ya dawa mbalimbali. Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba hicho ni kiwango ambacho ni mara tatu ya ukamataji ambao umefanyika nchini kwa kipindi cha miaka 11, hiyo ni kazi kubwa ambayo imefanyika. Wengine wanasema sababu ni ongezeko la uingizaji wa dawa, hapana, ni kwa sababu Mheshimiwa Rais amekuwa na utashi wa kutosha kwenye mapambano dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeboresha sheria, na Mheshimiwa Rais ameamua kutoa fedha na kununua vitendea kazi na hapa ninapowaambia tumeingiza boti moja mpya ambayo inaweza kufanya kazi mpaka kwenye Bahari Kuu na kukamata majahazi huko yanakotokea. Tumefanya mafunzo na tunategemea uzalendo walionao watumishi wa Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti na Dawa za Kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana mwezi Desemba dawa za kulevya zilikamatwa pale Dar es Salaam, zilinunuliwa kwa fedha za Kitanzania zenye thamani kama ya bilioni 40. Kama zisingekamatwa na zikauzwa wafanyabiashara haramu walikuwa wanakwenda kupata bilioni 95, fedha za Kitanzania. Sasa tufikirie ndani ya Taifa bilioni 95, fedha haramu ingeingia humu ndani ingekuwaje? Ingekuwa ni kazi kubwa, lakini kwa sababu ya uzalendo wa watumishi wetu, hilo jambo walifanikiwa, hawakutaka rushwa, walisimama imara, wakafanya kazi zao vizuri. Kwa hiyo tutaendelea kuona ni namna gani tunasimamia eneo hili. Faida za kufanya hii kazi ni kuokoa nguvu ngazi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi, vijana wa Tanzania wenye umri wa miaka 15 hadi 35 ni 20,612,566. Hawa tusipowalinda kutokana na madhara ya dawa za kulevya, tutakuwa tumeangamiza kizazi. Masuala ya afya na masuala mengine ni muhimu sana kuyaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea na suala la elimu, Waheshimiwa Wabunge wameniandikia kwamba mnawezaje kuwatambua waraibu wa dawa za kulevya. Tumekuwa tukiangalia tafiti nyingi zinatuongozaje, kwa mfano, wale ambao wamebobea kwenye matumizi ya bangi, macho yao yanakuwa mekundu sana, wanakuwa na tabia za kucheka cheka hovyo, wanakuwa na hasira za haraka, wanaongeza hamu ya kula chakula na wanakuwa wagonjwa wa akili. Kwa hiyo ukianza kutathmini hizi na ukaangalia uhalisia unaweza ukawafahamu. Kwa wale wanaotumia *heroine* na wenyewe kwa mfano wanakuwa na macho yaliyosinyaa, lakini pua zao zinakuwa nyekundu kwa sababu ya kunusa nusa sana, wanakuwa wachovu, wanapoteza uzito, wanakabiliwa na maradhi mengine. Kwa hiyo, kazi hiyo tutaifanya vizuri na tutaendelea kuangalia namna bora ya kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko eneo lingine la kuunganisha Mifuko, tumeliona na Waheshimiwa Wabunge wamesema, tunaomba tuwahakikishie kwamba jambo hili tunalifanya kwa uangalifu mkubwa. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba Mifuko hii iendelee kutoa huduma na kuwawezesha wananchi wa Tanzania na hasa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Mifuko mingi ilikuwa inashia mijini na sasa tunataka vijijini kwa kuwa kule ndiko kwenye uzalishaji na tunahitaji ibadilishe hali ya hewa mpaka huko vijijini. Tunayo mengi ya kueleza lakini naomba tu… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kengele ya pili hiyo…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** … tunayo mengi ya kueleza, lakini naomba niwahakikishie kwamba tutatoa majibu yetu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, tunawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri wanayoifanya kwenye Majimbo. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na sisi tunapokea pongezi za Wabunge. Pongezi

hizo walizotupatia zinatupa changamoto ya kuendelea kupambana, kufanya kazi kwa utii na uaminifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Ahsante, shukurani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nataka nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima wa afya hata leo tumeweza kukutana kwenye Kikao hiki cha Sita cha Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi la Mbili kwa ajili ya kuhitimisha mjadala kuhusu hoja ya bajeti ya Waziri Mkuu, taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kutumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge na Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Mabunge ya Dunia kwa namna ambavyo analiongoza Bunge letu kwa umahiri mkubwa. Nashukuru na kukupongeza sana wewe binafsi pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu imara na thabiti. Sina shaka Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakubaliana nami kuwa wameweza kuongoza vyema kipindi chote cha mjadala kuhusu hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zake na Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru na kuwapongeza sana Wenyeviti na Wajumbe wote wa Kamati za Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa michango yao muhimu ambayo wameitoa mbele ya Bunge lako Tukufu. Nikiri kwamba maoni na ushauri wao wakati wote umekuwa ukileta tija kubwa kwenye hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa hoja na michango yenu yenye tija katika kipindi chote cha mjadala wa hoja ya Bajeti ya Waziri Mkuu. Nataka nitumie nafasi hii kuwahakikishia kwamba Serikali wakati wote itazingatia maoni yao na ushauri walioutoa katika mipango na utekelezaji wa majukumu yake kwa ustawi wa maendeleo ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mawaziri wa Sekta na Naibu Mawaziri waliochangia hoja ya Bajeti ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kuwashukuru Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara, Mashirika, Taasisi na Wakala wa Serikali kwa ushirikiano mkubwa walioutoa na kufanikisha hoja ya Bajeti ya Waziri Mkuu, Taasisi zake na Mfuko wa Bunge. Nawapongeza sana Watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya katika hatua zote za maandalizi ya hotuba ya bajeti hadi tunapoelekea kuhitimisha mjadala wa hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Vilevile nawashukuru kwa ushirikiano walionipa ambao wakati wote ambao umeniwezesha kutimiza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, salamu za pole; wakati tukiendelea na Mkutano huu wa Kumi na Tano wa Bunge lako Tukufu, mnamo tarehe 9 Aprili, 2024 tuliondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani. Sina shaka Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakubaliana nami kuwa Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil alikuwa ana uwezo mkubwa na ushawishi wa kipekee ndani ya Bunge hili na mchango wake utakumbukwa daima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kutoa salamu za pole kwa wana CCM wote, familia, ndugu na jamaa wa marehemu, wananchi wa Jimbo la Kwahani na Watanzania wote

kwa ujumla. Niwaombe Watanzania wote tumwombee marehemu kwa Mwenyezi Mungu apumzike mahali pema peponi.

**WABUNGE FULANI:** Amina.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni wapo Watanzania wenzetu waliopatwa na majanga mbalimbali yakiwemo ajali za barabarani, mafuriko na mengine yaliyosababisha vifo na uharibu wa mali. Kwa masikitiko makubwa naungana tena na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa salamu za pole kwa waathirika wote wa majanga hayo. Nitumie nafasi hii kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki waliowapoteza wapendwa wao kutokana na majanga hayo. Tumwombe Mwenyezi Mungu awajalie uponyaji wa haraka majeruhi wote na kuwapa pumziko la amani marehemu wote.

**WABUNGE FULANI:** Amina.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mjadala huu ukiendeshwa, Waheshimiwa Wabunge 129 wamechangia hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kati yao Waheshimiwa Wabunge 119 walichangia kwa kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge 10 walichangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kutumia nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Hoja ya Waziri Mkuu. Ningependa kuwataja majina yao, lakini kutokana na ufinyu na muda naomba uridhie nisiwataje na badala yake majina yao yaingizwe kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wametoa ufafanuzi wa hoja nyingi zilizowawasilishwa na Waheshimiwa Wabunge wakati tukiendelea na mjadala wa Hoja ya Waziri Mkuu. Sikusudii kuzirudia, lakini nataka nishukuru kwa michango yao tena na kwamba tutaendelea kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa Waheshimiwa Mawaziri wataendelea kufafanua zaidi

baadhi ya hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge kwenye mjadala huu wakati wakiwasilisha hoja za bajeti za sekta zao. Kadhalika kama ilivyo ada Serikali itatoa ufafanuzi zaidi kuhusu hoja zilizosalia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waheshimiwa Wabunge wanavyofahamu kwamba tayari tumetimiza miaka mitatu ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni jambo la kujivunia kuwa katika kipindi hicho cha miaka mitatu ya uongozi wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya mambo makubwa kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa Taifa letu. Sisi sote ni mashahidi kwamba amekuwa kinara katika Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020. Mheshimiwa Rais wakati wote amekuwa akionyesha busara, uhodari mkubwa, uzalendo, usikivu, uwajibikaji na kuwa mfano wa kuigwa ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kutumia nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu kumshukuru kwa uzalendo wake na namna anavyojitoa kulitumikia Taifa letu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali. Miradi hiyo inahusisha Sekta za Maji, Elimu, Afya na Miundombinu ambayo niliieleza wakati nilipokuwa nawasilisha hoja yangu. Naomba sasa nieleze kwa uchache mafanikio mengine yaliyopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, ni kuleta maridhiano ya kisiasa, amani na utulivu wa kidemokrasia hapa nchini. Niendelee kutokuwa na mashaka na Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakubaliana nami kuwa Mheshimiwa Rais ni kinara katika kuimarisha demokrasia vilevile haki za binadamu na utawala bora. Katika kipindi hiki cha uongozi wake tumeshuhudia utekelezaji wa falsafa yake ya *4R (Reconciliation, Resilience, Reform and Rebuilding)*. Kwa lugha ya Kiswahili ni Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Mabadiliko ambayo kwa hakika yamekuwa chachu ya kuimarisha siasa za ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utashi wake, mwelekeo wa mitazamo na uendeshaji wa masuala ya kisiasa umebadilika na kuchagiza siasa za kistaarabu. Sote ni mashuhuda kuwa nchi yetu inaendelea kuwa na mshikamano, amani na umoja wa kitaifa. Hii inatokana na msisitizo wake kuhusu utekelezaji wa masuala ya haki za binadamu, utawala bora na demokrasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza masuala ya demokrasia kwa vitendo, tumeshuhudia maboresho mbalimbali ya upande wa mifumo, sheria na uendeshaji wa shughuli za kisiasa hapa nchini. Licha ya hayo tumeshuhudia pia uwepo wa fursa zaidi za mijadala na maridhiano miongoni mwa makundi ya wadau wa demokrasia na masuala ya siasa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni maboresho ya mfumo wa utoaji haki na Taasisi za Hakijinai katika kuhakikisha mfumo wa utoaji haki unaboreshwa. Mnamo tarehe 31 Januari, 2023, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliunda Tume Maalum aliyoipa jukumu la kushauri namna njema ya kuboresha mfumo wa utendaji kazi katika taasisi zinazohusika na hakijinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, tume hiyo ilipokea maoni kutoka kwa wananchi na wadau wengine wa hakijinai na kutoa mapendekezo ya maboresho yanayohitajika kufanyika. Tangu tume ilipowasilisha mapendekezo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za maboresho ya mfumo wa utoaji wa hakijinai, ikiwemo kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa Taasisi za Hakijinai. Licha ya hayo Serikali inaendelea kufanyia kazi mapendekezo yote yaliyotolewa kwa lengo la kuhakikisha kuwa, wananchi wanapata haki zao kwa wakati ili waweze kuendelea kufanya shughuli za maendeleo yao binafsi na Taifa zima kwa ujumla. Hii ndiyo dhamira ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kukidhi kiu na matarajio ya wananchi katika utoaji wa hakijinai kuanzia hatua ya uchunguzi, ukamataji watuhumiwa hadi utoaji wa hukumu yenyewe pale inapofanyika haki mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, ni matumizi ya TEHAMA na Lugha ya Kiswahili mahakamani. Katika hatua nyingine Serikali ya Awamu ya Sita, imeendelea kufanya jitihada kubwa ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia kutokana na mapinduzi ya nne ya viwanda hapa duniani. Jitihada hizo zimeanza kuleta mafanikio katika utendaji wa Serikali kwa kuunganisha Serikali yote (Wizara, Idara, Wakala na Taasisi zake) ili ziweze kusomana kwa kimfumo. Tumeanza kupata mafanikio tukianza na Mahakama ya Tanzania, ambapo mifumo mbalimbali ya TEHAMA imejengwa ili kurahisisha na kuhakikisha utoaji wa haki kwa wananchi unaimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifumo hiyo ni pamoja na mfumo wa usajili, uendeshaji na usimamizi wa mashauri kwa ajili ya kurahisisha, kuharakisha na kuokoa muda wa mwenendo wa shauri mahakamani. Mfumo mwingine ni wa unukuzi na tafsiri ya mienendo ya mashauri mahakamani kwa lengo la kuwa na suluhu ya kudumu, ili kuwawezesha Waheshimiwa Majaji na Mahakimu kuondokana na adha ya kuandika kwa mkono mwenendo wa mashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatua kubwa sana katika mfumo huu unaorekodi sauti na kupeleka kwenye maandishi. Vilevile unaweza kutafsiri Lugha ya Kiswahili au Kiingereza kulingana na uhitaji na kwa upande mwingine Kanuni za Mahakama zimeanza kutafsiriwa sambamba na uandaaji wa mihtasari ya hukumu katika Lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha wananchi kuelewa mwenendo wa mashauri yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni mafanikio kwenye Sekta ya Uzalishaji ambako kuna kilimo, mifugo, uvuvi na viwanda. Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kufanya jitihada mbalimbali za kuinua sekta ya uzalishaji. Kama tunavyofahamu uzalishaji kupitia Sekta ya Kilimo umeendelea kuongezeka na kuiwezesha sekta hii kuchangia 26% ya Pato la Taifa kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zinazofanywa na Serikali ni katika kuhakikisha kuwa, Sekta ya Kilimo inaendelea kutoa

mchango mkubwa katika upatikanaji wa ajira, malighafi za viwandani, kuleta fedha za kigeni kutokana na mauzo ya nchi za nje, pamoja na kulihakikishia Taifa letu usalama wa chakula. Jitihada mbalimbali zinazofanywa zimewezesha nchi yetu kuwa na utoshelevu wa chakula kwa 124%.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina shaka Waheshimiwa Wabunge watakubaliana na mimi kuwa, Mheshimiwa Rais amefanya jitihada kubwa kuimarisha Sekta ya Uvuvi. Utekelezaji wa ujenzi wa Mradi mkubwa wa Bandari ya Uvuvi ya Kilwa Masoko unaogharimu zaidi ya bilioni 289.5 ni kielelezo tosha cha dhamira yake njema ambayo pia Mheshimiwa Rais ameionesha hadharani. Tayari ameshatoa ridhaa ya matumizi ya shilingi bilioni 106.2 za kuendeleza ujenzi wa bandari hiyo, ambayo itachochea ukuaji wa Sekta ya Uvuvi na kuongeza pato la Wananchi kama ilivyoelezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020 – 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sekta ya Mifugo, vilevile tumeshuhudia ikiendelea kuimarika na kuwezesha kutoa ajira kwa wananchi milioni 4.5. Aidha, kutokana na jitihada zilizopo mchango wa sekta katika pato la Taifa umefikia 7.1% kwa mwaka. Uwekezaji kwenye viwanda umeongezeka, ili kuzalisha bidhaa kwa mahitaji ya ndani na kupata masoko ya bidhaa nje ili kuongeza pia pato la kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Mheshimiwa Rais amelieleza ni mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Amelifafanua vizuri zaidi, lakini nataka nieleze tu kwamba, Serikali imeendelea kufanya jitihada mbalimbali za kupambana na tatizo la dawa za kulevya hapa nchini. Hii inatokana na ukweli kwamba, kundi la vijana ambao ni nguvukazi ya Taifa linalotarajiwa kuwakilisha maendeleo, ndiyo linaathirika zaidi na matumizi ya dawa za kulevya hapa nchini. Licha ya tatizo la dawa za kulevya kuendelea kuwepo hapa nchini, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya katika kipindi kifupi, imefanya kazi kubwa sana. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa hatua anazozichukua za kuiwezesha mamlaka hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka inafanya kazi kubwa na nzuri, katika hili natoa rai kwa Taasisi za Serikali, Taasisi Binafsi, Mashirika ya Dini, Taasisi zisizokuwa za Serikali na Washirika wa Maendeleo na wananchi wote kwa ujumla, kutoa ushirikiano kwa mamlaka ili iweze kutimiza majukumu yake. Vilevile namwomba kila mmoja kwa nafasi yake, ashiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya dawa ya kulevya. Taasisi inaendelea kufanya kazi nzuri ya kudhibiti uzalishaji, usafirishaji, uuzaji na utumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana pia Waheshimiwa Wabunge kwa michango waliyoitoa kuhusu udhibiti na mapambano dhidi ya madawa ya kulevya, umoja ni ushindi. Hivyo basi, Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi wote tushirikiane katika mapambano ya dawa za kulevya, kwa pamoja tutashinda, mapambano bado yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze kidogo juu ya utekelezaji wa sera na fursa za kujikwamua kiuchumi. Serikali imeendelea kutekeleza sera mbalimbali za uwezeshaji wa makundi maalum ya wanawake, vijana na wenye ulemavu. Lengo likiwa ni kuhakikisha makundi haya yanashiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi hapa nchini. Utekelezaji wa sera hizo unafanywa kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi, ambayo imeendelea kunufaisha makundi yote, wakiwemo wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, fedha kiasi cha shilingi bilioni 743.7 zimetolewa kwa wanufaika zaidi ya milioni sita kupitia Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Katika utekelezaji wa sera ya ushirikishwaji Watanzania kwenye miradi ya kimkakati na uwekezaji nchini, wanawake na vijana wameendelea kunufaika kupitia miradi ya kimkakati na uwekezaji. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya Watanzania 162,968 wamenufaika na ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuratibu masuala ya uzalishaji wa fursa za ajira nchini kwa kujenga mazingira wezeshi kwa wawekezaji na kuimarisha ushirikiano baina

ya Serikali na sekta binafsi. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, fursa za ajira 2,489,136 zimezalishwa sawa na wastani wa ajira mpya 829,712 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuwezesha vijana ili waweze kujiajiri kushiriki kwenye shughuli za maendeleo na kuchangia pato la Taifa. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, kiasi cha shilingi bilioni 3.19 kimeshatolewa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, ambazo zilitumika kutoa mikopo kwa ajili ya kuwezesha miradi 148 katika Sekta za Kilimo, Viwanda na Biashara katika halmashauri 62.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali imetoa mafunzo ya ujasiriamali, usimamizi, kurasimisha na kuendeleza biashara kwa vijana katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI hivi karibuni itatoa taarifa ya mfumo utakaotumika kutoa mikopo ya 10% kutoka katika halmashauri zetu nchini ili wajasiriamali waweze kuendesha shughuli zao za kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utunzaji wa mazingira, sote tunatambua kuwa uhifadhi wa mazingira una umuhimu mkubwa katika maisha yetu ya kila siku, kwa kuwa unatuwezesha kupata mahitaji muhimu ikiwemo maji, chakula, madawa, malighafi za viwandani, pamoja na nishati ya umeme itokanayo na maji. Ni ukweli usiopingika kuwa upatikanaji wa mahitaji haya, unaharakisha maendeleo yetu ya kiuchumi na kijamii, hivyo, tuna kila sababu ya kutunza mazingira ili nayo yaweze kututunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu huo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amekuwa mstari wa mbele kuhamasisha utunzaji wa mazingira kwa faida yetu na vizazi vijavyo. Vilevile, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mara kwa mara amekuwa akitukumbusha kuhusu utunzaji wa mazingira yetu. Nitumie nafasi hii kuungana na viongozi wetu, kuzungumza kwa uchache kuhusu uhifadhi wa mazingira hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na uharibifu mkubwa wa mazingira ambao kimsingi unasababishwa na ukataji wa miti hovyo kwa matumizi ya nishati. Kilimo kisicho endelevu kinachofanyika kwa kukata miti na kuchoma mashamba ikiwa ni njia ya kurahisisha maandalizi ya shamba. Sababu nyingine ni ufugaji holela usiozingatia uwezo wa eneo la malisho, ambao umesababisha mifugo kuharibu ardhi na maeneo mengine yaliyohifadhiwa ikiwemo vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa athari za uharibifu wa mazingira ni mbaya kwa kuwa, huathiri masuala ya kijamiii na kiuchumi mathalani mara kadhaa tumeshuhudia vifo vya mifugo kutokana na ukame na uhaba wa maji, vilivyotokana na mabadiliko ya tabianchi yaliyosababishwa na uharibifu wa mazingira. Vilevile mvua nyingi kupita kiasi zimeendelea kusababisha athari kubwa nchini, ikiwemo mafuriko, vifo, na uharibifu wa miundombinu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa uhifadhi wa mazingira, nitumie fursa hii kusisitiza masuala yafuatayo:-

(i) Viongozi wote kuanzia ngazi za vijiji hadi mikoa, wasimamie kikamilifu utunzaji wa mazingira na suala hili liwe ajenda ya kudumu katika vikao vyote katika ngazi hizo; *(Makofi)*

(ii) Viongozi wa Mikoa na Wilaya wasimamie utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu athari za kuchoma misitu hovyo, pia kufuga bila kuangalia uwezo wa maeneo ya kulishia, kufanya shughuli za kilimo kwenye maeneo yaliyohifadhiwa na kuondokana na tabia ya kukata miti hovyo;

(iii) Halmashauri zote nchini, zisimamie kikamilifu sheria ndogo za uhifadhi wa mazingira na kuwachukulia hatua wale wote wanaofanya uharibifu wa mazingira yetu;

(iv) Taasisi za Uhifadhi wa Misitu *(TFS)* na halmashauri ziandae vitalu vya miti inayoendana na ikolojia ya maeneo yao, kuigawa kwa wananchi na kuhakikisha inapandwa na kukua. Hatua hii iendane sambamba na kusimamia upandaji wa miti kwa kila kaya. Vilevile *TANROADS* na *TARURA* wahakikishe wakandarasi wanapanda miti pembezoni mwa barabara katika kila mradi wa ujenzi wa Barabara. Kwa kufanya hivyo itasaidia upandaji na utunzaji wa mazingira; *(Makofi)*

(v) Wananchi tuendelee kushirikiana na Serikali katika uhifadhi wa mazingira ili kuepusha madhara yanayotokana na uharibifu wa mazingira ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia mabadiliko ya hali ya hewa. Kasi ya mabadiliko ya hali ya hewa duniani inaendelea kuongezeka kila mwaka na athari zake zimekuwa kubwa. Tathmini ya Shirika la Hali ya Hewa Duniani, limeonesha kuwa wastani wa ongezeko la joto kwa 2023 ulifikia nyuzi joto 1.4 kwa kipimo cha selsiasi *(Celsius)* na kuvunja rekodi ya kuwa mwaka wenye joto kubwa zaidi katika historia ya dunia. Kwa upande wa Tanzania, wastani wa ongezeko la joto kwa mwaka 2023 ulifikia nyuzi joto 1.0 kwa kipimo cha selsiasi. Pia ulivunja rekodi kwa kuwa mwaka wenye joto kubwa zaidi katika historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la joto limesababisha uwepo wa *El-Nino* ambayo imeambatana na mvua kubwa na mafuriko hapa nchini. Oktoba hadi Desemba, 2023 kulikuwa na ongezeko kubwa la mvua, ambapo jumla ya milimita 534.5 zilipimwa ikilinganishwa na milimita 227.2 kwa mwaka 2022, ikiwa ni ongezeko la 135.5%. Vilevile ongezeko hilo la mvua limeshuhudiwa katika kipindi cha Januari hadi Aprili, 2024 na kwa mujibu wa Taasisi ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)*, imesema mvua zitaendelea kunyesha hadi mwezi Mei, 2024 kwenye Mikoa ya Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi, Ukanda wa Mikoa ya Kusini mwa Tanzania na Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kwa nchi mbalimbali duniani, nchi yetu imeendelea kupata mvua nyingi zaidi ya wastani kutokana na mabadiliko ya tabianchi, ambayo yamesababisha maafa mbalimbali. Maafa hayo ni pamoja na vifo, uharibifu wa mazao, makazi, mali za wananchi, miundombinu kama vile barabara, madaraja na reli. Kama mnavyofahamu maeneo mengi yameathirika na mvua. Mikoa ambayo imeathirika kwa sasa ni Mikoa ya Arusha, Lindi, Manyara, Kigoma, Morogoro, Pwani na Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Maafa Kitaifa kwa kushirikiana na Kamati za Maafa za Mikoa na Wilaya, zimeendelea kuchukua hatua mbalimbali kurejesha hali katika maeneo yaliyoathirika ikiwemo Wilaya ya Rufiji, eneo la Muhoro; Wilaya ya Kibiti, eneo la Delta; Newala, Lindi Mjini, Liwale, Arusha, eneo la Kisongo; Mkoani Morogoro Malinyi, Wilaya ya Kilombero; kule Mrimba maeneo ya Masagati na Utengule na kule Mbeya kulikotokea maporomoko ya udongo kutoka milimani eneo la Kawetere.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizo ni pamoja na kutoa misaada ya kibinadamu kwa waathirika, kurejesha miundombinu iliyoathirika, kutoa elimu kwa jamiii kuhusu kujikinga, kuchukua tahadhari na kuendelea kufanya tathmini ya kina ya athari na vyanzo vya maafa hayo. Kamati za Maafa za Kitaifa kwa kushirikiana na Kamati za Maafa za Mikoa na Wilaya, zinaendelea kufanya tathmini kwenye maeneo yote yaliyopata athari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuchukua hatua kadhaa tena za haraka na za dharura ikiwemo uokoaji, kutoa chakula, maji, makazi ya muda, dawa, mbegu na huduma za unasihi, katika maeneo yaliyopata athari kubwa za mvua ambazo zinaendelea hivi sasa. Tunatoa pole kwa ndugu zetu walioathirika na mvua hizo na naomba wananchi wote kuchukua tahadhari katika kipindi hiki cha mvua kubwa zinazoendelea kunyesha hapa nchini. Niwasihi sana wananchi, waendelee kuwa na subira pale wanapoona maji mengi yanapita hususani barabarani ili kuepusha ajali zinazoweza kuepukika.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa waendesha vyombo vya moto vya usafiri na wavuka kwa miguu, kuchukua tahadhari ya kutovuka mahali popote wanapoona maji yanakatiza barabara, ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza kama ambavyo imetokea eneo la kisongo kule Mkoani Arusha, kwa gari la wanafunzi kutumbukia kwenye shimo, kwa dereva kupinga, kukaidi na kupita kwenye eneo ambalo maji yanavuka bila kujiridhisha kama eneo hilo lina maporomoko au la.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANROADS, TARURA* na Shirika la Reli waendelee kuchukua hatua za haraka wakati uharibifu wa miundombinu ya barabara na reli unapoendelea kujitokeza. Hatua hizo ziendelee sambamba na kutoa taarifa kwa watumiaji wa miundombinu hiyo, kuweka alama za tahadhari na kuweka kambi maalum za matengenezo katika maeneo yaliyoathirika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizikumbushe mamlaka za upangaji kuzingatia mipango ya matumizi bora ya ardhi pamoja na kusimamia upangaji wa makazi kwa kuzingatia sheria ya mipango miji. Aidha, Wizara ya Maji kwa kushirikiana na sekta mtambuka, waendelee na mkakati wa ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua ikiwemo mabwawa na kuyahifadhi kwa ajili ya huduma za jamii na uzalishaji ikiwemo kilimo, pia majosho ya kunyweshea mifugo ili kupunguza athari za uharibifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakumbushe watendaji wote wa Serikali kusimamia uratibu wa maafa kwa kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 6 ya mwaka 2022 na kanuni zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa mwaka 2022 umeweka bayana majukumu ya kukabiliana na maafa kwa kuanzia ngazi ya kijiji au mtaa, kata, shehia, wilaya, mkoa na Taifa, kupitia Kamati za Usimamizi wa Maafa zilizopo katika ngazi husika. Hivyo basi, nasisitiza kuwa, Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi zote ziendelee kuweka mipango madhubuti ya kutekeleza majukumu ya usimamizi wa maafa katika ngazi hizo pamoja na kutoa elimu kwa wananchi ya kutoishi maeneo ya mabonde ili

kuepusha kutokea kwa maafa kama ambavyo sasa tunashuhudia kwenye maeneo yaliyoathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia mwelekeo na mwenendo wa maandalizi ya Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo. Tarehe 3 Aprili, 2024 wakati nawasilisha Hotuba yangu ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na mwelekeo wa kazi zake kwa mwaka wa fedha 2024/2025, nililieleza Bunge lako Tukufu kuhusu mchakato wa maandalizi ya Dira Mpya ya Maendeleo ya Taifa. Niruhusu niwapitishe Waheshimiwa Wabunge katika mafanikio yaliyopatikana katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 pamoja na maandalizi ya Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, umewezesha Taifa letu kuwa na mafanikio yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kuboresha hali ya maisha ya Watanzania ikiwemo utoshelevu wa chakula, kuimarika kwa huduma za jamii hususan afya, elimu na upatikanaji wa maji, ongezeko la idadi ya wanawake katika nafasi za uongozi na utawala katika maeneo mbalimbali hapa nchini, kuongezeka kwa umri wa kuishi kwa Watanzania na kupunguza kiwango cha umaskini wa kutupwa kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuimarika kwa mazingira ya amani, usalama na umoja, ikiwemo kuzingatiwa kwa utii wa sheria na utawala wa kisheria kulikowezesha kupungua kwa matukio ya uhalifu wa aina mbalimbali, hususan mauaji, wizi wa watoto, unyang'anyi wa kutumia silaha, wizi katika barabara kuu, uhalifu wa kifedha na dawa za kulevya. Yale ambayo yanajitokeza yanaendelea kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuimarika kwa utawala bora ikiwemo utaratibu wa makabidhiano ya kiuongozi na kiutawala kwa amani na utulivu. Kuongezeka kwa kiwango cha haki za msingi za binadamu na kuendelea kupungua kwa kiwango cha rushwa hapa nchini. Kuwepo jamii inayoelimika

vema na inayojifunza ambapo idadi ya Watanzania wanaopata elimu rasmi imeongezeka katika ngazi mbalimbali ikiwa ni ngazi ya elimu ya msingi, sekondari na vyuo vikuu. Aidha, kumekuwa na ongezeko kubwa la nyenzo na fursa za kuwezesha kuendelea kujifunza kupitia uwepo wa majukwaa ya mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, uchumi wetu kuweza kukabiliana na ushindani katika nchi nyingine kulikochangia kuongezeka kwa mpango wa pamoja wa Sekta ya Viwanda, Ujenzi na Uzalishaji wenye pato la Taifa. Kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi kupitia Sekta Ndogo ya Uzalishaji na kuhimili kiwango cha mfumuko wa bei kwa chini ya tarakimu moja. Ongezeko la pato la Taifa kwa mwaka kwa wastani wa 6.7%, kati ya mwaka 2000 na 2021, kuimarika kwa miundombinu ya msingi na ya kiuchumi, hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, huduma za mawasiliano na huduma za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, matarajio yetu kwa Dira Mpya ya Taifa ni mafanikio yaliyopatikana yanayotokana na utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 ambayo itafikia tamati ifikapo Juni, 2026. Sasa, tuko kwenye mchakato wa maandalizi ya Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo inayotarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2026/2027. Ni matarajio yetu kuwa, utekelezaji wa Dira Mpya utawezesha nchi yetu kupiga hatua zaidi kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dira Mpya pamoja na mambo mengine itazingatia masuala muhimu yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kufungamanisha ukuaji wa uchumi na sekta za uzalishaji; Kuimarisha upatikanaji wa *data* kwa sekta isiyo rasmi ili kuweza kurasimisha shughuli na kutambua mchango wake katika ukuaji wa Uchumi; Kuboresha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini; Kuwepo kwa utaratibu jumuishi wa programu mbalimbali za utekelezaji wa Dira Mpya; Kutoa kipaumbele katika ufanisi wa Mashirika ya Umma wakati wa utekelezaji wa Dira Mpya; Kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi ndani na nje ya nchi pamoja na kuwawezesha wenyeji kuwa na utayari wa kupokea na kushirikiana na wageni wanaokuja kuwekeza na kufanya biashara

hapa nchini; na Kuweka mkazo zaidi katika suala la Maadili ya Taifa na kubainisha mapema viashiria hatarishi na namna ya kukabiliana navyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine natumia nafasi hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kushiriki kikamilifu katika mchakato wa maandalizi ya Dira yetu Mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia Maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano. Wakati tunaelekea kutimiza miaka 60 ya Muungano wetu, sote ni mashahidi kwamba, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umedumu na umekuwa ni wa kipekee na wa kuigwa Barani Afrika na duniani kwa ujumla. Vilevile, sote tunatambua kwamba, jitihada kubwa zimefanyika katika kulinda Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao ni Tunu ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matunda ya Muungano wetu yanajumuisha kuimarika kwa utaifa, umoja, amani, utulivu na hali ya maisha ya wananchi kutokana na ukuaji wa uchumi wa pande zote mbili za Muungano. Aidha, kuingiliana kwa kuoleana pia nako kumeimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuendelea kuutunza Muungano wetu ulioasisiwa na kuenziwa kwa manufaa ya Watanzania kwa kizazi cha sasa na baadaye, Serikali ilizindua kitabu kinachoelezea chimbuko la historia hiyo, misingi na maendeleo ya Muungano. Vilevile, elimu kwa umma kuhusu muungano imekuwa ikitolewa kupitia vipindi vya redio na *television*. Tumepeleka magazetini semina, warsha, makongamano, Maonesho ya Kitaifa, ziara za viongozi, machapisho mbalimbali na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa terehe 26 Aprili, 2024, nchi yetu itaadhimisha Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Maadhimisho hayo yataongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yatakayofanyika Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio yaliyopangwa kufanyika ni pamoja na uzinduzi wa Maadhimisho ya Sherehe za Muungano ambayo yalifanyika tarehe 14, jana, kule Zanzibar. Matukio mengine ni uzinduzi wa maonesho ya Muungano yatakayofanyika tarehe 19 Aprili katika Viwanja vya Mnazi Mmoja Jijini Dar es Salaam. Kutakuwa na Tukio la Dua na Sala ya kuliombea Taifa letu siku ya terehe 22 Aprili, 2024 katika Uwanja wa Jamhuri hapa Jijini Dodoma. Natumia fursa hii kuwajulisha Watanzania kuwa, maandalizi yanaendelea vizuri na wote mnaalikwa kushiriki katika matukio hayo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio hayo ni muhimu katika kuimarisha Muungano wetu, ikiwa ni njia mojawapo ya kuwaenzi waasisi wa Muungano ambao ni Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Amani Karume. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa pumziko la amani waasisi hawa wa Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wanafahamu kwamba Taifa letu mwaka huu litakuwa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, uchaguzi huu ni muhimu sana kutokana na ukweli kwamba, viongozi wa Serikali za Mitaa ni msingi imara katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Taifa letu. Licha ya hayo, Viongozi wa Serikali za Mitaa ni wasimamizi wa karibu wa shughuli za maendeleo ya wananchi na pia, wanalo jukumu kubwa la kuhakikisha ulinzi na usalama wa wananchi katika maeneo yao. Kutokana na umuhimu huo, napenda kusisitiza kuhusu masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ni Watanzania wenzangu bila kujali jinsia watumie haki yao ya Kikatiba ya kuchagua na kuchaguliwa. Wale wenye uwezo wajitokeze kugombea nafasi za uongozi pamoja na kushiriki kikamilifu siku ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Watanzania wote wajitokeze kwa wingi ili kushiriki katika hatua zote za uchaguzi huo, ikiwemo Maboresho ya Daftari la Mpiga Kura.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, ni viongozi wa Serikali watumie kila fursa zikiwemo semina, warsha na mikutano kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika uchaguzi huo. Waweke mkakati wa kutoa elimu kwa umma ili waweze kuwajulisha wananchi kufahamu haki zao na wajibu wao katika kuchagua viongozi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ni wamiliki wa vyombo vya habari waweke mkakati wa kuhamasisha umma wa Watanzania kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Waandae makala maalum na vipindi maalum kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie utambuzi au kutambua mchango wa watumishi wa umma. Watumishi wa umma wana mchango mkubwa katika kutafsiri na kutekeleza maono ya Mheshimiwa Rais. Mafanikio tunayoshuhudia sasa katika utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya Taifa ni kutokana na kazi nzuri inayofanywa na watumishi wa umma. Natumia nafasi hii kuwapongeza kwa dhati watumishi wote wa umma kwa kujitoa kwao na kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, nawakumbusha watumishi wenzangu kuimarisha ufanisi wa utoaji huduma kwa wananchi na kutekeleza kikamilifu wajibu tulionao. Watumishi wote tujikite katika kutatua changamoto na kero za wananchi, tuwafuate kwenye maeneo yao tukawasikilize na kutoa majawabu yanayohitajika. Kwa kufanya hivyo wananchi wataishi kwa amani na utulivu na kuendeleza shughuli za uzalishaji mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nifafanue baadhi ya hoja ambazo zilichukua nafasi kwenye mijadala yetu. Hoja ya kwanza ilitolewa na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Janejelly Ntate James, Mbunge wa Viti Maalumu. Hoja ilikuwa ni Serikali kufanya maboresho ya ulipaji wa mafao ya wafanyakazi kupitia

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na kwamba, Serikali iongeze wigo wa utoaji elimu ya kanuni mpya za mafao kwa watumishi, kwa lengo la kujenga uelewa wa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni mpya ya ulipaji wa mafao iliyoanza kutumika tarehe Mosi Julai, 2022 kwa kuzingatia tathmini ya uhimilivu na uendelevu wa Mfuko iliyofanyika katika kipindi husika. Serikali imesikia ushauri na kupokea maoni mbalimbali ya wadau wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Vyama vya Waajiri na wafanyakazi wenyewe. Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mafao kwa wastaafu na itaendelea kufanya tathmini ya kuzingatia sheria za kazi ili tuweze kufikia hatua nzuri ambayo haitazua malalamiko mengi. Aidha, kuhusu utoaji wa elimu ya kanuni za mafao kwa watumishi, Serikali itaendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa jamii ikiwemo na mafao kwa watumishi kupitia njia mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kumtaka Waziri wa Kazi na Ajira asimamie kuongeza wigo wa utoaji wa elimu ya mafao kwa watumishi kwa lengo la kujenga uelewa wa kutosha pamoja na mjadala ambao wanaendelea nao juu ya uwepo wa kikokotoo ambacho sasa kimekuwa kinatolewa ushauri na makundi mbalimbali ya wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ilitolewa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mbunge wa Jimbo la Gairo, Serikali ihakikishe inaweka mikakati ya kuwezesha upatikanaji wa vyanzo vingi vya mapato ili kuwezesha upatikanaji wa Bima ya Afya kwa wananchi vijijini. Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya mwaka 2023, imeanzisha Mfuko kwa ajili ya kugharamia Bima ya Afya kwa watu wasio na uwezo na kubainisha vyanzo vya fedha vya Mfuko huo. Serikali itaendelea kupokea mapendekezo ya uendeshaji wa mfuko, ikiwemo vyanzo vya mapato na kufanya maboresho kadri inavyofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya wanyamapori kuvamia maeneo ya wananchi pamoja na mauaji ya watu kwenye hifadhi, iliyotolewa na Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, Mbunge wa Viti Maalum. Serikali inatambua uwepo wa

changamoto ya wanyamapori kuvamia makazi na mashamba na kusababisha madhara kwa wananchi wanaoishi karibu na hifadhi; madhara hayo ni pamoja na ulemavu, vifo na uharibifu wa mali. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na utoaji wa elimu ya kukabiliana na wanyama waharibifu, uanzishaji wa Vituo vya Ulinzi kwa Maafisa Wanyamapori. Kwa upande mwingine, kumekuwa na changamoto ya baadhi ya wananchi kuvamia maeneo ya hifadhi na kusababisha migogoro baina yao na Askari wa Hifadhi, changamoto ambayo pia imekuwa ikisababisha majeruhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kuwakumbusha wasimamizi wa hifadhi kuzingatia taratibu wakati wa kushughulikia changamoto za uvamizi wa hifadhi. Kwa upande mwingine, nawasihi wananchi kuheshimu mipaka ya maeneo yaliyohifadhiwa na kuacha tabia ya kuingia hifadhini kiholela, kuingiza mifugo, kufanya shuguli za kilimo ndani ya hifadhi na uwindaji haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni ya Mheshimiwa Kasalali, Mbunge wa Sumve ya utekelezaji wa ahadi za Mawaziri. Serikali inaendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 na ahadi za viongozi katika maeneo mbalimbali kupitia mipango ya bajeti ya kila mwaka. Utekelezaji unafanyika na unaendelea mpaka mwezi Juni, 2025 ambapo ndio mwisho wa mwaka huu wa fedha kwa hiyo, ahadi zote ambazo zimetolewa zinatarajiwa kutekelezwa katika kipindi hiki kwa zaidi ya 90%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho. Wakati nahitimisha Hoja hii ya Waziri Mkuu, naomba nitumie nafasi hii kuzungumzia masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikiko kwenye sekta ya michezo; sote ni mashahidi, katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naongeza dakika 30.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya michezo imepata mafanikio makubwa. Michezo inapendwa na Watanzania walio wengi na imekuwa ni chachu ya maendeleo na nguzo muhimu kwa ustawi wa jamii pamoja na kuitangaza nchi yetu Kimataifa na kuliletea sifa Taifa letu. Wabunge watakubaliana nami kwamba, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni mpenda michezo na amekuwa mstari wa mbele kusimamia ukuaji wa Sekta ya Michezo, maono na maelekezo yake yameleta mchango mkubwa na mafanikio katika sekta hii. Aidha, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa kinara katika kuongeza hamasa kwa wanamichezo wetu. Suala ambalo limechangia kuimarika kwa nafasi ya Taifa kwenye michezo mbalimbali ya Kimataifa hususan kwenye ngumi, riadha na mpira wa miguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa hamasa kubwa anayoitoa katika Sekta ya Michezo pamoja na kuhamasisha wadau mbalimbali kuchangia timu zetu, ili ziweze kufanya vizuri. Kama mtakumbuka, kupitia "Goli la Mama" mafanikio makubwa yamepatikana katika Mchezo wa Mpira wa Miguu. Katika hili, Mama amefanya mambo makubwa na kwa lugha ya sasa, "Ameupiga Mwingi na Apewe Maua Yake". *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, jitihada za Mheshimiwa Rais zimewezesha Vilabu vyetu vya Mpira wa Miguu kuendelea kung'ara Kimataifa. Katika Msimu wa Ligi wa 2023/2024, Tanzania imekuwa nchi pekee iliyoingiza timu mbili kwenye hatua ya Robo Fainali ya Mashindano ya Klabu Bingwa ya Afrika. Hatua hii ni ya kupongezwa na kujivunia kama Taifa. Hongera sana wachezaji wetu, hongera sana viongozi wa vilabu, hongera sana timu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii kuvipongeza Vilabu vya Yanga na Simba kwa kufikia hatua ya robo fainali. Nawapongeza sana kwa kucheza mpira wa viwango vya hali ya juu. Michuano yote ilikuwa mikali na kwa yeyote anayefahamu mchezo wa mpira wa miguu atakubaliana nami kwamba,

wachezaji wetu walionesha umahiri mkubwa, viwango vya hali ya juu na waliweza kukonga mioyo ya washabiki wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao, ama kwa hakika wanalitendea haki jukumu la kuishauri Serikali, la kuwawakilisha wananchi pamoja na kuhakikisha kwamba, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 imetekelezwa kama ilivyoelekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kutoa rai kwa Watanzania wote kuendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Serikali yake. Dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Mama Samia ni safi ambayo ni kuwaletea maendeleo ya haraka Watanzania wote. Jitihada kubwa anaendelea kuzifanya hivyo basi, Watanzania wote tumpe ushikiano unaohitajika ili aweze kufanikisha utekelezaji wa maono, mipango na mikakati ya kuinua ustawi wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo yote, sasa naomba Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi zilizo chini yake na Mfuko wa Bunge kama ilivyowasilishwa katika Hoja yangu ya tarehe 3 Aprili, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu, hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA J. MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na Kitabu cha Pili – Matumizi ya Kawaida. Sasa Kamati yako ijielekeze Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu kwenye vishikwambi ni ukurasa wa 23.

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*....................................Sh. 11,040,986,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tupo kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri Mkuu na tuna majina mawili. Tunaanza na Mheshimiwa Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Naomba kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa tatizo la madawa ya kulevya ni suala la kidunia na tunaona tafiti nyingi zinafanyika duniani na hasa katika matumizi ya bangi, lakini baadhi ya nchi zimeruhusu matumizi mbalimbali hasa katika tiba. Je, ni upi mtazamo wa Serikali yetu ukilinganisha na mtazamo wa kidunia katika kudhibiti madawa ya kulevya? Naomba nipate ufafanuzi na nisiporidhika nitashika shilingi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika ulimwengu kwa ujumla wake, mapambano dhidi ya dawa za kulevya

yanatawaliwa na mikataba mitatu mpaka sasa. Mkataba wa kwanza ni wa mwaka 1961 unahusu *Narcotic Drugs*, Mkataba wa pili ni wa mwaka 1971 unahusu *Psychotropic Drugs* na Mkataba wa tatu ni wa mwaka 1988 huo unahusu usambazaji na biashara nzima ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba wa mwaka 1961 wa *Narcotic Drugs* uliamua kutengeneza majedwali manne ambayo yanatambua aina mbalimbali ya dawa za kulevya. Jedwali la kwanza linaitambua bangi, *heroin* na *cocaine* kama dawa ambazo zinauraibu mkubwa. Jedwali la pili na jedwali la tatu ni dawa za tiba, lakini jedwali la nne lilikuwa limeweka tafsiri ya dawa ambazo zinauraibu mkubwa lakini zinaweza kutumika kama tiba na katika jedwali hilo bangi ilikuwa ni dawa ambayo ilitajwa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hivi karibuni kumekuwa na *movement* kubwa ya kuifanya bangi ifanyiwe utafiti na ipewe kibali cha kulimwa ili iwe tiba. Kamisheni ya *Narcotic Drugs* ya 67 ilipoketi iliamua kutengeneza utaratibu wa kuzihoji Nchi Wanachama ambazo ni 53 zitoe maoni kuhusiana na bangi kuondolewa kwenye jedwali la nne ambalo lilikuwa linaifanya bangi kuwa ni dawa yenye madhara makubwa lakini inayoweza kutumika kama tiba. Kwa hiyo nchi zile 53 zilipiga kura, nchi 27 zilikubali bangi iondolewe kwenye jedwali la nne, nchi 25 zilikataa na nchi moja ili-*abstain*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo baada ya upigaji kura huo, ikaamuliwa bangi iondolewe kwenye jedwali la nne na hivyo ikaruhusiwa ifanyiwe tafiti na iruhusiwe kulimwa. Baada ya kibali hicho sasa kwenye Kamisheni ya 67 na Ripoti ya Hali ya Dawa za Kulevya Ulimwenguni ya mwaka 2023 imeonekana zile nchi ambazo zilianza kulima bangi kwa kibali cha kuzalisha bangi kwa ajili ya tiba, 40% ya hizo nchi zimeripoti kwamba wananchi wake kwenye mataifa hayo wameongeza idadi kubwa ya matatizo ya afya ya akili lakini kumeongezeka pia na uhalifu *(crime)* kwenye nchi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, 60% ya dawa zinazolimwa kwa kibali hicho kwenye Nchi za Afrika imeonekana 60% ya uzalishaji wa bangi hauna soko na bangi hiyo haijanunuliwa mahali popote. Kwa hiyo ni kama 40% tu ndiyo iliyonunuliwa. Bangi hiyo sasa imeanza kutengenezwa kwa mfumo mpya wa aina ya bangi kama dawa ya kulevya inayoitwa *skanka*, ambayo ni dawa kali sana. Hivi karibuni hiyo *skanka* katika Nchi za Afrika imeonekana, hata ndani ya Tanzania imeanza kuingia ni kama mabaki kwenye hizo asilimia 60 ya *production* ambayo haijanunuliwa kwenye nchi hizo ambazo zimeruhusiwa kulima bangi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kinachojitokeza hapa ni kwamba ruhusa imetolewa nchi hizo zimeanza kulima, lakini matumizi ya hiyo bangi kupeleka kwenye tiba ni madogo. Kwa hiyo bangi nyingi imeendelea kubaki na kutengenezwa na sasa hivi imeanza kutoroshwa ili iuzwe kama dawa haramu kwa matumizi ya binadamu na kuendelea kuleta madhara makubwa. Mpaka nchini Tanzania tumeanza sasa kuona tunapokea hizo *skanka* ambayo ni mabaki ya bangi iliyolimwa kwenye kibali lakini haijanunuliwa. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge ni sisi wenyewe kuamua kama kweli tunataka kufika kwenye hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokifikiria ni kuanza kuwasiliana na vyuo vikuu vyetu kuanza kufanya hizo tafiti, lakini mjadala wa kuikubali nchi iingie katika kibali cha kulima bangi na utafiti wa namna moja ama nyingine ni lazima tuwe na makubaliano ya pamoja; ni lazima kama nchi tufanye kwanza tafiti ili tuweze kufanya maamuzi hayo. Waheshimiwa Wabunge, bangi mpaka sasa kama Taifa tunaiona ni dawa ambayo ina madhara makubwa sana. Inaharibu sana afya za vijana wetu, nimesema vijana karibu milioni 20 ndio nguvu kazi kwenye *population* yetu ya milioni karibu 60 na kitu. Sasa wakiharibika hawa vijana nadhani tutakuwa tumeharibu nguvu kazi kubwa. Kwa hiyo ni jambo ambalo halitakiwi kufanyiwa maamuzi kwa haraka, Serikali ijipe muda, ifanye kazi ya tafiti za kutosha na ifanye maamuzi ambayo yatakuwa ni maamuzi kweli yenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tulizonazo huenda mwaka huu mwezi Septemba kukafanyika tena Mkutano mkubwa wa Kamisheni hiyo ya *Narcotic Drugs* ambayo inasimamiwa na Mkataba huo wa mwaka 1961 na huenda mkutano huo ukafanyika hapa Zanzibar, lakini mjadala mkubwa ni kuitazama bangi kama inaweza kuendelea kutolewa kibali kulimwa kwa ruhusa na kuendelea kutumika. Kwa hiyo tupo hapo na kama Taifa ni lazima tusikimbie katika jambo hili, ni lazima tutulie na tufanye maamuzi ambayo kwa kweli yanaweza kuwa na tija kubwa kwenye Taifa letu kwa kuzingatia tulivyojifunza kutoka kwenye mataifa mengine na mwenendo mzima wa uzalishaji wa bangi na matumizi ya bangi kama dawa ya kulevya na tiba kama ilivyoelezwa kwenye mkataba husika. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika na ufafanuzi wa Serikali. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nisiporidhika nitashika shilingi. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 14 imezungumzia kuhusu haki ya kuishi. Kwa maana ya kila Mtanzania ana haki ya kuishi na kupata hifadhi ya maisha yake kutoka katika jamii kwa mujibu wa sheria. Sanjari na Sheria ya mwaka 1984 imezungumzia kuhusu haki ya uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mwendelezo wa matukio ambayo unakuta Watanzania aidha wamekosa au hawajakosa lakini wanapewa hukumu ya kifo badala ya kupelekwa kwenye vyombo vyetu vya dola na kusikilizwa na kuhukumiwa kwa mujibu wa sheria. Matukio haya yamekuwa yakitokea kwa baadhi ya Askari wa vyombo vya dola, imetajwa hapa ambao wanazunguka kwa wananchi wanaozunguka hifadhi, kwa wananchi waliopo kwenye mipaka, aliongea hata Mbunge wa Kyela hapa na kule kwetu Sirari haya mambo yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea pia kuona mwendelezo wananchi wakipigwa risasi na kufariki kwenye migodi na Askari wa Jeshi la Polisi ambao wanalinda migodi mbalimbali Tanzania. Kwa hiyo nataka nijue ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba unakomesha kabisa kadhia hii ya mauaji, kulemazwa, kutaifishwa mali ambako kunafanywa na watu hawa dhidi ya Watanzania hawa? Pia kuchukua hatua stahiki kwa hawa ambao wanatuhumiwa ili kuweza kukomesha sambamba na kuwalipa fidia wahanga hawa ambao wamekuwa wakipitia haya madhila kwa muda wote. Nisiporidhika nitashika shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa suala la Mheshimiwa Esther, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Esther amezunguka sana hakuwa na hoja *specific*, kwa sababu suala la polisi kushiriki katika kutoa uhai wa mtu linahitaji uthibitisho siyo jambo ambalo linaweza likatolewa kijuu juu kama hivi. Sheria ya Jeshi la Polisi inataka polisi isimamie ulinzi wa raia na mali zao na hiyo ndiyo kazi ambayo inafanya kila siku, siyo kutoa uhai wa raia na haifanyi hivyo. Kama kuna matukio ambayo *specific* labda yametokea isivyo bahati polisi amesababisha kifo cha mtu ni vizuri tukapata kujua *exactly* tukio lenyewe likoje ili tulifanyie uchunguzi. Mazingira ambayo polisi yanamfanya aweze kutumia nguvu ya kadri inategemea na mazingira ambayo polisi wanaruhusiwa kutumia njia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana pengine tukio hilo limetokea katika mazingira kama hayo, inawezekana pengine wakati ambapo polisi ametumia nguvu ya kadri ya ziada ikaweza kusababisha madhara kwa raia, inaenda sambamba na matakwa ya kisheria. Kwa hiyo, nahisi siyo busara kwa Mheshimiwa Mbunge ku-*generalize* kuhusu tatizo la mtu mmoja ama tatizo la jambo ambalo halijathibitishwa. Kwa hiyo sijui

Mheshimiwa Esther Matiko, anakusudia nini anapozungumzia Jeshi la Polisi linaua raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja ya Mgodi wa Geita, jambo hili tayari tumeshalifanyia uchunguzi na ripoti yake itakavyokuwa tayari itawasilishwa, lakini kimsingi tofauti kabisa na Mheshimiwa Mbunge ambavyo anazungumza, jambo hili limetokana na uvamizi wa wananchi katika mgodi ule ambao ulisababisha madhara hayo na polisi wakachukua hatua ya kujihami kwa tukio moja. Sasa tukio moja ambalo linaweza kuwa *justified* baada ya kufanyia uchunguzi, haliwezi kuhalalisha Mbunge akasema Jeshi la Polisi kazi yake linaua raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Mbunge awe makini sana anapozungumzia masuala yanayogusa vyombo vya usalama, vyombo hivi vya usalama vipo hapa kwa ajili ya kulinda raia na wanafanya kazi hiyo kwa kweli kwa jitihada kubwa sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Matiko, ripoti ya mgodi ambao uliuzungumzia Geita, Mheshimiwa Waziri amesema ripoti yake ikikamilika itakuja.

*(Hapa Mhe. Esther N. Matiko alizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** *Don't interrupt me*, nitakutoa nje sasa hivi. Usiniingilie wakati mimi nasema, uwe na adabu ndani ya Bunge. Mnapenda sana kufanya utovu wa nidhamu muonekane kwa wananchi mnawatetea wakati wala hufuati Kanuni za Bunge.

Sasa sikiliza, takribani siku tano au sita zilizopita ulileta na ukachangia hapa kwenye mjadala huu wa Mheshimiwa Waziri Mkuu na ukawasilisha vielelezo kwenye meza yangu na vielelezo vyako vimekabidhiwa Serikalini viende vikafanyiwe kazi kuthibitisha hayo unayoyasema au hayo unayoyaleta yana ukweli au hayana ukweli. Kwa maana hiyo ripoti ya Serikali ya hayo uliyosema ya Serengeti pamoja na migodi zitaambatanishwa pamoja kuletwa kwenye Bunge.

*(Hapa Mhe. Esther N. Matiko alizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Unaendelea kunisemesha? Kwa nini mnakuwa namna hiyo lakini, hivi huko nyumbani hamnini? *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo nikuombe, kwa mujibu wa kanuni unayo haki ya kusimama tena baada ya maelezo haya, lakini nakwambia ripoti zote hizo zitaletwa kwenye Kiti na zitawasilishwa ndani ya Bunge kwa mwongozo tuliyotoa.

Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesikitika tu alichokijibu Mheshimiwa Waziri, sijaridhika. Kwenye hoja yangu nimetanabahisha nikaonesha hifadhini, migodini na mipakani. Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum alichangia hapa akaonesha jinsi Jeshi la Wananchi linavyotuhumiwa mpakani kule, lakini Mbunge wa Mbarali alishawahi kuleta hapa hoja, Serikali ikaunda *so called* Kamati wakaenda vikaendelea. Pia nimezungumzia mgodi siyo hata Geita, sija-*cite* hata Geita, ningekuwa na-*cite* hapa ningei-*cite* Nyamongo ambapo ndani ya miezi mitatu raia zaidi ya 14 wameuawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikasema Serikali ije na mkakati kwa sababu hii pia inaondoa imani kwa Serikali dhidi ya wananchi na nipo hapa kuishauri Serikali ili tukomeshe mauaji *once and for all* na nimeongea *so humbly* leo. Kwa hiyo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mbona hamtoshi? Haya Mheshimiwa Hawa, wanaochangia nani na nani? Anatropia, Makamba, Waziri wa Mambo ya Ndani, Waziri wa Sheria, Waziri wa Ulinzi, Naibu Waziri wa Utalii na Kilumbe Ng'enda. Tunaanza na Anatropia. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, hoja aliyoileta mezani Mheshimiwa Matiko ni suala zima la *impunity*. Ameanza ku-*cite* haki ya msingi

ya raia ambayo ni kuishi, ni haki ambayo mtu anazaliwa nayo, tunaita *inalienable*. Haiwezi kuondolewa ni haki ambayo Mungu ameitoa lakini aka-*cite* Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo ina-*comprehend* hiyo haki ya kuishi ambayo imetolewa na Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba yetu inazuia hivyo vifo lakini akaeleza kumekuwepo matukio kadha wa kadha na mimi nilichangia humu Bungeni nikieleza matukio ya kuua watu ambayo yamekuwa hayachukuliwi hatua. Kwa hiyo tunachokiongelea hapa ni namna gani tunaweza kuachana na *issue* inayoitwa *impunity*. Mtu anaweza kuua mtu, anaweza kuchukua sheria mkononi, anaweza kukosea lakini akaendelea na maisha kama kawaida. Tunataka mkakati sasa tujue Serikali imejiandaaje kukomesha kitu kinachoitwa *impunity*? Mtu atakayetoa uhai wa mtu bila sababu sheria ichukue mkondo wake, ndiyo hicho tunachotaka kukisema. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka niongezee kwenye hoja ya Mheshimiwa Matiko. Kwanza Mheshimiwa Matiko haongelei polisi peke yake, anaongelea Jeshi kwa kumaanisha Jeshi Usu, Jeshi wanaoshughulika na mambo ya wanyamapori. Tangu 2015 nimeingia humu Bungeni kelele iliyopo humu ya Wanajeshi hawa wanaohusika na wanyamapori kuvamia watu, kuchukua mifugo yao, kuingiza kwenye hifadhi, kuuza kwa bei rahisi na kuwaacha hawa watu maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zilishaundwa Kamati nyingi sana kuhusiana na jambo hili. Ni lazima tufike mwisho kutatua changamoto ya watu wa maliasili kupanua mipaka, ardhi za vijiji na kuziongezea kuwa eneo la hifadhi, wananchi wanakosa maeneo, matokeo yake wanaenda kuchunga kwenye maeneo ambayo Jeshi hili la Wanyamapori linasema ni ya kwao. Wakiingia humo ni vita, imekuwa ni mauaji, wananchi wanapigana na Serikali yao. Hayo yote yanasababishwa na kutokuwa na majibu

sahihi ya mipaka ya maeneo ya hifadhi ambayo yanaongezeka kila siku na kupora ardhi za kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tupate majibu ya namna ambavyo wawekezaji wanapewa maeneo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** …na kuwanyanganya wananchi maeneo yao… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naomba nisisitize juu ya umuhimu wa kwanza kuwa makini sana tunapozungumzia mambo yanayohusu vyombo vya dola, ambapo vyombo hivi ndiyo vinavyotusababishia tukawa na amani, tukaweza kufanya shughuli zetu bila tatizo, vyombo hivi vimekuwa vikijitahidi kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tutambue kwamba, nasi Waheshimiwa Wabunge tunalo jukumu la kujaribu kuwasihi sana wananchi kufuata sheria. Kwa mfano, Polisi anapokuwa na silaha anatakiwa ajilinde kwanza yeye mwenyewe, alinde na raia wengine. Sasa mazingira yoyote ya kuhatarisha maisha yake na raia wengine itategemea katika mazingira hayo kwa mujibu wa *CPA* yapoje? Kama wananchi wametoka na silaha, panga na shoka wanamfuata Polisi kwa ajili ya kumdhuru yeye mwenye silaha ana haki ya kujilinda, sasa kama mazingira kama hayo yametokezea, si matukio mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya uchunguzi, kwa mfano tunafanya uchunguzi wa kina ndiyo maana umesema vizuri kwamba, kwa hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wana wasiwasi nazo, mara ya mwisho wakati nimezungumza katika Bunge hili nilisema kwamba, kuna matukio yalikuwa yamezungumzwa yanahusisha Polisi na mauaji, nikasema tumeyafanyia uchunguzi na matukio mengi hayakuwa chanzo ni Askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matukio kama saba ama nane ambayo tuliona haya kuna haja ya kuyaundia Tume, tuliunda Tume na mpaka sasa hivi kwa yale matukio mengine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri muda wako tayari.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio haya tumeyaundia Tume na Tume ile inafanya kazi yake vizuri. Kuhusiana na hizi hoja ya masuala haya mawili ambayo yamezungumzwa nilieleza hapa mwanzo, ndiyo maana nikamtaka Mheshimiwa Mbunge awe na hoja mahsusi kama ni hoja ya migodi imeshafanyiwa uchunguzi na taarifa yake kama ulivyosema itawasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna sehemu ambayo imeonekana na amejiridhisha kweli kuna makosa ya Polisi hatua zitachukuliwa na tunafanya hivyo. Kama kuna sehemu ambayo makosa ni ya raia itakuwa wazi, hatupo hapa kumlinda Askari ambaye amefanya makosa, lakini ni lazima tuwatendee haki askari, kwa sababu hawa ndiyo wanaolinda amani kuwatengenezea taswira kwamba, wao ni wauaji si sawa! Hili ni jambo ambalo halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi wanayofanya hawa ni kubwa na mazingira wanayofanyia kazi vilevile ni magumu. Kwa hiyo, kwa hoja hiyo, niendelee kukubaliana na maelekezo yako uliyotoa kwamba wasubiri taarifa ile ambayo imefanya uchunguzi

kwa maelekezo ya Bunge, itatoa uhakika juu ya hali ya matukio ya migodini ambayo *specifically* yamegusa Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa *Engineer* Masauni, hapa yameelezwa mambo ya kiujumla ambayo ni vigumu kuelewa ni nini hasa kinaongelewa? Kama ulivyosema hoja ya kwanza ilivyowasilishwa ulishaitolea maelezo na sipendi kurudia maneno yako kwa sababu umeshaeleza kwa ufasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Matiko wakati anaongea amerejea hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, ambayo pia hoja hiyo ilikwishatolewa maelezo na Kiti chako kwamba Mheshimiwa Mbunge alete uthibitisho na bado tunasubiri uthibitisho huo atuletee ili tuweze kuona kama kweli kuna hayo anayosema kwamba, kuna *impunity* ambayo sidhani kama Serikali inafanya kazi kwa njia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vya ulinzi na usalama ni vyombo ambavyo vimepewa dhamana kubwa sana ya kuwalinda wananchi wake. Vinafanya kazi katika mazingira ya aina zote hata magumu kuhakikisha kwamba, wananchi wake wapo salama. Hili la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum pamoja na kwamba hajaleta uthibitisho, lakini napenda kueleza kwamba, iliundwa Kamati na Kamati hiyo ilihusisha vyombo vya ulinzi mbalimbali kwa ajili ya kudhibiti utoroshaji wa kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hiyo iliundwa na Mkuu wa Wilaya na imefanya kazi yake vizuri sana. Kama alivyosema Mheshimiwa *Engineer* Masauni, bahati mbaya sana aliyetakiwa kulalamika kama ni kulalamika ilikuwa ni Polisi na hao Wanajeshi wanatuhumiwa, kwa sababu wananchi walikwenda kuwavamia Polisi na wananchi walienda kuwavamia Wanajeshi, walikwenda na pikipiki, walikwenda na silaha za jadi, lakini hawakudhuriwa hata kidogo, Askari wetu walikuwa wastaarabu wakawa sambaza

wakaendelea na kazi yao na utoroshaji wa kahawa ulidhibitiwa na haukuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lilikuwa bei, sasa hivi Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imehakikisha kwamba wakulima wanapata bei nzuri. Kwa hiyo, hili suala la kwamba, kuna Askari, kuna Wanajeshi, kuna Askari Usu, walivamia walishambulia watu si suala la ukweli lakini kama ulivyokuwa umeelekeza tangu mwanzo, kama anao uthibitisho, basi tutasubiri alete huo uthibitisho wake na Serikali italiangalia suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri wa Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, tarehe 8 Aprili, Kiti chako kilitoa maelekezo baada ya kupokea maelezo ya Mheshimiwa Mbunge ndani ya Bunge lako Tukufu. Ulitoa maelekezo kwa Serikali twende tukazifanyie kazi hoja zilizozungumzwa. Kabla hatujapokea maelekezo, Serikali ilitoa maelezo jinsi ambavyo tumekuwa tukishughulikia jambo hili kwa taarifa zilizokuwa zimepita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelekezo yako yale, Serikali imeunda timu ya vyombo vyetu vya usalama, timu *independent* na hivi tunavyozungumza timu hii ipo uwandani inafanya kazi. Sitaki kuamini kwamba, Bunge hili linaweza kufanya maamuzi ya kudharau vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, sitaki kuamini kwamba, Bunge hili linaweza kufanya maamuzi ambayo hayajafanyiwa kazi na mchakato ukafika mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nchi hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu na nchi hii inaheshimu uhai wa Watanzania. Niwaombe sana kama Taifa tukifika mahali kila anayelalamika tukaamini anacholalamika ni sawa, tukaacha mifumo ya kutafuta haki ikafanya kazi yake sawasawa, nadhani tutaingia kwenye matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana tukubaliane, timu hii inayofanya kazi iachiwe muda ifanye kazi ikamilishe. Naamini hakuna yeyote atakayekuwa amekiuka sheria za nchi hii akaachwa abaki salama. Naomba tupewe muda tuweze kufanyia kazi. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Matiko, kama utakumbuka kama nilivyosema mwanzo nakukumbusha tena, vielelezo vyako vinafanyiwa kazi *commitment* ya Serikali umeisikia kuna Tume inafanya kazi, *commitment* ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais aliunda Tume Maalum ya Haki Jinai kuondoa uonevu kwa wananchi wake. Ile Kamati ilipewa miezi mitatu, wakaomba waongezewe miezi mitatu, Mheshimiwa Rais akaridhia kuwaongezea ili kuwe na taarifa sahihi ya matukio yote ya uhalifu kwenye Taifa letu. Mheshimiwa Rais anayaona na Serikali inayaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Matiko sasa nakurudishia kwa mujibu wa Kanuni ufunge hoja yako. Hoja hii ina vitu viwili, ukubaliane na maoni kwa sasa unarudisha shilingi ya Waziri Mkuu, tunasubiri maamuzi au kama hutaki tunaendelea na hatua ya pili ya kupiga kura.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa mwongozo wako wa siku ile ya tarehe 8 Aprili, ila tu nikupe taarifa baada ya kutoa tu yale maelekezo tarehe 13 Aprili kijana anayeitwa Timas Zakaria aliuawa Serengeti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko sikiliza Mwongozo na maelekezo ya Kiti. Kwa mujibu wa Kanuni una nafasi mbili za maamuzi, kwanza kukubaliana na Tume ambayo inafanya kazi, ipo kazini sasa hivi. Pili, uendelee na haki yako ya kuishika shilingi na tupige kura. Hakuna mjadala mwingine, hakuna taarifa nyingine.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nilikuwa nataka kueleza kwa sababu Tume iliyoundwa ni ya Hifadhi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia *content* tatu hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko, nakuomba usipende kuwa *object of pity*, nimekwambia kwamba kwa mujibu wa Kanuni una haki mbili, kukubaliana na maelezo ya Serikali urudishe shilingi tuendelee au unasema sikubali naendelea kuishika shilingi ni mawili tu, ndiyo haki yako ya kikanuni ya Bunge.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudisha shilingi maelezo ya Serikali, wananchi wameyasikia, watapima waone nini kinaenda kufanyika.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaingia kwenye *guillotine*.

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 37- Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*..................Sh.11,040,986,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*..............Sh. 2,076,678,800
Kifungu 1003 - *Policy & Planning Unit*........................Sh. 1,106,335,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*.................................Sh. 386,631,000
Kifungu 1005 - *Government Communication Unit*......Sh. 332,289,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*.........Sh. 522,788,000
Kifungu 1007- *Legal Services Unit* ................................Sh. 296,079,000
Kifungu 1008 - *Management Information System Unit*……………………………….. Sh. 328,829,000
Kifungu 2001- *Civil Affairs and Contingencies*..........Sh. 2,975,541,000
Kifungu 2002 - *National Festivals*.................................Sh. 843,463,000
Kifungu 3001- *Parliamentary and Political Affairs*........Sh. 962,524,000
Kifungu 4001 - *Private Sector Development and Economic Empower*..........................Sh. 7,903,387,200

Kifungu 5001 - *Coordination of Government Business*……………………………….Sh. 1,122,152,000
Kifungu 5002 - *Performance, Monitoring and Evaluation Division*............................Sh. 1,069,336,000
Kifungu 7001- *Government Printer*...........................Sh. 2,886,960,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 15 - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…...............Sh. 1,892,611,969
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.................Sh. 344,413,520
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Division Unit*.........................................Sh. 230,698,754
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*................................Sh. 212,341,700
Kifungu 1005 – *Information, Communication and Technology Unit*…...............................Sh. 210,181,822
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*........Sh.132,467,167
Kifungu 2001 – *Mediation*........................................Sh. 1,685,395,274
Kifungu 2002 – *Arbitration*........................................Sh. 1,347,126,970
Kifungu 2003 – *Dodoma Regional Office*......................Sh. 13,561,815
Kifungu 2004 – *Lindi Regional Office*...............................Sh. 3,240,000
Kifungu 2006 – *Ruvuma Regional Office*.........................Sh. 3,240,000
Kifungu 2007 – *Kigoma Regional Office*..........................Sh. 3,000,000
Kifungu 2008 – *Iringa Regional Office*............................Sh. 26,040,000
Kifungu 2009 – *Njombe Regional Office*.........................Sh. 3,600,000
Kifungu 2010 – *Geita Regional Office*.............................Sh. 3,000,000
Kifungu 2011 – *Mara Regional Office*..............................Sh. 3,600,000
Kifungu 2012 – *Singida Regional Office*..........................Sh. 3,000,000
Kifungu 2013 – *Kagera Regional Office*..........................Sh. 3,960,000
Kifungu 2014 – *Shinyanga Regional Office*......................Sh. 4,800,000
Kifungu 2015 – *Katavi Regional Office*............................Sh. 3,240,000
Kifungu 2016 – *Tabora Regional Office*...........................Sh. 3,240,000
Kifungu 2017 – *Mbeya Regional Office*.........................Sh. 14,161,815
Kifungu 2018 – *Arusha Regional Office*.........................Sh. 22,271,815
Kifungu 2019 – *Mtwara Regional Office*..........................Sh. 3,000,000
Kifungu 2020 – *Pwani Regional Office*............................Sh. 6,480,000

Kifungu 2021 – *Tanga Regional Office*............................Sh. 4,440,000
Kifungu 2022 – *Mwanza Regional Office*.......................Sh. 20,871,815
Kifungu 2023 – *Songwe Regional Office*..........................Sh. 3,120,000
Kifungu 2024 – *Manyara Regional Office*........................Sh. 3,240,000
Kifungu 2025 – *Dar es Salaam Regional Office*............Sh. 89,631,564
Kifungu 2026 – *Rukwa Regional Office*...........................Sh. 3,000,000
Kifungu 2028 – *Kilimanjaro Regional Office*.....................Sh. 3,000,000
Kifungu 5005 – *Morogoro Regional Office*.......................Sh. 3,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 25 - Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*................Sh. 26,191,548,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 27- Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*....................Sh. 967,768,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*................Sh. 317,997,000
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring, Evaluation and Research Unit*……..................................Sh. 261,467,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*................................Sh. 264,407,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*........Sh. 237,451,000
Kifungu 1006 – *Information and Communication Technology Unit*...................................Sh. 517,935,000
Kifungu 1007 – *Communication and Civic Education Unit*………………………….Sh. 211,965,000
Kifungu 1008 – *Registration of Political Parties Division*……………………………………....Sh. 835,767,000
Kifungu 1009 – *Election Expenses and Civil Education*........................................Sh. 19,285,812,000
Kifungu 1010 – *Monitoring of Political Parties Unit*....Sh. 1,586,662,000

Kifungu 1011 – *Zanzibar Office*......................................Sh. 354,710,000
Kifungu 1012 – *Legal Services Unit*............................... Sh. 197,832,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 42- Mfuko wa Ofisi ya Bunge**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*……………......Sh. 15,506,573,309
Kifungu 1002 – *Library and Research Division*..............Sh. 744,462,000
Kifungu 1003 – *Information and Communication Technology Unit*……………………....Sh. 2,001,236,000
Kifungu 2001 – *Budget Division*...................................Sh. 3,397,411,800
Kifungu 2002 – *Table Office Division*......................Sh. 113,327,911,000
Kifungu 2003 – *Parliamentary Committees Division*…………………………………Sh. 18,581,513,000
Kifungu 2004 – *Hansard Unit*.......................................Sh. 1,376,620,000
Kifungu 2005 – *Legal Services Division*.......................Sh. 2,938,732,000
Kifungu 3001 – *Private Office of The Speaker*...........Sh. 1,743,129,000
Kifungu 3002 – *Private Office of The Deputy Speaker*..................................................Sh. 837,406,000
Kifungu 3004 – *Private Office of The Clerk*...............Sh. 1,620,764,000
Kifungu 3005 – *Finance and Accounts Unit*................Sh. 998,796,000
Kifungu 3006 – *Communication and International Relations Unit*.......................................Sh. 6,124,648,892
Kifungu 3008 – *Internal Audit Unit*.................................Sh. 626,945,000
Kifungu 3009 – *Procurement Mgt Unit*..........................Sh. 862,771,000
Kifungu 3010 – *Defense and Security Unit*.................Sh. 1,061,538,999
Kifungu 3012 – *Zanzibar Office*.....................................Sh. 373,965,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 61- Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..................Sh. 4,147,337,000

Kifungu 1002 – *Planning Monitoring and Evaluation*……………………………….Sh. 535,254,000
Kifungu 1003 – *Finance and Planning Unit*..................Sh. 625,328,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*................................Sh. 454,127,000
Kifungu 1005 – *Legal Services* .....................................Sh. 525,292,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management and Logistics Unit*..........................................Sh. 569,996,000
Kifungu 1007 – *Zanzibar Office*.....................................Sh. 355,386,000
Kifungu 2001 – *Election Management Division*...........Sh. 742,173,000
Kifungu 2002 – *National Voters Registration and Information Communication Technology Division*…………………….Sh. 935,512,000
Kifungu 2003 – *Voters Education and Public Information Division*...............................Sh. 830,496,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 65 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..................Sh. 3,933,644,557
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*................Sh. 487,920,828
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*......................Sh. 827,181,457
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*..................................Sh. 326,996,692
Kifungu 1005 - *Procurement Management Unit*.........Sh. 346,738,946
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*.....Sh. 179,685,759
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*....................................Sh. 285,947,968
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit*...............................Sh. 281,456,972
Kifungu 1009 - *Monitoring and Evaluation Unit*............Sh. 99,073,316
Kifungu 2001 – *Labour Division*..................................Sh. 8,296,560,421
Kifungu 2002 – *Employment Division*............................Sh. 697,932,000
Kifungu 2003 – *Registrar of Trade Unions*.....................Sh. 198,548,526
Kifungu 2004 – *Arusha Regional Labour Office*...........Sh. 90,731,414
Kifungu 2005 – *Dodoma Regional Labour Office*........Sh. 80,731,414
Kifungu 2006 – *Geita Regional Labour Office*...............Sh. 33,649,217
Kifungu 2007 – *Iringa Regional Labour Office*...............Sh. 76,353,386

Kifungu 2008 – *Kagera Regional Labour Office*............Sh. 60,081,417
Kifungu 2009 - *Kigoma Regional Labour Office*............Sh. 66,513,619
Kifungu 2010 – *Kilimanjaro Regional Labour Office*......Sh. 69,921,184
Kifungu 2011 - *Lindi Regional Labour Office*..................Sh. 45,838,231
Kifungu 2012 – *Manyara Regional Labour Office*.........Sh. 51,056,746
Kifungu 2013 – *Mara Regional Labour Office*................Sh. 53,364,940
Kifungu 2014 – *Mbeya Regional Labour Office*..........Sh. 112,462,678
Kifungu 2015 – *Morogoro Regional Labour Office*.......Sh. 79,434,736
Kifungu 2016 – *Mtwara Regional Labour Office*...........Sh. 83,812,766
Kifungu 2017 – *Mwanza Regional Labour Office*........Sh. 153,735,132
Kifungu 2018 – *Njombe Regional Labour Office*...........Sh. 46,570,335
Kifungu 2019 – *Pwani Regional Labour Office*...........Sh. 116,503,694
Kifungu 2020 – *Rukwa Regional Labour Office*............Sh. 63,002,536
Kifungu 2021 – *Katavi Regional Labour Office*.............Sh. 44,678,754
Kifungu 2022 – *Ruvuma Regional Labour Office*..........Sh. 63,488,984
Kifungu 2023 – *Shinyanga Regional Labour Office*......Sh. 79,335,016
Kifungu 2024 – *Simiyu Regional Labour Office*.............Sh. 52,678,754
Kifungu 2025 - *Singida Regional Labour Office*............Sh. 71,380,528
Kifungu 2026 – *Tabora Regional Labour Office*............Sh. 87,812,728
Kifungu 2027 – *Tanga Regional Labour Office*.............Sh. 90,349,552
Kifungu 2028 – *Temeke Regional Labour Office*.........Sh. 109,543,991
Kifungu 2029 – *Kinondoni Regional Labour Office*.......Sh. 97,326,280
Kifungu 2030 – *Ilala Regional Labour Office*................Sh. 104,084,689
Kifungu 2031 – *Social Security Division*.........................Sh. 657,838,705
Kifungu 2032 – *Youth Development*..........................Sh. 1,729,294,781
Kifungu 2033 - *Employment Services Unit* ...................Sh. 966,417,947
Kifungu 2034 – *Persons with Disability Unit*.................Sh. 1,898,242,000
Kifungu 2035 – *Productivity Promotion Unit*..................Sh. 478,484,414

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 91- Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

Kifungu 1001 – *Corporate Services Division*………..Sh. 5,535,470,075
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*................Sh. 649,087,500
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*.................................Sh. 448,415,500
Kifungu 1005 – Legal Services Unit……………………Sh. 1,020,263,120

Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*…….Sh. 360,292,313
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*.....Sh. 465,483,876
Kifungu 2001- *Intelligence Division*……………………*Sh.* 1,691,039,386
Kifungu 3001- *Operations and Investigation Division*……………………………….….*Sh.* 2,321,614,832
Kifungu 4001- *Prevention and Treatment Division*…*Sh.* 1,663,153,963
Kifungu 5001- *Inspection and Forensic Sciences Division*………………………….*Sh.* 947,514,685
Kifungu 6001- *Zonal Offices* ……………………..…. *Sh.* 2,274,896,750

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti ya UKIMWI Tanzania**

Kifungu 1001- *Policy, Planning and Research*.............Sh. 576,132,000
Kifungu 1002- *Finance, Administration and Resource Mobilization*..........................Sh. 1,163,902,732
Kifungu 1003 - *Monitoring and Evaluation*...................Sh. 267,012,000
Kifungu 1004 - *Advocacy and Information Unit*..........Sh. 375,040,000
Kifungu 1005 - *National Response*................................Sh. 692,050,668
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*.........Sh. 248,574,000
Kifungu 1007- *Legal Services Unit*..................................Sh. 363,530,600
Kifungu 1008 - *Management Information Systems Unit*……………………………………...Sh. 238,160,000
Kifungu 1009- *Internal Audit Unit*....................................Sh. 278,693,000
Kifungu 1010- *Special Programs Unit*............................Sh. 242,580,000
Kif 1011- *Government Communication Unit*..................Sh. 96,808,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:** Sasa tunaingia katika Kitabu cha Nne, Miradi ya Maendeleo.

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu15 - Tume ya Usuluhishi na Uamuzi**

Kifungu 1005 - *Information, Communication and Technology Unit*....................................Sh. 460,077,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 27 - Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa**

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management*.....................................Sh. 0
Kifungu 1011- *Zanzibar Office* ....................................Sh. 940,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 37 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

Kifungu 2001- *Civil Affairs and Contingencies*.............................Sh. 0
Kifungu 5001- *Coordination of Government Business*…………………………………..Sh. 5,268,570,000
Kifungu 7001- *Government Printer*...........................Sh. 1,235,635,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 42 - Mfuko wa Ofisi ya Bunge**

Kifungu 1001 - *Administration & Human Resources Management Division*……………....Sh. 2,661,000,000
Kifungu 1003 - *Information and Communication Technology Unit*…..............................Sh. 4,045,470,000

Kifungu 2001- *Budget Division*......................................Sh. 974,340,000
Kifungu 3004 - *Private Office of The Clerk*.................Sh. 2,000,000,000
Kifungu 3006 - *Communication and International Relations Unit*....................................Sh. 9,680,810,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 61- Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi**

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Management*…..............Sh. 28,016,247,500
Kifungu1002 – *Planning, Monitoring and Evaluation Division*…..............................Sh. 350,000,000
Kifungu 1003 - *Finance and Accounts Unit*…..............Sh. 150,000,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*…..............................Sh. 72,280,000
Kifungu 1005 - *Legal Services Unit*…........................Sh. 3,704,250,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management and Logistics Unit*.......................................Sh. 1,249,880,000
Kifungu 1007- *Zanzibar Office*…...............................Sh. 1,092,850,000
Kifungu 2001- *Election Management Division*…..Sh. 120,538,280,500
Kifungu 2002 - *National Voters Registration and Information Communication Technology Division*……….............Sh. 6,162,600,000
Kifungu 2003 - *Voters Education and Public Information Division*............................Sh. 6,281,430,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 65 - Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.......................Sh. 346,309,740
Kifungu 1009 - *Monitoring and Evaluation Unit*….........Sh. 296,650,855
Kifungu 2001- *Labour*…..............................................Sh. 161,599,145
Kifungu 2002 - *Employment Division*….....................Sh. 7,881,665,972
Kifungu 2003 - *Registrar of Trade Unions*…...................Sh. 60,000,000
Kifungu 2031- *Social Security Division*…......................Sh. 519,675,000

Kifungu 2032 -*Youth Development*…...........................Sh. 991,802,013
Kifungu 2033 - *Employment Services Unit*…..............Sh. 2,469,398,599
Kifungu 2034 - *Persons with Disability Unit*…..............Sh. 1,689,286,666
Kifungu 2035 - *Productivity Promotion Unit*…................Sh. 75,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 91- Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

Kifungu 4001 - *Prevention and Treatment Division*...Sh.1,314,506,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 92 – Tume ya Kudhibiti UKIMWI**

Kifungu 1001- *Policy, Planning and Research*…............Sh. 94,100,000
Kifungu1002 - *Finance, Administration and Resource Mobilization*..........................Sh. 2,230,285,988
Kifungu 1003 - *Monitoring and Evaluation*...................Sh. 532,414,300
Kifungu 1004 - *Advocacy and Information Unit*..........Sh. 920,920,070
Kifungu 1005 - *National Response*.............................Sh. 8,432,114,603
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*...........Sh. 16,230,000
Kifungu 1007 - *Legal Services Unit* ...............................Sh. 770,763,039
Kifungu 1008 - *Management Information Systems Unit*………………………………..Sh. 67,480,000
Kifungu 1009 - *Internal Audit Unit* ...................................Sh. 22,540,000
Kifungu 1010 - *Special Programs Unit*............................Sh. 60,000,000
Kifungu 1011- *Government Communication Unit*.......Sh. 119,650,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa hoja kwamba, kwa mujibu ya Kanuni ya 123(3)(a) na (b) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu lilikaa kama Kamati ya Matumizi limemaliza kazi zake. Naomba sasa taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Wote wameafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Nachukua nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri unayofanya wewe na timu yako na kwa majibu mazuri ya Serikali ambayo mmetoa leo kuwaridhisha na kuwafahamisha wananchi mambo ambayo Serikali ya Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia inaifanya. Hongereni sana. *(Makofi)*

Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu na leo tumekamilisha bajeti hii ya Ofisi ya Waziri

Mkuu, hongereni sana Serikali na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.16 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 16 Aprili, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*